**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 23 Julai, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:**Waheshimiwa Wabunge, karibuni tena wiki nyingine ya kazi baada ya shughuli nzima iliyofanyika siku ya Jumamosi, napenda kuwapongeza wote waliofanikisha siku ile. (*Makofi*)

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA :** Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Taarifa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2007/2008.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:** Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2007/2008.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 263

**Ujenzi wa Makao Mapya ya Polisi Muheza**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI** aliuliza**:**

Kwa kuwa, Serikali kupitia Wizara ya Usalama wa Raia ilianza ujenzi wa Makao Makuu Mapya ya Polisi Wilayani Muheza mwaka wa fedha 2004/2005, kazi

ambayo imesimama kwa sasa, na kwa kuwa majengo yanayotumiwa sasa ni mali ya Shirika la Reli Tanzania:-

(a) Je, ni Lini ujenzi huo utaendelezwa na kukamilika?

(b) Kwa kuwa, Serikali ilishauriwa kuhamisha umiliki wa majengo ya Makao Makuu ya zamani na nyumba za Polis kutoka Shirika la Reli kwenda Wizara husika kabla ya ubinafsishaji au ukodishaji wa Shirika hilo kukamilishwa. Je, jambo hilo limetekelezwa kwa kiwango/hatua gani hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza Ujenzi wa Makao Makuu Mapya ya Polisi Wilaya ya Muheza Mwaka wa Fedha 2004/2005. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Herbert James Mntangi kwamba ujenzi wa Kituo hicho ulishakamilika na Kituo kukabidhiwa kwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Tanga tangu tarehe 16 Novemba, 2006. Kwa sasa hatua za kuunganisha umeme katika kituo hicho zinaendelea.

Hata hivyo, kutokana na miundombinu hafifu ya maji, Kituo hakina maji. Jeshi la polisi linafanya jitihada ya kuchimba visima virefu ili kukipatia kituo maji kwa ajili ya matumizi ya kila siku, na matarajio yetu ni kukamilisha zoezi hili katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepokea ushauri wa Mheshimiwa James Herbert Mntangi, juu ya kuhamisha umiliki wa majengo ya Makao Makuu ya zamani na nyumba za Polisi kutoka Shirika la Reli kwenda Wizara ya Usalama wa Raia. Wizara yangu inaahidi kufuatilia suala hilo kwa Wizara husika. Aidha, tunamshukuru Mheshimiwa James Mntangi kwa ufuatiliaji wake wa karibu kuhusu makazi ya Askari Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa James Herbert Mntangi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ametoa. Hata hivyo nina swali moja dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa, kabla ya Wilaya ya Muheza kugawanyika kati ya Wilaya ya Muheza na Mkinga vilikuwepo vituo vitano (5) vya Polisi vitatu (3) vikiwa Mkinga na viwili (2) vikiwa Muheza. Sasa hivi Muheza imebakia na Makao Makuu na kituo kidogo sana kule Amani ambapo hakiko katika hali nzuri. Je, Wizara inasema nini kuhusu kuongeza vituo vya Polisi katika Wilaya ya Mheza hasa katika eneo ambalo lina uzalishaji mkubwa wa matunda kule katika Kata ya Mtindiro. Lakini vilevile kusaidia kuboresha kituo cha Polisi cha Amani ambapo eneo kubwa la utalii?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa James H. Mntangi kwa namna anavyofuatilia masuala haya ya Askari wetu na anavyotaka kuhakikisha kwamba vituo vya Polisi vinajengwa ili kutoa huduma karibu zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimjibu Mheshimiwa Herbert James Mntangi, kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, nia ya Serikali ipo ya kujenga vituo zaidi katika Jimbo la Mheshimiwa Mntangi na vituo ambavyo tunakusudia kuvijenga ni Kigombe, Kicheba, Gwembela, Songa Mabatini, Mkunzi na Mtindililo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, tunakuomba uvute subira huku tukishughulikia hilo.

Suala la Polisi Amani ni kwamba tuna utaratibu wa kukifanyia ukarabati ili kiwe katika hali nzuri zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyohiyo, Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud.

Na. 264

**Majengo ya Polisi**

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, majengo mengi ya Askari Polisi ziwani amechakaa sana kiasi cha kushusha hadhi ya majengo hayo:-

Je, Serikali itafanya lini ukarabati wa majengo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud Mbunge wa Jang'ombe kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Soud kwamba majengo mengi ya Askari Polisi ya Ziwani, Zanzibar yanahitaji ukarabati.

Hata hivyo, tatizo hili si la Kambi ya Ziwani pekee bali ni la nchi nzima. Serikali inaendelea kuyashughulikia awamu kwa awamu matatizo mbalimbali ya Jeshi la Polisi yakiwemo matatizo ya uchakavu wa Ofisi na Kambi za Askari ili kuboresha mazingira ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kukarabati na kujenga majengo mapya ya Askari Polisi yakiwemo ya Ziwani

Zanzibar.Aidha, Serikali imeshasaini mkataba wa kujenga maghorofa 30 na *NSSF*. Kambi ya Polisi Ziwani imo katika mpango huo.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud.

**MHE. MOHAMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwanza napenda nimpongeze kwa hatua hiyo na nitafurahi zaidi nikiona utekelezaji umeanza mapema.

Lakini swali la pili, kwa kuwa Ziwani ni kambi kubwa na inachukua Askari wengi lakini ukiangalia hawana sehemu inayoweza kuwawezesha kuangalia angalau *TV* na masuala mengine. Je, ni lini atawawekea sehemu hiyo ili waweze kuwa pamoja muda waote?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mohamed Rajab Soud naomba kwanza naye nimpongeze sana kwa jitihada zake za kupigania Askari wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inawapa moyo vijana wetu na mmeona juzi namna walivyopambana kule Arusha. Kwa hiyo, mimi napenda nichukue fursa hii niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud kama ifuatavyo:-

Kwanza napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud kwamba kwa kuwa maandalizi yote yamekamilika wakati wowote sasa ujenzi wa majumba yale pale Ziwani utaanza na vilevile tutajenga majumba 25 pale Kurasini, Dar es Salaam.

Kuhusu suala la *Welfare* tupo katika mpango na ninataka kumhakikishia Mheshimiwa kwamba katika ujenzi huu sehemu ya *Welfare* itakuwepo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Majibu mengi yatatokea kwenye hotuba ya Waziri kwa hiyo tunaendelea, na tunaendelea na Wizara ya Miundombinu. Mheshimiwa Ramadhan A. Maneno.

Na. 265

**Hitaji la Huduma ya Mawasiliano ya Simu - Sadani**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza :

Kwa kuwa, Sadani imepata hadhi ya kuwa Hifadhi ya Kitaifa ya Kiutalii, na kwa kuwa kuna vivutio vingi vya kitalii vilivyowafanya watalii wengi kutembelea maeneo hayo na hivyo kutuongezea pato la Taifa, na kwa kuwa, kuna tatizo la ukosefu wa mawasiliano ya simu ;

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya Simu katika maeneo hayo ?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI**) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshiwa Ramadhani Athumani Maneno, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo;

Kampuni ya Simu Tazania yaani *(TTCL)* ina mpango kabambe wa kusambaza mawasiliano katika Wilaya zote nchini ikiwa ni pamoja na maeneo muhimu ya vijijini. Mpango huu utaweka mtandao wa mitambo inayotumia teknolojia ya *Code Division Multiple Access* (*CDMA*) na awamu ya kwanza ya utekelezaji ilianza mwishoni mwa mwaka 2006 kwa kujenga mitambo ya kurushia simu maeneo yote ya mijini ikiwa ni Makao makuu ya Mikoa, Wilaya na maeneo machache ya vijijini. Utekelezaji wake unaendelea na unategemea kumalizika mwezi Desemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sadani ni mojawapo ya maeneo muhimu yatakayofaidika na mradi huu ifikapo mwishoni mwa mwaka huu 2007 ambapo mnara wa kurushia mawasiliano na mitambo ya *CDMA* itajengwa ili kutoa huduma ya mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Celtel* katika kuhakikisha kwamba inadumisha shughuli zake katika maeneo mbalimbali nchini, ina mpango wa kupeleka huduma zake katika maeneo ya Hifadhi ya Kitaifa ya Sadani ifikapo mwezi Septemba, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *MIC (Tigo)* kwa sasa haina mawasiliano ya simu katika maeneo ya Hifadhi ya Kitaifa ya Sadani, hata hivyo, kutokana na maombi ya Mheshimiwa Mbunge Kampuni hiyo itafanya uchunguzi wa kitaalamu na kujumuisha maeneo hayo katika mipango yake ijayo ili wananchi wa maeneo ya Hifadhi hiyo pamoja na watalii waweze kunufaika na huduma hiyo muhimu.

**NAIBU SPIKA:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Mgana I. Msindai.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, wananchi wetu wengi wameitikia mwito wa kupokea hizi simu za mikononi je, Serikali sasa haioni upo umuhimu sana kwa kuhimiza hizi simu zienee mahali pengi hasa kipindi hiki ambacho wananchi wanapata mikopo na kuendesha biashara zao kwa hiyo mahitaji kuwasiliana na wengine na hizi simu zikienda huko vijiji vikiwepo vijiji vya Kinyangili, Mwangeza, Mkalakala na Matongo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI**): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, kama ifuatavyo;

Nashukuru na ninakubaliana na Mheshimiwa Mgana I. Msindai umuhimu wa simu vijijini ili wananchi wapate taarifa na kuweza kupeleka taarifa ipasavyo katika harakati hizi za kiuchimu.

Napenda nimhakikishe Mheshimiwa Mgana I. Msindai kwamba nia ya Serikali na Sera ya Simu ni kupeleka simu vijijini. Juzi na jana tulikuwa katika Wilaya ya Manyoni na tulitembelea katika vijiji kama 6 na katika vijiji hivyo 6 Mheshimiwa Mgana I. Msindai kama utakumbuka Kijiji kimoja cha Londoni ambacho ulikuwa unakilalamikia sana tulipata nafasi ya kukitembelea na kule tuna nia ya kupele huduma za simu.

Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba vijiji alivyovitaja vitafikiwa muda ukifika, nawomba awe na subira kwa sababu huduma hizi za mawasiliano ya simu makampuni yanajitahidi ni nichukue nafasi hii niwashukuru sana, sana.

**MHE. PHARES KASHEMEZA KABUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la Chalinze linafanana na matatizo ya Biharamulo, ni lini kampuni za simu zitashawishika kupeleka huduma hiyo katika vijiji vya Runazi, Nyakanazi, Nyakahura na Rusahunga?

**NAIBU SPIKA:** We sema Biharamulo tu huko kote hakujui. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI**): Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, kama ifuatavyo:-

Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Phares K. Kabuye kwamba mimi mwenyewe ndiye niliyeweka jiwe la msingi kule Biharamulo na nina hakika vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vitafikiwa kwa wakati muafa.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na swali lingine katika Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

Na. 266

**Uuzaji wa Nyumba za Serikali**

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO** aliuliza:

Kwa kuwa, Serikali iliamua kuwauzia wafanyakazi wa Serikali baadhi ya nyumba:-

(a) Je, ni wafanyakazi wangapi wanaofanya kazi katika Balozi zetu nje ya nchi wamepewa nyumba hapa nyumbani au kuuziwa nyumba wanazoishi nje ya nchi?

(b) Je, ni wanasiasa wangapi ambao si wafanyakazi wa Serikali, na ni wananchi wangapi ambao si wanasiasa au wafanyakazi wa Serikali wameuziwa nyumba hizo?

(c) Je, ni wastaafu wangapi walioamua kujihusisha na siasa wamepewa au kuuziwa nuumba hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa utekelezaji wa jukumu hili la kuuza nyumba kwa watumishi wa umma ni wafanyakazi saba tu wanaofanya kazi kwenye Balozi zetu nje ya nchi walioweza kuuziwa nyumba za Serikali. Hata hivyo, hakuna nyumba ya Serikali iliyopo nje ya nchi iliyouzwa kwa wafanyakazi kwenye Balozi hizo. Hatua hii imetokana na ukweli kuwa Serikali yetu bado ina mahitaji makubwa sana ya nyumba za kuishi watumishi wetu nje ya nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kuondokana na gharama kubwa za matengenezo ya nyumba hizo, lengo lingine la Serikali kuwauzia watumishi wa umma ambao wanaishi katika nyumba ambazo zimeainishwa kuuzwa, lilikuwa ni kuwasaidia watumishi hao wa umma kupata makazo bora na ya uhakika wakati wote wakiwa kazini na baada ya kustaafu kazi, hivyo hakuna wananchi wa kawaida au mwanasiasa yeyote ambaye si mfanyakazi wa Serikali aliyuziwa nyumba za Serikali, labda mwanasiasa huyo awe pia anatumikia Serikali wakati huo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mikataba ya kuuza nyumba za Serikali, mtumishi wa umma aliyeuziwa nyumba, hana budi kukamilisha malipo kabla hajastaafu. Kwa mantiki hiyo, hakuna wastaafu walioamua kujihusisha na siasa ambao wamepewea au kuuziwa nyumba hizo. Hata hivyo, kama kuna watumishi waliouziwa nyumba ndani ya utumishi wao na bada ya kustaafu wakaamua kujihusisha na siasa, hatuna orodha yao kwa vile Wizara yangu haifuatilii watumishi waliostaafu ili kujua wanafanya nini baada ya kuondoka kwenye utumishi wa umma.

**MHE. PHILEMON NDESAMBURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ambao wameuziwa nyumba hizi na ambao wako katika ajira ya Serikali lakini wanakaa katika nyumba za kupangisha na nyumba zile

wamezipangisha kwa watu. Je, huku si kukiuka makubaliano na siyo wakati muafaka Serikali ifute ule mkataba na nyumba zile zirudishwe Serikalini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Pili, kwa kuwa tuna upungufu wa nyumba za wafanyakazi wa Serikalini katika Vituo na sehemu nyingine unakuta nyumba hizi walizokuwa wameuziwa wafanyakazi wa Serikali ni tupu au wamezipangisha kwa watu ambao si wafanyakazi wa Serikali. Je, Siyo hekima nyumba hizi wakazirudisha Serikalini kupangisha Serikali ili ziweze kupunguza matatizo ya wafanyakazi wa Serikalini ili ziweze kutumika?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, kwa pamoja kama ifuatavyo:

Katika mkataba wa kuuza nyumba hizi kitu ambacho kiliwekewa mkazo ni kwamba nyumba zile aliyeuziwa hataruhusiwa kuuuza ndani ya miaka 25, mengine yote kwamba anafanya ukarabati na nyumba bado iko tupu au ameweka ndugu yake au amefanya nini hayamo kwenye mkataba.

Lakini la msingi ni kwamba ile nyumba isiuzwe. Haya mambo ya kupangisha na mengineyo hayakuwepo kwenye mkataba na hatuwezi kuwa na hakika kwamba amepangisha au amemweka ndugu yake anakaa wakati anaendelea kuihudumia na kwamba nyumba imeonekana tupu inawezekana bado ana mipango ya kuikarabati huwezi kusema kwamba sasa haitaki kwa sababu kama angekuwa haitaki asingeomba na asingelilipia sidhani kwamba mtu unaweza kuilipia nyumba halafu bado ukaitelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, atakuwa amenielewa kwamba utaratibu ulikuwa ni huo na hakuna mahali ambapo pamekiukwa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri ametaja hapa kwama hana list kamili ya hao watu ambao wamekabidhiwa na jibu hilo ndilo alilonipa wakati anajibu swali langu kama hilihili hapa Bungeni na kwa kuwa katika utekelezaji wa Shughuli hii bado kuna watu wanakaa na wanatumia fedha za wananchi kwa mfano pale *Courtyard.* Sasa je, kwa vile Waziri aliahidi ndani ya Bunge hili kwamba kuna Kamati imeundwa na Serikali na kuwa Kamati hiyo itakapomaliza kazi yake wataleta taarifa hapa Bungeni. Je ni lini sasa Kamati hiyo itamaliza kazi yake na taarifa italetwa Bungeni?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kama ifuatavyo:-

Si kweli kwamba tulisema kazi hiyo itakapokamilika kwamba itakuja Bungeni, tulichosema ni kwamba Kamati inafanya kazi na tutakuwa tunachukua hatua za kurekebisha maeneo ambapo hatua hizi au hizi taratibu za uuzaji zilikiukwa na hayo yameendelea kufanyika pale ambapo kuna dosari tunarekebisha na ndivyo inavyoendelea.

Kwa hiyo, la kusema kwamba *list* ya watu waliouziwa hakuna wala sikusema hivyo vilevile lakini tulisema kwamba kwa sababu ni ndefu kama Mheshimiwa Mbunge anataka kuona watu wote waliozuwa akija ofisini tunaweza tukamwonyesha.

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo swali linaulizwa na

Na.267

**Ujenzi wa Barabara ya Ferry – Pemba Mnazi**

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kupanua barabara kutoka Feri-Pemba Mnazi kwa kiwango cha lami?

(b) Je, wananchi ambao nyumba au mazao yao yatakumbwa na ujenzi/upanuzi huo watalipwa fidia husika?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu naomba kwa kujibu swali la Mheshimiwa Mwinchoum Abdulrahman Msomi, Mbunge wa Kigamboni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kivukoni (Feri) – Pembamnazi yenye urefu wa kilometa 56.4 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara Mkoa wa Dar es Salaam. Katika barabara hiyo, sehemu ya Kivukoni – Mjimwema (Mwongozo) yenye urefu wa kilometa 9.4 iko katika kiwango cha lami. Nayo sehemu ya Mwongozo- Kimbiji – Pembamnazi yenye urefu wa kilometa 47 iko katika kiwango cha changarawe.

Serikali itaendelea kutafuta fedha za kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kivukoni – Mjimwema –Pembamnazi, kadri hali ya upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu. Kiasi cha shilingi 84,068,000/= zimetengwa kwa ajili ya kuongeza tabaka la pili la lami nyepesi kwenye urefu wa kilometa 2.2 toka Mjimwema hadi

Mwongozo. Aidha, upanuzi wa barabara hii utafanyika kadri bajeti itakavyoruhusu na kwa kuzingatia viwango vya upana wa barabara za Mikoa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya fidia kwa wananchi watakaokumbwa na ujenzi au upanuzi utazingatiwa kwa majibu wa sheria ya barabara.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa vile, Barabara hii inavyotaka kupanuliwa kuna baadhi ya nyumba ambazo zimeingizwa katika *road reserve* bila matarajio. Je, kama zile nyumba ambazo haziko katika matarajio ya kuingizwa kwenye matarajio je watalipwa fidia wale ambao tayari wameshavunjiwa nyumba zao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON MAKONGORO MAHANGA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir kama ifuatavyo;

Hakuna nyumba iliyovunjwa ambayo haipo katika *road reserve,* isipokuwa kulikuwa na malalamiko kwamba wengine waliwekewa X" nje ya *road reserve.* Hili tunaliangalia kama kuna mwingine aliwekewa X' basi tutawajulisha kwamba hiyo X ilikosewa, lakini wale ambao wako kwenye hifadhi ya Barabara kwa mujibu wa Sheria hawatafidiwa.

Na. 268

**Matumizi ya Dawa za Kuchubua Ngozi**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna baadhi ya wananchi ambao wanapendelea kutumia dawa za kuchubua ngozi (*skin dye*) na inasemekana kuwa, dawa hizo husababisha madhara makubwa kwa afya za watumiaji:-

(a) Je, ni madhara ya aina gani yanayosababishwa na utumiaji wa dawa hizo?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba, dawa hizo zimesambaa kwenye masoko yetu licha ya kwamba zimepigwa marufuku?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi ili kuinusuru jamii kutokana na matumizi ya dawa hizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye vipengele (a), (b), (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kuwa matumizi ya dawa za kuchubua ngozi hususan zile zenye viambata vya sumu husababisha madhara kwa watumiaji. Naomba kutaja baadhi tu ya madhara yatokanayo na matumizi ya vipodozi vyenye sumu kama ifuatavyo:-

1. Ngozi kuwa na mabaka meusi na meupe na kukunjamana.

2. Ngozi kuwa nyembamba sana na laini na endapo itapata jeraha halitapona haraka.

3. Kutokwa na chunusi kubwa kubwa.

4. Kupata mzio (*allergy*) wa ngozi.

5. Muwasho na athari kwenye ngozi endapo itapata mwanga wa jua.

6. Madhara katika ubongo, figo, ngozi, maini, mapafu n.k.

7. Kupoteza fahamu mara kwa mara.

8. Kusababisha saratani ya damu, ngozi, maini, ubongo, mapafu na kadhalika.

9. Mama mjamzito anayetumia vipodozi hivyo kwa muda mrefu huweza kusababisha mtoto wake kuathirika akiwa bado tumboni. Pia kuna uwezekano mkubwa wa kuzaliwa mtoto mwenye mtindio wa ubongo.

(b) Serikali inafahamu kwamba dawa hizo bado zimesambaa kwenye masoko yetu licha ya kwamba zimepigwa marufuku. Sababu kubwa ni kwamba baadhi ya wafanyabiashara wa dawa hizo (vipodozi) wamekuwa wakiziingizwa nchini kwa njia za kificho yaani kwa kutumia njia zisizo halali na kuendelea kuziuza madukani kwa njia za vificho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa zipo aina 933 tu za vipodozi ambavyo vimethibitishwa kuwa na ubora na usalama kwa afya ya watumiaji. Vipodozi hiyo ndivyo vinavyoruhusiwa kuuzwa nchini.

(c) Hatua zinazochukuliwa na Serikali ili kuinusuru jamii kutokana na matumizi ya dawa (vipodozi) zenye viambato vya sumu ni kama ifuatavyo:-

1. Serikali imepiga marufuku matumizi ya aina 182 za vipodozi vilivyothibitika kuwa na sumu.

2. Serikali inawataka wafanyabiashara wa vipodozi, yaani waingizaji na watengenezaji kutoa taarifa za viambato vyote vinavyotumika katika kutengenezea vipodozi vyao.

3. Serikali imeendesha semina mbalimbali kwa wadau ili kuwaelimisha kuhusu kazi za Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA)* katika udhibiti wa vipodozi na orodha ya viambato vya sumu vilivyopigwa marufuku ilitolewa.

4. Serikali imetengeneza Kanuni za udhibiti wa vipodozi kwa kushirikisha wadau wa vipodozi.

5. Serikali inadhibiti ubora na usalama wa vipodozi kwa kufanya tathmini ya taarifa za kisayansi na uchunguzi wa kimaabara kabla ya kuvisajili na kuviruhusu kuingizwa nchini. Aidha, Serikali huchukua sampuli mbalimbali za vipodozi katika soko na kuvifanyia uchunguzi wa kimaabara ili kubaini viambato vilivyotumika kutengeneza vipodozi husika.

6. Serikali hufanya ukaguzi katika vituo vya mpakani na maduka ya vipodozi kwa kushirikiana na wasimamizi wa sheria kutoka taasisi nyingine za umma kama vile Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

7. Serikali imeendelea kutoa elimu ya matumizi sahihi ya vipodozi kwa wananchi, na mfano hai ni jarida la madhara ya vipodozi liitwalo. Je, nitapendeza? Ambalo lilizunduliwa tarehe 6 Septemba, 2006.

**MHE. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa vipodozi hivyo vinaathiri kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyojibu. Je, kuna uhusiano gani wa vipodozi hivi kuharibika kwa ngozi na uhusiano wa kuota ndevu kwa wanawake kunakozidi? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna akinamama wanaoota ndevu wakati wanapotumia vipodozi hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba katika vipodozi vingine unakuta kuna aina ya dawa kama *hormones* ambazo huleta kuota kwa ndevu kwa akinamama iwapo watazitumia, kwa sababu zile ni *hormones* ambazo zinapatikana katika miwili ya wanaume. Kwa hiyo, kama watatumia zile dawa ambazo zina *hormones* zile basi zinaweza kusababisha kuota kwa ndevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda nichukue nafasi hii kuwakumbusha wananchi kwamba watumie dawa za vipodozi ambazo hazina viambato

vya sumu. Lakini vilevile napenda kuifahamisha jamii kwamba kuwa mweupe siyo kwamba ndiyo uzuri. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa mwaka 2005/2006 kitengo cha *Tanzania Food and Drug Authority* kilionyesha kasi kubwa katika kudhibiti vipodozi hivyo. Lakini kwa mwaka huu vipodozi hivyo vimeendelea kuonekana kwenye maduka. Je, kasi hiyo ya *TFDA* imeishia wapi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba kasi ya *TFDA* kukagua vipodozi imepungua. Kasi imeongezeka kwa sababu nilizotaja katika jibu langu la msingi ni kwamba kuna baadhi ya wauzaji ambao wanauza dawa hizo kwa kificho. Lakini vilevile napenda niseme kwamba kasi hiyo imeongezeka kwa sababu wananchi au watumiaji wale hawapendi kusikiliza na kufuatilia ushauri wanaopewa na wataalam ndiyo maana wanaendelea kuzitumia dawa hizo. Lakini hata hivyo, *TFDA* kwa kushirikiana na Mamlaka ya *TRA,* lakini vilevile na TAMISEMI wamekuwa wakifanya ukaguzi wa hapa na pale wa kushtukiza na kukamata dawa hizo ambazo zina viambata vya sumu.

Na. 269

**Mradi wa Umeme wa Makongorosi na Lupa Tingatinga**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwaka 2002, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ilianza utekelezaji wa mradi wa umeme unaounganisha Miji Midogo ya Makongorosi na Lupa Tingatinga Wilayani Chunya; na kwa kuwa, mradi huo utasaidia kuleta Maendeleo na pia utatoa njia mbadala ya kukausha Tumbaku katika maeneo hayo na hivyo kutunza mazingira:-

(a) Je, ni sababu zipi zinazosababisha mradi huo kutokamilika mpaka sasa?

(b) Je, wananchi wa Mamba, Lupa Tingatinga , Mtanila na Matwiga wategemee mradi huo kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b), naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kupeleka umeme Makongorosi, Lupa na Tingatinga Wilayani Chunya, gharama zake zimekadiriwa kuwa shilingi milioni 660. Mradi huo unajumuisha ujenzi wa kilomita 44 za njia ya umeme msongo wa kilovoti

33, ujenzi wa kilomita 12 za njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 na ujenzi wa vituo vinne vya kupoza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ufinyu wa Bajeti, ni shilingi 24,229,348 tu zilizotolewa kwa njia ya utekelezaji wa mradi huo, hivyo kufanya Maendeleo ya mradi kuwa madogo. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni usimikaji wa nguzo 180 umbali wa kilomita 17 na ufungaji wa vyuma na vikombe (*insulators*) juu ya nguzo 42 kwa umbali wa kilomita 4.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa mradi wa kupeleka umeme Makongorosi, Lupa na Tingatinga Wilayani Chunya kunatokana na ukosefu wa fedha uliosababishwa na ufinyu wa Bajeti ya Serikali na pia hali mbaya ya kifedha ya Shirika la *TANESCO.*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mamba, Lupa Tingatinga, Mtanila na Matwiga wategemee kuwa mradi huo, kama ilivyo miradi mingine ya umeme ambayo imeshaanzishwa, itaendelea kutekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha chini ya Wakala wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Agency*) pamoja na mfuko wake.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana na fasaha

La kwanza kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba mwaka huu zimetengwa bilioni 10 katika Mradi wa *Rural Electrification Agency* atawahakikishia wananchi wa Wilaya ya Chunya kwamba mradi huo wa Makorongosi mpaka Lupa utaanza kwa kutumia hizo bilioni 10?

La pili, kwa kuwa, *TANESCO* mjini Chunya ina gari moja la lori ambalo linazidi ya miaka 20 ni *spare* mkononi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atawahakikishia wananchi wa Chunya kwamba watapatiwa gari lingine la kufanyia miradi hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo amekuwa akiwasiliana na Wizara yetu hasa kufuatilia maendeleo si tu ya Nishati, lakini pia na masuala mengine yanayohusiana na Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia na swali la kwanza la nyongeza. Kama ambavyo ilijitokeza wakati tunawasilisha Bajeti yetu na kama ambavyo tumekuwa tukirudia kusema hapa katika Bunge lako Tukufu. Wizara yenu ina nia ya kuanza na miradi ambayo imeshaanzishwa kuitekeleza kwa kupitia huu Mfuko wa Nishati Vijijini.

Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule ni kati ya miradi ambayo itapewe kiupambele wakati wa utekelezaji mara Mfuko huo utakapoanza. Kwa sababu ndiyo dhamira ya Serikali, kwanza ni miradi ambayo imeshaanzishwa kabla hatujaanza kutekeleza miradi mingine mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili, kuhusu hilo gari ambalo ni la muda mrefu. Tunaheshimu na tunathamini sana maoni na ufuatiliaji wa Mheshimiwa Mbunge na hivi niseme tu kwamba tutawasiliana na Shirika letu la *TANESCO* kama kwenye Kasma zao tunaweza kuwapatia *TANESCO* Wilaya ya Chunya gari lingine ili kuweza kurahisisha huduma za huko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. YONO S. KEVELA**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala la kule Chunya ni sawasawa na la Wilaya ya Njombe kuhusu *grid* ya Taifa ya umeme. Kwa kuwa vikombe na nguzo zimeishafungwa katika vijiji vya Kindugara na Waging'ombe katika Wilaya ya Njombe.

Je, ni lini umeme huo utawashwa kwa sababu kila kitu kimeishakamilika?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza wakati nawasilisha Bajeti yangu ya mwaka 2007/2008, kipaumbele chetu cha kwanza ni kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya zote. Hicho ndicho kipaumbele cha kwanza katika umeme vijijini. Lakini kama tulivyoelezwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka huu tumeanza na vipaumbele vya Sekta ya Elimu, Sekta ya Kilimo na Sekta ya Miundombinu.

Lakini mwaka ujao Sekta ya Nishati na yenyewe itafikiriwa. Katika mipango hiyo ndiyo vijiji vyote hivyo tulivyokuwa tunazungumza tutaanza kuviwekea kipaumbele kwa kuanzia na miradi iliyokwishaanza kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri.

Na. 270

**Umeme wa BIOGAS**

**MHE. SAID J. NKUMBA (K.n.y. MHE. AZIZA S. ALLY)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali inafahamu kuwa upo uwezo wa kupata umeme kwa kutumia *BIOGAS;* na kwa kuwa, viko vijiji ambavyo havina umeme:-

Je, Serikali haioni sasa kuwa, kuna haja ya kutoa elimu kwa wananchi ili waelewe utaratibu wa kuandaa na kupatikana kwa umeme huo kuliko kusema kwa maneno bila vitendo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, kabla ya kujibu swali la Mheshimwia Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, bayogesi ni chanzo cha nishati ipatikanayo kwa kuozesha aina zote za tungamotaka (*biomass*), hasa kinyesi katika mchanganyiko ambao unatakiwa uwe na kiasi kidogo sana cha hewa ya oksijeni (*anaerobic digestion*). Bayogesi inajumuisha asilimia 60 ya *methane* na asilimia 40 ya hewa ya ukaa (*carbon dioxide*). Bayogesi inaweza kutumiwa majumbani kwa kupikia na kutoa mwanga wa taa. Ili kutumia biogesi katika kupikia inabidi uwe na *digestor*. Hapa nchini hutumika *digestor* zinazojengwa kwa matofali na kwa plastiki . Gharama zake hutegemea aina na uwezo wa *digesto*r. Hata hivyo, *digestor* zinazojengwa na matofali zinafaa zaidi kwa wananchi wengi wa vijijini hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuzalisha umeme wa bayogesi inabidi kuwa na tungamotaka, maji ya kutosha, injini (*Internal combustion engine*) na jenereta. Ni bora kutumia bayogesi moja kwa moja kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya kupikia na mwanga, badala ya kuzalishia umeme. Uzalishaji wa umeme kutokana na bayogesi unafaa pale penye wingi wa tungamotaka za viwandani kama mabaki ya miwa na mkonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika maelezo ya utangulizi, uzoefu unaonesha kuwa ni bora kutumia bayogesi moja kwa moja kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya kupikia na mwanga, badala ya kuzalishia umeme kwani uzalishaji wa umeme kutokana na bayogesi unahitaji kiasi kikubwa cha tungamotaka na hivyo kufaa tu katika viwanda vinavyozalisha taka kwa wingi kama viwanda vya miwa na mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inahamasisha kuratibu matumizi ya bayogesi hasa kwa ajili ya kupikia majumbani kama mkakati mmojawapo wa kupunguza matumizi ya kuni na mkaa. Katika kufanya hivyo, Wizara ilijenga mambo wa majaribio (*pilot scheme*) wa kusukuma maji ya kisima kwa kutumia teknolojia ya bayogesi, kwa kushirikiana na *GTZ* kule Nsasa, Dodoma mwaka 1987.

Aidha, Wizara yangu inaratibu Maendeleo ya teknolojia ya bayogesi inayoendelezwa na taasisi mbalimbali zikiwemo Kituo cha Zana Kilimo na Teknolojia Vijijini (*CAMARTEC)* cha Arusha, Miradi ya Gesi ya Samadi Dodoma (*MIGESADO)*; Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT); na Asasi nyingine zisizo za Serikali. Chini ya Taasisi hizo hapa nchini kumejengwa zaidi ya *digestor* 6,000 na hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza Afrika katika uenezaji wa teknolojia hii katika kupikia majumbani.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa Serikali imekuwa inaacha mambo muhimu kama haya kwa Mashirika yasiyo ya Kiserikali kama alivyokuwa amejibu swali la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri hapa; na kwa kuwa maisha bora kwa kila Mtanzania hasa huko vijijini yatachochewa sana na matumizi mbalimbali ya nishati ikiwemo Bayogesi. Je, sasa Serikali inaweza kusema nini kuhusu zile fedha bilioni 10 zilizotengwa zielekezwe huko vijijini ili zikaanzishe mitambo midogo midogo ya bayogesi ambayo inaweza kusaidia kuleta Maendeleo ya matumizi ya nishati huko vijijini?

Pili, kwa kuwa baadhi ya ushuru wa vifaa vya *solar* uliondolewa na Serikali ili wananchi hasa wa vijijini waweze kununua vifaa hivyo kwa gharama ya chini, lakini mpaka sasa hivi bado vifaa hivyo na uunganishaji wa vifaa hivyo vijijini bado ni wa gharama kubwa sana. Je, Serikali inasema nini juu ya suala hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niseme tu kwamba Wizara na Serikali kwa ujumla si kwamba zimeacha kutekeleza au kufuatilia mambo haya ya msingi. Nadhani imeshajitokeza mara kadhaa na ufafanuzi umeishatolewa mara nyingi tu kwamba kuna miradi mingi ambayo inaenda sambamba na hii miradi mingine ya utekelezaji kwa ajili ya nishati kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu na wananchi wa ujumla kwamba Serikali inaendelea na mikakati yote kwa pamoja kwa njia mbalimbali na kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwamba Serikali majukumu yake makubwa hasa ni kuhamasisha na kushirikiana na wadau wengine zikiwemo Asasi zisizo za Serikali na kuratibu zoezi nzima la usambazaji wa nishati hapa nchini. Lakini kibiashara Serikali kutokana na sera zake kimsingi haishiriki moja kwa moja katika maeneo mengi ila ni kwa baadhi tu ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha bilioni 10 ambacho kimejitokeza hasa ambacho tunatarajia tukitumie hasa katika kusambaza umeme kupitia Mfuko wa Usambazaji Nishati Vijijini una malengo yake hasa kwa miradi ambayo tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na ile mingine ambayo tunaendelea kuifanyia kazi.

Lakini kwa hili kwamba tukijite kwa kutumia hizo fedha kueneza nishati mbadala, zipo njia zingine na Serikali inaendelea kuzifanyia utekelezaji kwa kupitia washirika mbalimbali ili tuweze kueneza hiyo nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, pamoja na kwamba Serikali ilishatoa unafuu hasa wa ushuru kwa bidhaa mbalimbali au vifaa mbalimbali ambavyo vitasaidia kueneza nishati mbadala.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge kama kuna tukio analolifahamu kwamba liliishajitokeza na bado akaona kwamba wananchi katika maeneo waliyotarajiwa kupata unafuu hayatekelezwi basi awasiliane na Wizara yetu ili tujaribu kufuatilia ni kwa vipi. Kwa sababu dhamira ya Serikali ni kupunguzia wananchi gharama hizo ili waweze kueneza hizo huduma kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namkaribisha Mheshimiwa Mbunge kama kuna mambo ambayo anahisi hayajatekelezwa na unafuu haujapatikana kwa kiwango kikubwa. Kwa sababu pia tumekuwa na maoni ya upande wa pili kwamba kweli baada ya kutekeleza hiyo fursa ya kutoa unafuu, tunaona huduma zinaendelea, lakini niseme tu kwamba huduma zinazotolewa ni pamoja na kuzingatia gharama zinazotumika. Kwa hiyo, namkaribisha Mheshimiwa Mbunge kama kuna mahali ambapo bado anaona kuna dosari tuendelee kuirekebisha.

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa matumizi ya nishati inayotokana na samadi ya ng'ombe si jambo la kufanyiwa majaribio kwani ni jambo ambalo linajulikana na utaalam wake unajulikana. Je, Serikali inaweza kukubaliana kwamba suala la kuhimiza na kuchagua baadhi ya viwanda ambavyo vingeweza kutengeneza vifaa vidogo vidogo na kuviuza kwa wakulima ingekuwa ni muhimu ili nishati hiyo ienezwe kila mahali palipo na mifugo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo kama hayo ya Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, ni mazito na ni muhimu sana kwa Maendeleo ya nchi yetu hasa kwenye suala la nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkaribishe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine na wananchi kwa ujumla wenye mawazo kama hayo tuyafanyie kazi. Ni mambo ambayo hatuwezi kuyaacha kwa sababu yanalenga kusaidia jamii yetu. Lakini kimsingi tunakubali kabisa kwamba matumizi ya nishati hasa inayotokana na samadi ni jambo la msingi; na kwa kweli kuna miradi ambayo inaendelea kutekelezwa na Serikali kupitia chanzo hicho cha nishati.

Na. 271

**Ufunguzi wa Uwanja wa Taifa**

**MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MHE. SUSAN A. J. LYIMO)** aliuliza:-

(a) Kwa kuwa, Serikali ina mpango wa kuileta timu ya *Real Madrid* kutoka Hispania kwa ajili ya ufunguzi wa Uwanja Mpya wa Taifa; na kwa kuwa, timu hiyo imetoa masharti magumu kuwa ni pamoja na *direct flight* kutoka Hispania – Dar e Salaam mbuga za wanyama na kuishia katika Hoteli ya Hadhi ya Nyota tano?

(b) Je, Serikali haioni gharama hii ni kubwa mno kwa nchi yetu ambayo kuna wananchi wanaoishi chini ya U$D moja kwa siku?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, mapema mwaka huu alitoa mwaliko kwa Klabu ya *Real Madrid* toka Hispania kuja nchini kucheza michezo ya kirafiki ya mpira wa miguu katika Uwanja wetu mpya wa kisasa wa *Tanzania National Main Stadium* unaotarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Aidha, utekelezaji wa mwaliko huu ulitolewa na Serikali kwa sekta binafsi na makampuni ya ndani na nje ili yagharamie kwa ukamilifu ujio *Real Madrid* kwa kuunda Kamati Maalum ya kushughulikia ujio huo. Gharama zote za ujio wa kablu hiyo ni juu ya wadhamini kupitia matangazo ya kibiashara na sio fedha za Serikali.

Pia ujio huo haufungamani na sherehe za uzinduzi wa uwanja mpya wa michezo, bali sherehe hizo za uzinduzi wa uwanja huo zitajitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa sasa ujio wa kablu ya *Real Madrid* umeahirishwa hadi mwakani na hii inatokana na ratiba ya michezo mingi waliyokuwa nayo huko kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua fika hali ya wananchi na kipato chao, ndiyo maana imetafuata njia za kusaidia kuinua Pato la Taifa. Moja ya njia hizo ni Utalii kupitia michezo. Ujio wa *Real Madrid* ni moja ya njia ya kuwekeza katika michezo.

Tanzania imedhamiria kutekeleza dhana ya utalii katika michezo kama kunavyofanyika duniani kote ambayo imepata msukumo mkubwa katika nadharia za kiuchumi ili kuongeza Pato la Taifa kwa nchi husika. *(Makofi)*

Ujio wa Klabu ya *Real Madrid* utakuwa kichocheo kikubwa cha kuinua kiwango cha mpira wa miguu nchini pamoja na kuwa daraja la kutangaza vivutio vya utalii nchini kwa mfano mbuga zetu za wanyama, hifadhi, Mlima wa Kilimanjaro, Michoro ya kale, kutengeneza ajira kwenye hoteli zetu na hatimaye Tanzania kutambulika duniani hata kuwezesha mechi za Kimataifa kufanyika hapa nchini kwetu.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ingawa sina uhakika timu hiyo itakapokuja inaweza kucheza na timu gani katika nchi yetu. Lakini nina swali moja la nyongeza. Je, Serikali haioni ni busara kutumia fedha nyingi hizo ambazo zitatolewa na wafadhili kuzipeleka timu zetu mbili; yaani timu ya vijana na timu ya Taifa nchi za nje ili kupata mazoezi na timu nyingine?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kulitaarifa Bunge lako Tukufu kwamba suala la kualika timu na suala la kufanya mazoezi ni vitu viwili tofauti. Tunachokizungumza hapa zipo sababu nyingi sana za msingi ambazo timu ya *Real Madrid* au Timu yoyote kutoka nje kuja ni faida kwa Taifa letu. Ningependa kuzitaja chache. Timu ya *Real Madrid* ni maarufu sana katika dunia na ni moja ya klabu tajiri na ina wachezaji wazuri sana na wachezaji ambao watakapokuja hapa kwetu tutafaidika na mengi. Tanzania ni nchi ambayo sasa hivi inapiga hatua katika suala la michezo hasa mpira wa miguu.

Kwa hiyo, itakapofika timu kama hiyo zipo faida nyingi ambazo zitapatikana. Moja, kubwa wachezaji wetu wataona wachezaji wa Kimataifa na wachezaji maarufu ambapo hawajawahi kuwaona duniani, watawaona. Watoto wadogo pia wataona wachezaji kama hao. Wachezaji kama Canavaro, unamwona tu kwenye luninga lakini watamwona kwa macho yao na mchezaji kama Robinho, na wengine wengi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu nyingine ya msingi ni kwamba wachezaji wetu wengi hawana uzoefu wa Kimataifa. Ni lini watakuwa na uzoefu wa Kimataifa kama hawachezi na timu kubwa. Ndiyo maana tunaalika timu kama hizo kuja na si Tanzania pekee yake inafanya hivyo ni nchi nyingi zinafanya hivyo. Ndiyo maana hata timu yetu mnaona imefanya vizuri zaidi kwa sababu imefanya mazoezi na timu kama tano, walicheza na Angola, walicheza na Kongo, walienda Brazil wote huo ni uzoefu ambao umefanya timu ifanye vizuri. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambaye ninampoongeza sana kwa jitihada zake za kuinua michezo hasa hapa Bunge. Ningependa kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa uwanja huo unaozungumzwa unakaribia kumalizika na unatarajiwa kufunguliwa hivi karibuni; na kwa kuwa ni uwanja mzuri wa Kimataifa na wa kisasa.

Je, Serikali imejiandaa vipi katika kuutunza uwanja huo na katika uendeshaji ikiwa ni pamoja na kuwa na wafanyakazi hasa *Manager* ambaye anaweza akazungumza lugha tatu, Kiingereza, Kifaransa na Kiarabu kwa kuzingatia kwamba watakaokuja kutoka huko nje watatumia lugha hizo tatu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL N. BENDERA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali tumejipanga vizuri na tunatambua umuhimu wake.

Kwa kutambua hilo ni kwamba Kamati Maalum kama nilivyosema katika jibu langu la msingi iliundwa na imezingatia hayo na kuweza kufanikisha hivyo nilikwambia iko Kamati ambayo tunaandaa Mkataba Maalum ambao katika Mkataba huo mambo

hayo ambayo yamezungumzwa na Mheshimiwa Mpesya yamo. Kuhakikisha kwamba wachezaji wanaokuja ni wachezaji nyota na sio wachezaji ambao ni wa kiwango cha chini. Tunataka tukuhakikishie hilo.

Lakini pia nataka nisema pointi moja ya msingi. Waheshimiwa Wabunge suala la michezo ni sawa sawa na sekta nyingine zozote. Lakini yako mawazo potofu kwa watu wengi inapofikia suala la michezo hasa wakati timu ya *Real Madrid* inaagizwa wengine wamefikia hata kuzungumza lugha za kejeli kana kwamba michezo sio sehemu muhimu katika nchi hii. Ni vizuri tukatambua kwamba michezo ni sehemu mojawapo muhimu katika nchi nayo inatakiwa kupewa kipaumbele kama sehemu nyingine zote. Lakini tunaposikia mtu anachanganya madeski na viwanja na madarasa na michezo kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Sasa nina matangazo ya wageni. Kama mnavyofahamu leo ni zamu Wizara hii ni ya Wizara ya Usalama wa Raia. Kwa hiyo, watumishi wa Wizara hiyo bila hata kuwatambulisha mnawaona wamewakilishwa vizuri. Lakini ningependa kutambulisha tu viongozi ambao wapo katika nafasi ya uongozi mkubwa.

Kwanza nafurahi kumtambulisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye pia ni mume wake na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo wa Ufundi, Ndugu Bakari Mahiza.

Pia napenda nimtambulishe *DAP* wa Wizara hiyo Ndugu Mdogo. Napenda pia nimtambulishe Kaimu *DDP* Mama Nyoni. Naomba pia nimtambulishe *IGP* Ndugu Said Mwema. Tunapenda kukupongeza pia kwa kazi nzuri unayoifanya ambayo inaonekana katika nchi yetu. (*Makofi)*

Naomba nimtambulishe *CP* Ndugu Mtweve, *DOT* Ndugu Chagonja, *DCI* ambaye naye ni maarufu Ndugu Manumba, tunashukuru kwa kazi njema mnazofanya. *(Makofi)*

Pia naomba nimtambulishe *CP* Kanda Maalum na huyu maarufu tunamfahamu sana Ndugu Alfred Tibaigana. Tunakufahamu maarufu sana kwa Dar es Salaam na tunajua ndiyo Jiji lenyewe lina kila kitu cha ovyo na vizuri vyote viko, lakini unavimudu.

Naomba nimtambulishe pia *CP* kutoka Zanzibar, *CP* Khamis Simba, *CRP P.* Mosha. Pia naomba nimtambulishe *CIP* Zanzibar *Sergeant A.C*. Ngw'anamwaka. *Pay Master Zanzibar ACP* Mohamed Ussi. Naomba nimtambulishe *CDC, ACP* Ezzeti Munisi, Mrs. huyo mama, *CF ACP* Jonas Mgendi, *SSO* Gregory Kaijage, Arcado Mchinga Accountant na *ASP* Mangu, *ACP* Kusima na *SPC* Khamis.

Wageni wengine wote tunafurahi sana kuwaona mnatufanyia kazi nzuri sana ya ulinzi na kwa kweli matukio ni mengi lakini tunaridhika kabisa na kazi mnazozifanya, tunawatakieni kila la kheri. *(Makofi)*

Sasa wageni wengine nina Katibu Mkuu Mama Rose Lugembe mimi nilipoanza kazi Wizara ya Maendeleo ya Jamii ndiyo alikuwa Katibu wangu yuko wapi? Hayupo

alikuwa afuatane na Nipa Mdoe. Pia tuna mgeni wetu mtoto wetu Kelvin Shellukindo, mtoto wa Mr. na Mrs Shellukindo, Waheshimiwa Wabunge. *Where are you Kelvin*? Yuko pale. (*Makofi)*

Halafu nina wageni wengine watoto mapacha wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia Ahmed Mohamed Aboud na Ali Mohamed Aboud. Nina wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesya, Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Makatibu Kata wa Jiji la Mbeya naomba wote wasimame. Mnakaribishwa majirani zangu kule.

Halafu nina mgeni wa Mheshimiwa Switi, Bwana Suleiman Mohamed Tumaini, Mratibu Msaidizi wa Haki za Binadamu. Yuko wapi? Ahsante karibu sana. Halafu nina wageni wangu wapenzi kabisa wanafunzi 50 na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Uhuru Dodoma wote wasimame. Mnakaribishwa Wabunge wa kesho. Waheshimiwa Wabunge siwezi kuwataja wageni wote lakini nina mgeni mmoja wa Mheshimiwa Chitallilo, Mheshimiwa Stephen Shindika, Diwani Viti Maalum Buchosa yuko wapi? Karibu sana. (*Makofi)*

Wageni wengine wote uwanja ni huru kwa kila *Public Gallery* ni ya watu wote tu hawa wasiokaribishwa wana uhuru wa kuwepo hapa ili kufuatilia Shughuli za Bunge. Ni haki ya wananchi kusikiliza Wabunge wao wanapofanya kazi na ndiyo maana hata kwenye luninga *(TV)* tunaonyesha kwa sababu ni wajibu wetu kujionyesha tunachofanya ndani ya Bunge.

Baada ya kusema hayo nina matangazo ya kazi. Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati wa Kilimo na Ardhi anawatangazia Wajumbe wake kwamba watakuwa na kikao saa 6.00 mchana katika chumba Na. 231, jengo la Utawala.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatibu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira anawatangazia Wajumbe wake kwamba kutakuwa na kikao saa 5.00 asubuhi hii katika chumba 219. Halafu tuna Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, anawatangazia Wajumbe wake kwamba saa 5.00 asubuhi hii kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa chumba 432.

Lakini nina tangazo lingine la mwisho Waheshimiwa Wabunge mwenzetu Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed amefiwa na Mama yake mzazi huko Zanzibar jana tarehe 22 Julai, 2007 nadhani maziko yanaendelea sasa hivi kule Zanzibar.

Lakini tumewakilishwa na Mheshimiwa Mohamed Khatib katika mazishi hayo yanayofanyika hivi Zanzibar hivi sasa. Utaratibu wetu wa kawaida wa kumpa mwenzetu ubani utaendelea kama tunavyofanya kila wakati.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo ni mwisho wa matangazo yetu kwa siku ya leo.*(Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi Kwa Mwaka 2007/2008**
**Wizara ya Usalama wa Raia**

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitoe pole zangu kwa mheshimiwa Ali Ameir kwa kufiwa na mama yake mzazi. Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. (*Amin)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa Bungeni mapema leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa William Kusila, Mbunge wa Bahi, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007, Bunge lako Tukufu limempoteza Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti aliyekuwa Mbunge wa Tunduru na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, aliyefariki kwa ajali ya ndege iliyotokea Mkoani Mbeya. Katika ajali hiyo, watu wanne walipoteza maisha na wawili kunusurika. Napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa wafiwa wote. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. (*Amin*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 26 Juni, 2007 Bunge lako lilimpoteza Mbunge kijana na mahiri Mhe. Amina Chifupa aliyekuwa akishirikiana vema na Wizara yangu kwa kuwa mstari wa mbele kupiga vita maovu mbali mbali katika jamii, likiwemo suala la matumizi na biashara haramu ya madawa ya kulevya. Wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla ni mashahidi wa namna marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa alivyokuwa mstari wa mbele katika kuwawakilisha vyema vijana wote nchini. Namwomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa uvumilivu wazazi, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu. Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. (*Amin)*.

Aidha, kwa masikitiko makubwa, napenda kutoa pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu, jamaa na marafiki katika ajali za magari ya abiria na magari binafsi zilizotokea hivi karibuni katika maeneo mbali mbali hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** natoa wito kwa madereva wote wa magari ya abiria na magari binafsi, kuendesha magari kwa kuzingatia sheria zote za Usalama Barabarani ili kuepusha ajali ambazo zimekuwa zikisababisha hasara kubwa ya watu na mali kwa Taifa letu na kwa familia.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kwa hotuba zao nzuri ambazo zimetoa mwelekeo wa bajeti ya Serikali, hali ya uchumi wa nchi kwa jumla na masuala ya msingi yanayopaswa kutekelezwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza kwa dhati wewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa umahiri wenu katika kuliongoza Bunge hili. Aidha, nawapongeza kwa

namna mnavyotoa ushirikiano mkubwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote katika kufanikisha majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2007 Bunge limepata Wabunge wapya watatu. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba (Mbunge wa Kuteuliwa), Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura (Mbunge wa Tunduru) na Mheshimiwa Florance Essa Kyendesya (Mbunge Viti Maalum). Tunawakaribisha kwa moyo mkunjufu katika Bunge hili ili tuweze kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile napenda niungane na Mawaziri waliotangulia kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dr. Aman Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba na Mheshimiwa Septuu Nasoro.

Wengine ni Mheshimiwa Abdallah Ally Mwinyi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari na Mheshimiwa Dr. Fortunatus Masha. Kuchaguliwa kwao kunathibitisha imani kubwa ambayo Wabunge na Watanzania kwa ujumla waliyonayo kwao. Ninawatakia mafanikio mema katika kutekeleza majukumu yao.

Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007, Taifa letu limepata heshima kubwa Kimataifa kwa kupewa nafasi ya uongozi katika Taasisi kubwa ya Kimataifa. Nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Umma wa Watanzania una imani kubwa naye kwamba atamudu vema majukumu yake mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu pamoja na kuhoji masuala mbalimbali ya Wizara ya Usalama wa Raia na kuyatolea maoni na ushauri.

Aidha, napenda kutoa shukrani kwa ushirikiano wa karibu, ushauri na maelekezo fasaha ambayo Wizara ya Usalama wa Raia imekuwa ikiyapata kutoka kwa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama. Ushauri na maelekezo yao yametusaidia kwa kiasi kikubwa kuimarisha utendaji kazi wetu. Maelekezo yao yatakuwa dira yetu katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pongezi na shukrani nyingi kwa Inspekta Jenerali wa Polisi, Makamishna pamoja na Makamanda wote wa Polisi wa Mikoa, Vikosi na Wilaya, Wakuu wa Upelelezi wa Mikoa, Vikosi na Wilaya na askari wote kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya ya kudumisha amani, usalama na utulivu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya amani na utulivu ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi kwani huwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika maeneo mbali mbali nchini na hivyo kuongeza nafasi za ajira na Pato la Taifa. Ni katika mazingira hayo ya amani na utulivu ndipo mipango na mikakati ya Kitaifa inaweza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla nchi yetu imeendelea kuwa ya amani na utulivu. Vitendo vya uhalifu mkubwa vimeendelea kudhibitiwa. Takwimu za uhalifu katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2006 zinaonyesha baadhi ya makosa yamepungua na mengine yameongezeka ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa makubwa ya jinai yamegawanywa katika makundi matatu yafuatayo: Makosa Dhidi ya Binadamu, Makosa Dhidi ya Mali na Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii. Idadi ya matukio ya uhalifu nchini, Tanzania Bara na Visiwani, hususan makosa makubwa ya jinai kitakwimu imeendelea kushuka na kupanda katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, ya 2002 hadi 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha pia kwamba, idadi ya matukio hayo ilipanda mwaka 2003 na kufikia matukio 76,357. Mwaka 2004 kulikuwepo na ongezeko la idadi ya matukio yaliyoripotiwa Polisi ambapo jumla ya matukio 79,619 yaliripotiwa. Hata hivyo, idadi hiyo ya matukio kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2005 ilishuka hadi kufikia matukio 61,376, ikiwa ni upungufu wa matukio 18,243 ambao ni sawa na asilimia 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, makosa makubwa ya jinai yaliyotolewa taarifa katika vituo vya Polisi kuanzia Januari hadi Desemba 2006 katika Mikoa yote nchini yalikuwa 50,816 ikilinganishwa na matukio 61,376 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2005. Kuna upungufu wa makosa 10,560 sawa na asilimia 17.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti ya kushuka kwa makosa kati ya mwaka 2005 na mwaka 2006 ni kubwa na hii ni kutokana na juhudi zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi za kukabiliana na uhalifu ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola pamoja na Mashirika ya Kimataifa kama vile Interpol. Hata hivyo, bado juhudi zaidi zinahitajika kupambana na uhalifu kote nchini, Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Majedwali Na. 2(a) hadi 2(d) yanatoa mchanganuo wa makosa makubwa ya jinai kimkoa kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2006. Kwa muhtasari, Mkoa ulioongoza kwa Makosa Dhidi ya Binadamu ni Dar es Salaam ukifuatiwa na Iringa, Morogoro, Mwanza, Tabora, Mbeya, Kagera, Ruvuma, Singida na Pwani. Kwa ujumla wake, vyanzo vya makosa dhidi ya binadamu ni pamoja na imani za kishirikina, kulipiza kisasi, ulevi uliokithiri, wivu wa kimapenzi, ugumba, tamaa za mwili, mmomonyoko wa maadili katika jamii, na kadhalika.

Kwa upande wa Makosa Dhidi ya Maadili ya Jamii, Mkoa ulioongoza ni Dar es Salaam na kufuatiwa na Mwanza, Kagera, Mara, Pwani, Shinyanga, Arusha, Manyara,

Kilimanjaro na Mjini Magharibi. Katika aina hii ya makosa suala la dawa za kulevya, hususan cocaine na heroine bado ni tatizo kwani wahalifu wanaendelea kuziingiza nchini na kuathiri vibaya afya za vijana wanaotumia dawa hizo. Juhudi za Jeshi la Polisi kuendeleza mapambano dhidi ya dawa hizo ni kubwa na bado zinaendelea. Tunashukuru kwa ushirikiano tunaopata kutoka kwa wananchi. Aidha, kuhusu Makosa Dhidi ya Mali, Mkoa ulioongoza pia ni Dar es Salaam ukifuatiwa na Kagera, Mwanza, Morogoro, Mara, Tabora, Iringa, Singida, Rukwa na Ruvuma. Vyanzo vya makosa dhidi ya mali ni pamoja na ukosefu wa ajira kwa vijana, tamaa ya kupata utajiri wa haraka haraka, kupenda maisha ya starehe, wimbi la wahamiaji haramu na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, Jeshi la Polisi limeweka mikakati madhubuti ya kukabiliana na uhalifu katika maeneo mbali mbali yakiwemo maeneo ya ukanda wa utalii Zanzibar. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya doria za mara kwa mara karibu na hoteli za kitalii, kuhakikisha kila mfanyakazi katika hoteli hizo anachukuliwa alama za vidole kwa ajili ya kumbukumbu au endapo tukio litatokea, kutoa mafunzo kwa wananchi na walinzi wa mahoteli na maeneo mbali mbali, kuzungumza na wawekezaji ili walichangie Jeshi la Polisi kwa kujenga vituo, kutoa magari, pikipiki na vitendea kazi vingine.

Aidha, kuendeleza ushirikiano uliopo na Idara ya Uhamiaji, Usalama wa Taifa, Kamisheni ya Utalii Zanzibar na Taasisi nyingine ili kuhakikisha kuwa usalama, amani na utulivu katika Visiwa hivyo unadumishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi kubwa zinafanywa na Jeshi la Polisi na vyombo vingine kudhibiti ongezeko la ajali za barabarani, zikiwemo kutoa elimu kwa umma, ili umma uwe mstari wa mbele katika jitihada za Serikali za kupunguza ajali, kufanya doria za magari kwenye barabara kuu za mijini, kutumia askari wa Intelijensia kuorodhesha madereva wanaokwenda mwendo wa kasi na madereva wasio na leseni au wenye leseni bandia. Hata hivyo, bado matukio mabaya ya ajali za magari ya abiria na mengineyo yanayosababisha vifo vya watu wengi na wengine kujeruhiwa yameendelea kutokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya ajali ambazo ziliripotiwa Polisi kati ya Januari hadi Desemba 2006 zilikuwa 18,187 ikilinganishwa na 17,220 katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2005. Kuna ongezeko la ajali 967 sawa na asilimia 5.6. Kati ya Januari hadi Desemba 2006 watu waliofariki kutokana na ajali za barabarani walikuwa 2,657 na wengine 16,456 walijeruhiwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2005 ambapo watu 2,509 walifariki na wengine 17,434 kujeruhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya watu waliofariki iliongezeka kwa watu 148 sawa na asilimia 5.9 na waliojeruhiwa ilipungua kwa watu 978 sawa na asilimia 5.6 kama inavyoonyesha katika Jedwali Na.1. Takwimu hizo zinaonyesha kuongezeka kwa idadi ya ajali za barabarani na idadi ya watu waliokufa kutokana na ajali hizo.

Ajali za barabarani zina athari kubwa katika uchumi wetu kwani hupoteza nguvu kazi kutokana na vifo, ongezeko la watoto yatima, watu kuwa vilema na upotevu na uharibifu wa mali. Tatizo la ajali za barabarani ni kubwa, hivyo jitihada zaidi za Jeshi la

Polisi pamoja na wadau wengine katika kukabiliana na makosa ya usalama barabarani zinahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na takwimu za mwaka 2006, Mkoa ulioongoza kwa kuwa na ajali nyingi za barabarani ni Dar es Salaam ukifuatiwa na Mikoa ya Morogoro, Mjini Magharibi, Mwanza, Pwani, Mbeya, Ruvuma na Kilimanjaro kama inavyoonyesha kwenye Jedwali Na. 2(f). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za kuwepo ajali za barabarani ni nyingi na zinagusa wadau mbalimbali katika kupata ufumbuzi wake ukiwemo umma kwa ujumla. Wapo wananchi ambao wamekuwa wakifurahia na kushabikia mwendo wa kasi na kuwalaumu madereva wanaokwenda pole pole. Lipo tatizo la miundombinu michache ukilinganisha na mahitaji na uchakavu wa miundombinu hiyo. *(Makofi)*

Aidha, baadhi ya ajali zimeonyesha kwamba ujenzi wa bodi za magari haufuati viwango vinavyotakiwa na kusababisha ajali mbaya. Ushirikiano baina ya wadau ni njia sahihi ya kupata ufumbuzi wa tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara ya Miundombinu ambayo ni mdau mwenzetu mkubwa katika masuala haya ya Usalama Barabarani kwa hatua ambayo imechukua ya kuandaa Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani ambayo imelenga kufanya uchambuzi wa kina wa matukio ya ajali za barabarani na kuja na mapendekezo ya kudhibiti hali hiyo kwa mapana yake. Sera hiyo itaangalia mambo mbalimbali muhimu, ikiwa ni pamoja na kuunda Bodi itakayosimamia kwa makini usalama barabarani kwa ujumla (*Road Safety Management*), na hatimaye kutungwa kwa Sheria Mpya. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla wavute subira wakati Serikali inalishughulikia suala hili muhimu, ambalo ni la mtambuka na linagusa Idara na taasisi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kuanzisha Wizara hii na kufanya mabadiliko ya uongozi wa juu wa Jeshi la Polisi, wananchi na wadau wengine wameendelea kujenga imani na kuwa na matarajio makubwa kwa Wizara hii na kwa Jeshi la Polisi.

Aidha, mabadiliko ya uongozi yanayoendelea kufanyika ndani ya Jeshi la Polisi yenye lengo la kuboresha utendaji kazi, yamekuwa ni chachu ya wananchi kuendelea kujenga imani na Jeshi hilo. Katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu cha uhai wake, Wizara yangu imejitahidi kupanga, kuandaa na kutekeleza yafuatayo:

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuboresha huduma ya Polisi kwa wananchi, Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Wakuu wa Polisi wa Wilaya na baadhi ya Wakuu wa Vikosi na Vituo wamepatiwa mafunzo ya kuwajali wateja (*Customer Care)* ili askari waweze kuwahudumia wananchi kwa upendo, lugha na kauli nzuri. Kwa sasa hivi, somo la huduma bora kwa wananchi linafundishwa kwenye vyuo vyote vya Polisi kwa kozi ya awali. Aidha, kwa msaada wa Serikali ya Ujerumani, Wakuu wa Vituo

vyote vya Polisi nchini wamepatiwa mafunzo ya uongozi na menejimenti yaliyoendeshwa kikanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu mwaka uliopita nilieleza kwamba waathirika wakubwa wa uhalifu ni wananchi wenyewe. Hivyo, Jeshi la Polisi litaendelea kupokea taarifa mbalimbali za uhalifu na wahalifu kutoka kwa wananchi zitakazosaidia kuzuia vitendo vya uhalifu kutokea na pia kuwakamata wahalifu. Kazi hii inatekelezwa kwa usiri mkubwa.

Napenda kuwahakikishia wananchi kwamba itakapothibitika kwamba askari wamevujisha taarifa za raia wema, Jeshi la Polisi litawachukulia hatua kali za kinidhamu ikiwemo kuwafukuza kazi. Aidha, Utaratibu wa Polisi Jamii unaotarajia kuanzishwa ni njia mojawapo ya Jeshi la Polisi kuwa karibu zaidi na wananchi katika kushughulikia kero na malalamiko mbalimbali ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kama moja ya mikakati ya Jeshi la Polisi kuwa karibu zaidi na wananchi, mwaka huu Jeshi la Polisi kwa mara ya kwanza tangu tupate Uhuru limefungua Banda katika Uwanja wa Maonyesho wa SabaSaba ili kuwaelimisha wananchi shughuli mbali mbali za Jeshi la Polisi. Katika banda hilo, wananchi wameelezwa mambo mbali mbali, ikiwemo shughuli za Jeshi hilo, haki za wananchi, namna ya kushiriki katika kuzuia na kupambana na uhalifu na masuala ya usalama barabarani. Naamini elimu kubwa iliyotolewa kwa wananchi, kuhusu Jeshi lao itawasaidia kushirikiana nao kwa karibu na kwa uwazi zaidi kwa kuwa Jeshi la Polisi ni rafiki wa raia wema na si vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Jeshi la Polisi limeendelea kuwapatia askari mafunzo ya taaluma na ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ndani na nje ya nchi ili wafanye kazi kwa kuzingatia Sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Katika mwaka wa masomo wa 2006/2007, kati ya Julai, 2006 hadi mwezi Mei, 2007 askari 967 wamepelekwa kusoma katika vyuo mbalimbali hapa nchini na askari 13 wamepelekwa kusoma nje ya nchi ili kuimarisha taaluma zao.

Aidha, askari 86 wamehudhuria mafunzo mbalimbali ya taaluma yanayotolewa na nchi rafiki kwa ufadhili wa nchi hizo kama vile Marekani, Misri, Morocco, Algeria, Japan na Urusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuimarisha utendaji unaozingatia sheria, Wizara kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi imeendesha semina za Utawala Bora kikanda zilizojumuisha askari, Watendaji wa Mitaa na Waheshimiwa Madiwani. Kanda zilizohusika ni Kanda ya Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Magharibi, Kaskazini, Kati na Kanda ya Kusini kwa upande wa Tanzania Bara. Semina za aina hii zilifanyika pia Zanzibar.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2006 hadi mwezi Mei, 2007 askari saba (7) wamefukuzwa kazi kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa kama ifuatavyo: Kanda Maalum ya Polisi Dar es Salaam (2), Zanzibar (1), Shinyanga (1), Tabora (1), Iringa (1)

na Tanga (1), na askari (6) wamefukuzwa kazi Mkoani Rukwa kwa kuwabambikiza wananchi kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imejipanga kikamilifu kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi. Wizara imeunda Kamati Maalum (*Task Force*) ya wataalam kutoka Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ili kuchunguza malalamiko ya ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi na kuchukua hatua za haraka kurekebisha dosari zitakazobainika. Kazi hiyo inaendelea kufanyika kwa wataalam hao kutembelea mikoa yote nchini na kufanya ukaguzi wa kesi za siku nyingi ambazo bado zipo Mahakamani. Zoezi hili linaendelea vizuri na linatarajiwa kuwa la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa kwa Jeshi la Polisi ni kufika mapema eneo la tukio na kuyashughulikia matukio yote ya uhalifu kwa ufanisi kwa kuwakamata na kuwafikisha mahakamani wahalifu wote wanaohusika. Katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita jitihada za kufika mapema kwenye maeneo ya matukio zimeendelea kuimarishwa. Hata hivyo, ili kutekeleza suala hili kikamilifu, Jeshi la Polisi linahitaji kuwezeshwa ili liweze kuongeza idadi ya askari na vitendea kazi kama vile magari, pikipiki na vifaa vya mawasiliano.

Kwa upande wa idadi ya askari, jitihada zinaendelea za kupanua na kukarabati vyuo vya Polisi vilivyopo vya Dar es Salaam, Zanzibar na Moshi pamoja na kukarabati majengo ya kilichokuwa Chuo cha *TANESCO* cha Kidatu, kukifanya kuwa Chuo cha Polisi baada ya kukabidhiwa na Wizara ya Nishati na Madini. Kuhusu vitendea kazi, pamoja na magari machache yaliyonunuliwa kutokana na bajeti, Jeshi la Polisi limefanikiwa kupata msaada wa magari 40 na pikipiki 170 kutoka kwa Mtawala wa Dubai. Msaada huu umepatikana kufuatia jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamshukuru sana .

Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 nililieleza Bunge lako Tukufu kuhusu azma ya Wizara yangu kuandaa Sera ya Usalama wa Raia ambayo itaongoza utendaji na mahusiano na wadau na vyombo mbalimbali vya Serikali na wananchi katika suala la Usalama wa Raia**.** Napenda kutoa taarifa kuwa Mshauri Mwelekezi (*Consultant*) wa kufanya kazi hiyo amepatikana ambaye ni Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ameanza kazi mwezi Mei, 2007. Kazi hii inatarajiwa kukamilika katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana, nilieleza nia ya Wizara yangu kuangalia upya mfumo, muundo na kuzipitia upya Sheria na kanuni za Jeshi la Polisi kwa lengo la kuuboresha ili kuliwezesha kukabiliana kikamilifu na uhalifu wa kisasa. Napenda kutoa taarifa kwamba hivi sasa Jeshi la Polisi lipo kwenye mchakato wa kuandaa Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi *(Police Force Reform Programe*) chini ya usimamizi wa wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na Maofisa wa Jeshi letu la Polisi. Mchakato upo katika hatua nzuri ya utayarishaji.

Mnamo mwezi Aprili, 2007 Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama walipata fursa ya kupata maelezo kuhusu progaramu hii kutoka kwa wataalam hao hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu hii imejikita katika maeneo muhimu matatu yafuatayo:-

(i) Kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa (*Modernization*) ambapo litakuwa na mbinu za kisasa za kuzuia na kukabiliana na uhalifu, vitendea kazi vya kisasa, miundombinu ya kisasa na ustawi wa kuridhisha wa watendaji wa Jeshi la Polisi,

(ii) Kuimarisha taaluma katika Jeshi la Polisi *(Professionalism*) ili kuboresha ufanisi na utendaji ambapo askari atapanda cheo kwa kuzingatia utendaji na siyo kwa miaka aliyokaa Jeshini.

(iii) Kuimarisha Utaratibu wa Polisi Jamii (*Community Policing*) kwa kuwashirikisha wananchi katika maamuzi yanayohusu ulinzi na usalama katika maeneo yao na kuboresha uwajibikaji wa Jeshi la Polisi kwa wananchi.

Programu hii itakapokamilika itaiweka Wizara katika nafasi nzuri ya kuangalia upya muundo, mfumo, Sheria na kanuni za Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, *(Legal Sector Reform Programme*) Serikali ipo kwenye mchakato wa kuhamisha shughuli za uendeshaji mashtaka kutoka Jeshi la Polisi na taasisi nyingine zilizokuwa zinafanya kazi hiyo na kuzipeleka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini. Katika maboresho hayo, Idara ya Upelelezi inatarajiwa kugawanywa katika vitengo kulingana na utaalamu wa makosa mbali mbali ya jinai. Kazi ya kuigawa Idara hii itafanyika kwa awamu mara Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Kitengo cha Intelijensia kinaendelea kuimarishwa kwa kukipatia mafunzo na kukiongezea askari na vitendea kazi ili kiweze kutoa mchango mkubwa katika uzuiaji wa uhalifu. Kwa upande wa mafunzo, Serikali ya Uingereza imetoa msaada wa mafunzo kwa askari wa Kitengo hiki. Mafunzo hayo tayari yameanza kutolewa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya ulinzi wa Jeshi la Polisi kwenye bandari ilisitishwa tangu mwaka 1993 ambapo Mamlaka ya Bandari iliamua kutumia Polisi Wasaidizi (*Auxilary Police*) wa kwake. Jukumu la kulinda mipaka ya nchi na rasilimali muhimu za Taifa ni la Jeshi la Polisi kisheria. Ili kurudisha huduma za Polisi Bandarini, Wizara yangu inaendelea kulifanyia kazi suala hili kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu pamoja na Mamlaka ya Bandari Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** jukumu la msingi la Jeshi la Polisi ni kulinda usalama wa watu na mali zao popote walipo, nchi kavu na katika bahari, maziwa au mito. Hata hivyo, Kikosi cha Polisi Wanamaji kimekuwa kikikabiliwa na matatizo mbali mbali

likiwemo la ukosefu wa vitendea kazi, hasa usafiri kutokana na gharama kubwa ya boti za doria za kisasa zitakazoweza kufanya doria na operesheni mbali mbali kwa ufanisi.

Pamoja na dhamira njema ya Serikali ya kulipatia Jeshi la Polisi boti hizo, bado Serikali inakwamishwa na uwezo wetu mdogo wa kiuchumi. Mtakumbuka kwamba miezi michache iliyopita, Mheshimiwa Rais alitembelea Mkoa wa Mwanza na kuahidi kutatua tatizo hilo.

Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa ujumla, kuwa na subira, kwani hali itakaporuhusu Serikali itanunua boti nzuri za kisasa zenye vifaa kuwawezesha askari wa doria kufanya kazi zao. Kwa sasa, Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na vyombo vingine vya dola kufanya doria na misako ya mara kwa mara ili kudhibiti uhalifu majini.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuwa changamoto siyo kwa nchi yetu tu, bali kwa nchi zote duniani. Sababu mbalimbali zimechangia hali hii, zikiwemo Utandawazi, kukua kwa Sayansi na Teknolojia, kuongezeka kwa maingiliano ya watu duniani na upana wa mipaka ya nchi nyingi za Kiafrika, unaosababisha kutokuwepo udhibiti wa kutosha katika vituo vya kuingilia na kutokea kutokana na ukosefu wa rasilimali mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi mbalimbali zinachukuliwa na nchi zote duniani kupambana na tatizo la dawa za kulevya. Kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la kupambana na dawa za kulevya, *UNODC,* hivi sasa inasadikiwa zaidi ya asilimia 45 ya dawa za kulevya aina ya Cocaine zinazozalishwa duniani zinakamatwa katika nchi mbalimbali, ambapo mwaka 1999 kiasi kilichokuwa kikikamatwa ni asilimia 24 tu.

Katika kuendelea kuhamasisha nchi zote duniani kupambana na dawa za kulevya, Umoja wa Mataifa uliichagua tarehe 26 Juni, ya kila mwaka kuwa siku ya kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya duniani. Nchi yetu imekuwa ikishiriki kikamilifu katika vita hivyo ambapo mwaka huu maadhimisho hayo yalifanyika Mkoani Tanga na mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na juhudi za Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola kupambana na dawa za kulevya, mwaka 2005 tulifanikiwa kukamata jumla ya kilo 150,000 za dawa za kulevya aina ya Cannabis, kilo 1,206 za Mirungi, kilo 10 za Heroin na gram 362 za *Cocaine*. Jumla ya watu 4,532 walikamatwa katika matukio 3,368 ya kupatikana na dawa za kulevya.

Aidha, mwaka 2006 takwimu za kukamata dawa za kulevya zinaonyesha mafanikio zaidi ya kupambana na dawa hizo, kwani zilikamatwa kilo 91.5 za *Heroin,* kilo 4.13 za *Cocaine*, kilo 37 za *Morphine*, kilo 11 za Mirungi na kilo 225,229 za *Cannabis.* Jumla ya watu 7,194 walikamatwa kuhusiana na matukio 5,532. Halikadhalika,

Watanzania 54 walikamatwa katika nchi mbalimbali duniani kwa kujihusisha na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kurudia kutoa onyo kwa wote wanaotumia na wanaofanya biashara ya dawa za kulevya, kuacha mara moja tabia hiyo kwani hivi sasa juhudi za Serikali kupambana na dawa hizo zimeongezeka zaidi. Takribani wiki mbili zilizopita, ulifanyika Mkutano wa Wakuu wa Taasisi za Kupambana na Dawa za Kulevya wa Nchi za Afrika ulioshirikisha pia Maofisa kutoka Shirikisho la Polisi la Kimataifa *(Interpol*).

Mkutano huo ulifanyika Mkoani Arusha tarehe 9-10 Julai, 2007 na kuhudhuriwa na nchi 44 ambapo jumla ya washiriki 121 walihudhuria. Mbinu na mikakati mbalimbali imepangwa na mapambano dhidi ya dawa za kulevya yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi wa Jeshi la Polisi umebaini kuwa siyo watu wote wanaokamatwa kwa kuingia nchini isivyo halali ni wahamiaji haramu au Wakimbizi. Baadhi ya watu hao huwa katika biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Kwa kuwa tatizo hili linaelekea kushamiri na kuikumba Mikoa kadhaa hapa nchini, Jeshi la Polisi limefanya uchambuzi wa kina wa matukio kadhaa ili kufahamu ukubwa wa tatizo hili hapa nchini, athari zake, wanaojihusisha na biashara hiyo ndani na nje ya nchi, mbinu na njia wanazotumia. Tathmini hii italiwezesha Jeshi la Polisi kupanga mikakati thabiti ya kukabiliana na uhalifu huu wa Kimataifa ambao hapa nchini ni kosa la jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(a) Taarifa za wanamtandao pamoja na namba zao za simu kusambazwa kwenye nchi zote wanachama wa Shirikisho la Majeshi la Polisi Kanda ya Kusini *(SARPCCO)* na Mashariki na Pembe ya Afrika *(EAPCCO).*

(b) Jeshi la Polisi limeunda Kitengo Maalum cha kushughulikia tatizo hili.

(c) Doria za pamoja na vyombo vingine vya dola kufanyika mipakani.

(d) Wizara ya Usalama wa Raia inakamilisha mchakato wa kuwasilisha Serikalini mapendekezo ili itungwe Sheria kali itakayotumika kudhibiti biashara hii haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 nilieleza kwamba Wizara yangu inaangalia uwezekano wa kuanzisha Kikosi Maalum ndani ya Jeshi la Polisi cha kuimarisha ulinzi wa watalii nchini. Mashauriano yanaendelea na wadau wengine ikiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii ili kupata sura ya Kikosi hiki itakavyokuwa na namna kitakavyofanya kazi.

Ili kupata uzoefu wa nchi nyingine, wataalam wa Jeshi la Polisi walipata fursa ya kutembelea nchi jirani ya Kenya kujifunza namna ulinzi wa watalii unavyofanywa ili yazingatiwe yale yatakayoonekana ya manufaa katika mazingira yetu. Hata hivyo, kwa upande wa Zanzibar suala hili limeanza kutekelezwa. Ulinzi wa watalii unafanywa na Kikosi Maalum cha Polisi kwa uangalifu mkubwa na matunda mazuri yameanza kuonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuanzisha utaratibu wa Polisi Jamii limeanza kufanyiwa kazi kwa kuandaa Sera ya Polisi Jamii ili utaratibu huu utumike kwa misingi ya kisheria. Mchakato unaendelea vizuri. Wataalam wa Wizara kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi wameshaandaa rasimu ya Sera ambayo itatumika kupata maoni ya wadau mbalimbali. Kazi hii itaendelea katika Mwaka wa Fedha wa 2007/08.

Aidha, Sera ya Polisi Jamii itakuwa sehemu ya Sera ya Usalama wa Raia ambayo maandalizi yake pia yamekwishaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi lina jukumu kubwa la kutoa ushauri wa kiusalama kwa Taasisi mbalimbali za kibiashara zikiwemo benki, maduka ya fedha na taasisi nyingine za fedha kuhusu namna bora ya kuimarisha mifumo ya ulinzi katika maeneo yao. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania limekamilisha maandalizi ya kanuni za usalama wa mabenki na vyombo vingine vya fedha. Aidha, Jeshi la Polisi hivi sasa linatoa ulinzi kwa mabenki yafuatayo*: NMB, CRDB, NBC, BoT, TIB, POSTAL BANK, TWIGA BANK, STANBIC BANK, CITY BANK, KENYA COMMERCIAL BANK, AKIBA COMMERCIAL BANK* na *STANDARD CHARTERED BANK*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha taratibu za ajira, mafunzo na upandishwaji vyeo kwa askari Polisi, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezi imeanza mchakato wa kuandaa taratibu hizo ambazo zitaweka bayana utaratibu wa ajira, mafunzo, kupandishwa vyeo, kuthibitishwa kazini na kadhalika. Rasimu ya awali imekamilika na itawasilishwa kwa wadau mbalimbali ili iweze kujadiliwa na kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu kupitia Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi na Magereza imeendelea kushughulikia maslahi ya askari wa Jeshi la Polisi kwa kuwapandisha vyeo na kuwathibitisha kazini. Aidha, Tume ya Polisi na Magereza ndio Mamlaka ya nidhamu kwa askari wa ngazi ya Inspekta Msaidizi hadi Kamishna Msaidizi wa Polisi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/07 Tume imewapandisha vyeo jumla ya askari 1,184 na kuwathibitisha kazini askari 185.

Moja ya kazi muhimu za Tume ni kuhakikisha kuwa askari na maofisa wanapandishwa vyeo na kuthibitishwa kazini wanapostahili kwa kutumia vigezo mbalimbali, zikiwemo taarifa za utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi limeendesha zoezi la kuhakiki umiliki wa silaha ndogo ndogo kwa kusajili upya silaha hizo. Kati ya Agosti, 2006 na Mei, 2007 jumla ya silaha 52,700 zilihakikiwa katika zoezi hilo. Silaha 9,157 ziligundulika kumilikiwa kinyume cha sheria na watu 3,989 walikamatwa na Polisi kwa uchunguzi zaidi. Zoezi hili liliiongezea Serikali mapato kwa kuwa wamiliki wa silaha ambao walikuwa hawajalipia silaha zao walijitokeza na kulipa malimbikizo ya miaka ya nyuma. Hivi sasa Polisi inazo takwimu za kuaminika kuhusu silaha nchini. Takwimu hizo zitakuwa zikihuishwa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kushirikisha sekta binafsi kuunga mkono jitihada za Jeshi la Polisi kukabiliana na uhalifu linaendelea katika mikoa yote na Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Kwa msaada wa Benki ya *CRDB*, kila mkoa umefungua akaunti iitwayo ULINZI WA UMMA, ili watu binafsi, makampuni, mashirika na kadhalika waweze kuchangia kutunisha akaunti hiyo, ambayo fedha zake zinatumika kuwazawadia raia wema wanaotoa taarifa sahihi Polisi zinazowezesha kuzuia uhalifu na hata kuwakamata wahalifu. (*Makofi*)

Mlezi wa akaunti hii kwa mikoani ni Mkuu wa Mkoa. Vilevile sekta binafsi imeitika wito huo kwa kuchangia vitendea kazi kama vile magari, pikipiki, simu za mikononi na kadhalika. Mwamko wa Sekta binafsi ni mzuri. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliojitolea kuchangia jitihada za kupambana na uhalifu kwenye mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imekubali kutoa udhamini kwa Wizara yangu ili *NSSF* ianze kujenga nyumba za askari Polisi kwa awamu. Katika awamu ya kwanza yanatarajiwa kujengwa maghorofa 30 ambapo maghorofa 25 yatajengwa Tanzania Bara na matano Zanzibar. Maghorofa yote yana uwezo wa kuchukua familia 120. Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu wa Majengo (*UCLAS*), na *NSSF* kwa ushirikiano wao uliofanikisha mpango huu. Aidha, napenda kuishukuru Serikali kwa kukubali kudhamini ujenzi wa nyumba hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kulingana na idadi ya askari waliopo sasa linahitaji nyumba 18,000 ili kuwarejesha makambini askari wanaoishi uraiani. Uwezo wa Jeshi la Polisi kujenga nyumba hizi kwa kutumia bajeti yake ya maendeleo inayopata kila mwaka ni mdogo sana. Kwa mantiki hiyo lengo la kuwarejesha makambini askari wote waishio uraiani huenda likachukua muda mrefu. Hata hivyo, Wizara inafikiria kuzihusisha kampuni za nje kujenga kambi za Polisi kwa masharti nafuu ili kuharakisha zoezi la kuwarejesha askari makambini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa, makampuni binafsi ya ulinzi yamekuwa yakitoa huduma ya ulinzi kwa taasisi mbalimbali yakiwemo Mashirika ya Umma, viongozi wa Serikali na hata ofisi za Serikali. Baadhi ya makampuni hayo yamekuwa yakitoa pia huduma ya zimamoto na uokoaji. Pamoja na makampuni haya kutoa huduma, hakuna sera inayotoa maelekezo ya namna huduma hizo zinavyoweza kutolewa kwa wananchi na taasisi mbalimbali kwa ufanisi na haki.

Vilevile watumishi wanaofanya kazi kwenye makampuni hayo wamekuwa hawatendewi haki inavyopasa na pia mishahara yao ni midogo na hailipwi kwa wakati. Kutokana na udhaifu huu, Wizara ya Usalama wa Raia imeanza mchakato wa kuandaa Sera ya Ulinzi wa Makampuni Binafsi, na baada ya Sera kukamilika, itatungwa Sheria ya Ulinzi wa Makampuni Binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Kituo cha Uwekezaji na Mamlaka ya Mawasiliano ya Taifa kupitia utaratibu wa "*Public - Private Partnership*" limeunda Kamati ya Wataalamu ili kuimarisha usalama katika maeneo ya uwekezaji hapa nchini. Moja ya maeneo yenye kutishia usalama ni Sekta ya Mawasiliano ya simu za mkononi. Simu hizi imebainika zinatumika kuwezesha kutendeka makosa ya uhalifu kama utekaji nyara, ujambazi, vitisho, matusi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, makubaliano yamefikiwa kwamba Mamlaka ya Mawasiliano ya Taifa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2007/08 itaanzisha "*Database*" ili makampuni yote yanayouza simu za mkononi yaweze kuzisajili simu zote kwa kupata maelezo ya mtumiaji wa simu husika, na kujua nani mmiliki wa kadi au namba fulani ya simu. Hata hivyo, kufanikiwa kwa zoezi hili kutategemea mambo kadhaa, ikiwemo namna makampuni yanayofanya biashara ya simu yatakavyoshiriki katika zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya askari ni ngumu kwa vile kila wakati anatakiwa kuwa tayari kwa mapambano na wahalifu. Kutokana na hali hii askari hawana muda wa kufanya shughuli nyingine za binafsi za kuwapatia kipato. Tumeshaandaa mapendekezo ya kuboresha maslahi ya askari, hasa wa vyeo vya chini na kuyawasilisha kwenye Kamati ya Taifa ya kushughulikia maslahi ya watumishi wa Serikali.

Hata hivyo, mikakati ya ndani ya Jeshi la Polisi iliyotekelezwa na ile inayoendelea kutekelezwa kwa lengo la kuboresha maslahi ya askari ni pamoja na: (i)kuanzishwa kwa *SACCOS* ya Wizara inayoitwa "*URA SACCOS*"; (ii)kuanza kufufua Kantini za Polisi; (iii) kukamilika kwa makubaliano na *NSSF* ambapo nyumba za askari Polisi zitaanza kujengwa kwa awamu; (iv.) Serikali imekubali kuliuzia Jeshi la Polisi nyumba 22 za *TIPPER* zilizopo Kigamboni. Nyumba hizo zinagharimu shilingi milioni 600 ambazo zimetengwa katika bajeti ya maendeleo ya Jeshi la Polisi kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, malimbikizo ya madeni ya askari na wazabuni ya muda mrefu ni kero kubwa kwa askari na wazabuni. Katika Mwaka wa Fedha 2006/07, Serikali ilitenga shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kulipa madeni ya askari kuanzia mwaka 2001 hadi Juni, 2005. Madeni hayo yalihakikiwa na jumla ya shilingi bilioni 5.4 zilionekana ndiyo madeni halali. Hadi kufikia mwezi Mei, 2007 madeni hayo yalikuwa yamelipwa kwa askari wanaohusika.

Hata hivyo, Wizara bado inaendelea kukabiliwa na malimbikizo ya madeni ya askari kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2005 hadi sasa yanayofikia zaidi ya shilingi bilioni

4 na yale ya Wazabuni ya kuanzia mwaka 2001 hadi sasa yanayofikia shilingi bilioni 11. Ikumbukwe kuwa Jeshi la Polisi lazima litekeleze majukumu yake ya kupambana na uhalifu hata pale ambapo hakuna fedha, hivyo madeni hujitokeza bila ya kutarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuwajumuisha askari Polisi kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, umekwishaanza. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeshaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri, na sasa unasubiriwa uamuzi wa Baraza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, semina za kutoa elimu ya ukimwi zilifanyika. Semina hizo zilijumuisha askari na watumishi wasio askari. Aidha, kwa ufadhili wa *TACAIDS*, Wizara imeanza mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati wa Wizara wa kupambana na Ukimwi sehemu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuelezea hali ya ulinzi na usalama nchini kwa jumla na utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2006/07, naomba sasa kutoa tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Wizara katika kipindi cha mwaka 2006/07. Kwa ujumla utekelezaji wa malengo ya mwaka 2006/07 ulikuwa wa mafanikio. Hali halisi ya utekelezaji kwa maeneo muhimu ilikuwa kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2006/07, Wizara yangu iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya Serikali ya shilingi 5,760,894,000. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2007, makusanyo halisi yalikuwa ni shilingi 6,375,633,024. Makusanyo hayo ni asilimia 110.7 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/07, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako jumla ya shilingi 135,554,751,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 82,826,000,000 ni za Matumizi Mengineyo na shilingi 52,728,751,000 ni Mishahara. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2007 fedha zilizotumika ni shilingi 109,237,672,810 kati ya shilingi 110,774,181,948 zilizotolewa na Hazina. Aidha, kati ya fedha zilizotumika, shilingi 63,775,959,554 ni za Matumizi Mengineyo na shilingi 45,461,713,256 ni Mishahara. Matumizi hayo ni sawa na asilimia 98.6 ya fedha zote zilizotolewa na Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2006/07, Wizara iliidhinishiwa shilingi 7,353,256,300 za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 200,000,000 ni za nje za Benki ya Dunia kwa ajili ya kupambana na Ukimwi ndani ya Wizara na shilingi 658,256,300 ni za *UNHCR* kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama katika makambi ya Wakimbizi katika Mikoa ya Kigoma na Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2007 fedha zilizotolewa na Hazina ni shilingi 5,257,682,156 na fedha zilizotumika ni shilingi 3,271,040,372. Fedha hizo zilizotumika ni sawa na asilimia 62.2 ya fedha zilizotolewa na Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua mbalimbali zimefikiwa katika uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutokana na fedha zilizotengwa katika bajeti

ya 2006/07. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni pamoja na: kuendeleza ujenzi wa Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Mwanza, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Kilimanjaro, Dodoma na Tabora.

Aidha, kazi nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa nyumba tano katika Kituo cha Polisi *Oysterbay,* kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi Muheza, kuendeleza ujenzi wa vituo vya Polisi vya Makambako, Morogoro, Boko na Mapinga, ukarabati wa Ofisi za Kanda Maalumu ya Polisi DSM, ujenzi wa nyumba mbili, moja Unguja Kuu na nyingine Namtumbo.

Vilevile ulifanyika uendelezaji wa ujenzi wa wodi ya watoto Hospitali ya Kilwa *Road* na ununuzi wa vifaa vya hospitali, ujenzi wa maktaba Chuo cha Polisi Moshi, ukarabati wa mabweni mawili Chuo cha Polisi DSM, ufungaji umeme Hospitali ya Kilwa *Road* na Bwalo la Maofisa *Oysterbay*, ujenzi wa visima vya maji *FFU* Ukonga na ukarabati wa Maabara ya Uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2006/07 ni pamoja na:

(i) Operesheni na doria za Polisi zilifanyika katika Mikoa yote.

(ii) Ununuzi wa magari 70 ambapo magari 66 ni ya Polisi na Makao Makuu ya Wizara magari 4 pamoja na ununuzi wa vifaa vya mawasiliano.

(iii) Operesheni za pamoja na nchi za *SADC* za kukabiliana na wizi wa magari, biashara ya dawa za kulevya.

(iv) Upelelezi uliimarishwa kwa ununuzi wa vifaa vya "*Forensic Bureau*" na kuwapatia mafunzo Maofisa wa Upelelezi ndani na nje ya nchi.

(v) Wizara imeanza mchakato wa kuandaa sera tatu za Usalama wa Raia, Polisi Jamii na Ulinzi wa Makampuni Binafsi.

(vi) Maofisa mbalimbali wa Jeshi la Polisi walihudhuria mafunzo ndani na nje ya nchi katika nyanja za ugaidi, madawa ya kulevya, utekaji nyara, wizi wa magari, kuwalinda viongozi wa Kitaifa, na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio niliyoeleza, yapo matatizo yaliyoendelea kuathiri utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mwaka wa Fedha wa 2006/07 yakiwemo ufinyu wa bajeti. Pamoja na ukweli kwamba bajeti ya Jeshi la Polisi imekuwa ikiongezeka kila mwaka, ongezeko hilo halikidhi mahitaji halisi. Matatizo mengine ni upungufu wa askari kutokana na uwiano mkubwa uliopo wa askari kwa raia ambao ni 1:1,300 ukilinganisha na uwiano unaotambulika kimataifa wa 1:450, upungufu wa makazi makambini unaolazimu askari wengi kuishi uraiani na upungufu wa ofisi na vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Jeshi la Polisi yameendelea kuongezeka na kuwa nyeti siku hadi siku kutokana na sababu mbalimbali kama vile kuwepo kwa mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, uelewa mkubwa wa wananchi kuhusu haki zao, ulegezaji wa masharti ya kiuchumi, ubinafsishaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kadhalika. Mambo hayo kwa ujumla wake yamesababisha kuwepo kwa migogoro mingi yenye sura mbalimbali na kusababisha Jeshi la Polisi kuwa tegemeo la wananchi katika kutatua migogoro hiyo.

Ufumbuzi wa migogoro hiyo wakati wote unahitaji fedha nyingi na vitendea kazi kwa kuzingatia kwamba inatatuliwa kwa njia ya operesheni. Aidha, migogoro hiyo hujitokeza bila mpangilio na kwa kushtukiza, hivyo kulazimu kutatuliwa wakati inapojitokeza, bila kujali iwapo fedha zipo au hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2007/08, Wizara imejiwekea malengo mbali mbali katika kutekeleza majukumu yake. Pamoja na kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa ya amani na utulivu, Wizara itaendelea kukamilisha mchakato wa Sera mbalimbali nilizotaja awali, kupokea, kuchambua na kushughulikia malalamiko ya wananchi, kupiga vita rushwa na Ukimwi na kutekeleza miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini kwa kukarabati ofisi na nyumba, kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa vituo na makambi ya Polisi katika Wilaya na Mikoa mbalimbali Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na msisimko mkubwa ulioletwa na Serikali ya Awamu ya Nne wa kuendelea kuthamini michezo, Wizara ya Usalama wa Raia itaendeleza juhudi zake za kushiriki kikamilifu katika michezo. Hivi sasa timu za Polisi Morogoro na Polisi Dodoma zinashiriki katika Ligi Kuu ya Tanzania Bara (*Vodacom Premier League)* ambapo timu ya Polisi Morogoro ilifanikiwa kuingia hatua ya sita bora. Aidha, timu ya Polisi Zanzibar pia inashiriki ligi kuu ya Visiwani. Katika michezo ya Mei Mosi mwaka huu, Wizara ya Usalama wa Raia iliibuka mshindi wa jumla katika michezo ya mpira wa miguu na riadha. Vilevile timu ya Polisi Zanzibar (Wanaume) ni mabingwa wa mchezo wa Mpira wa Pete (*Netball*) wa Kombe la Afrika Mashariki na Kati kwa miaka minne mfululizo.

Hali kadhalika, timu za Polisi Tanzania za Riadha na Mpira wa Miguu ni mabingwa wa jumla wa Michezo ya Majeshi ya Kusini mwa Afrika (*SARPCCO*) yanayojumuisha nchi 13. Tarehe 13 – 26 Agosti, 2007 timu hizo zitakwenda Harare, Zimbabwe kuendelea kutetea ubingwa wao. Pia timu za Polisi Mikoani na Wilayani zipo kwenye madaraja mbalimbali katika mchezo wa mpira wa miguu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kabla ya kumalizia hotuba yangu naomba kutoa shukrani za pekee kwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, (Mb.), Katibu Mkuu wa Wizara ya Usalama wa Raia, Bwana Bakari A. Mahiza, Inspekta Jenerali wa Polisi, Bwana Said A. Mwema, Makamishna, Wakuu wa Idara, Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Vikosi na Wilaya, askari pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Usalama wa Raia ambao kwa ushirikiano wao wamewezesha hotuba hii kuandaliwa na kukamilika katika wakati unaotakiwa. Aidha, napenda kumshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Bwana Cassian Chibogoyo, kwa kufanikisha

uchapishaji wa hotuba hii. Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani wote ambao misaada yao imeiongezea nguvu Wizara yangu katika kutekeleza baadhi ya majukumu yake. Wahisani hao ni pamoja na Serikali za Jamhuri ya Watu wa China, Marekani, Uingereza, Ujerumani, Muungano wa Falme za Kiarabu, Afrika Kusini, Misri, *Morocco, Algeria, Japan,* na Urusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuyashukuru Mashirika ya Kimataifa ya *INTERPOL, SAEU, UNDP, EU*, *Hanns Seidel Foundation*, na wafadhili wa hapa nchini ikiwa ni pamoja na makampuni ya *MM Integrated Steel Mills, SSTL Group*, *Kobil, Agro Vision, Olam and Aulin,* wafanyabiashara, watu binafsi pamoja na wote ambao kwa njia moja au nyingine wanaendelea kuisaidia Wizara ya Usalama wa Raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa shukrani za pekee kwa nchi wahisani za *Canada, Sweden, Denmark* na *Belgium,* Shirika la *UNDP* na Benki ya Dunia ambao wamechangia fedha kwenye mfuko wa kutekeleza Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria *(Legal Sector Reform Programme)* ambapo Wizara yangu ni mdau katika sekta hiyo.Jeshi la Polisi litanufaika na programu hii katika maeneo kadhaa, yakiwemo mafunzo, kuimarisha upelelezi, marekebisho ya sheria na uboreshaji wa mazingira ya kazi.

Katika Mwaka wa Fedha wa 2006/07 Jeshi la Polisi lilipatiwa shilingi 593,676,000 ambazo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nane za askari katika Kambi ya Polisi ya Katubuka Mkoani Kigoma, kufanyia tathmini ya mahitaji ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai na kuendeshea mafunzo ya wapelelezi.

Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu kwa heshima na taadhima likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia ya jumla ya shilingi 146,896,446,000 kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/08.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante! Sasa nitamwita Mwenyekiti ama Mwakilishi wake wa Kamati inayohusika na Wizara hii. Ninaomba wale wote wanaowakilisha wawe wanasogea karibu, ndiyo maana mnaona Naibu Mawaziri wanasogea hapa.

**MHESHIMIWA COL. FETEH SAID MGENI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge,Toleo la Mwaka 2004, nachukua fursa hii kuwasilisha Taarifa na Maoni ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha

2006/2007 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadiro ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kutoa maoni ya Kamati, naomba kutumia fursa hii kueleza masikitiko na majonzi makubwa ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa vifo vya raia wema wasio na hatia walioteketea katika ajali ya Basi la *Mohamed Trans* iliyotokea hivi karibuni huko Singida na ajali ya Basi la *SABCO* iliyotokea Mbeya. Vilevile kwa mshituko mkubwa Kamati imepokea habari za ajali mbili zilizohusisha malori kugonga Daladala Ndogo (*Hiace*) Jijini Dar es Salaam eneo la Uwanja wa Ndege na pia hivi karibuni tu huko Arusha ambako abiria wote 20 waliokuwa ndani ya *Hiace* walipoteza maisha.

Ajali hizo zimetokea wakati ambapo Kamati imetoka kumaliza vikao vyake vya wiki mbili Jijini Dar es Salaam na Wizara ya Usalama wa Raia na kutoa ushauri kwa Wizara hiyo na Serikali kwa ujumla kuandaa maboresho ya Sheria ya Usalama Barabarani kwa kuweza kuwabana zaidi wamiliki wa mabasi ili wawajibishwe zaidi kuwalipa fidia waathirika wa ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inayo majonzi mazito kwa kifo cha Mbunge Mwenzetu, Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, ambaye uhai wake umetoweka mapema mno angali bado kijana na akihitajika sana kwa ustawi wa Taifa letu. Kamati inakupa pole Mheshimiwa Spika na Wabunge wote kwa kupotelewa na Mbunge mwenzetu na hii ikiwa na maana kuwa tumepoteza Mbunge mwingine wa pili katika kipindi cha mwaka mmoja tu. Aidha, Kamati inawapa pole Familia ya Mzee Chifupa, Mpakanjia pamoja na Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Kamati inatoa pole kwa familia, ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge wa zamani wa Mwanza Mjini, Mheshimiwa Stephen Kazi na Wajumbe wengine wawili wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkoa wa Mwanza waliofariki katika ajali ya gari iliyopinduka huko Singida wakiwa njiani kuja Dodoma. Aidha, Kamati inatoa pole kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa zamani wa Jimbo la Kilwa Kaskazini,Mheshimiwa Omari Saidi Chubi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati yanatokana na Taarifa ya Wizara ya Usalama wa Raia iliyowasilishwa mbele ya Kamati tarehe 30 Mei, 2007 na Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara iliyowasilishwa Tarehe 4 Juni, 2007 Jijini Dar es Salaam. Kwa kuzingatia Kanuni Na. 81(1) na (4) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2004, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 pamoja na Ushauri wa Bunge uliotolewa kwa Wizara hii. Aidha, Kamati ilipitia Mafungu ya Makadirio ya Fungu 28 kwa Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara hii, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kwa juhudi zake zinazoifanya nchi yetu iendelee kuwa na Utulivu na Amani katikati ya nchi zenye vurugu na migogoro inayofukuta kila pembe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningependa kutumia fursa hii kumpongeza Waziri wa Usalama wa Raia, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed, Katibu Mkuu, Ndugu Bakari Mahiza na wataalamu wote wa Wizara kwa juhudi wanazoendelea kuzifanya katika kuboresha Utendaji wa Jeshi la Polisi na kuweza kushirikiana vyema na wananchi katika kukabiliana na matatizo ya ujambazi. Aidha, naipongeza Wizara kwa kuandaa na kuwasilisha mbele ya Kamati Taarifa inayoelezea bayana utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ningependa kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, *IGP* Said Mwema na Makamanda wake kwa kuweza kukabiliana na ujambazi. Lakini zaidi natoa pongezi kwa Kamanda Venance Tossi kwa kuongoza operesheni yenye mafanikio makubwa mkoani Kagera kukabiliana na majambazi yakiwemo yanayotoka nchi jirani yaliyokuwa yakisababisha usumbufu mkubwa katika mkoa huo na mikoa mingine ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa namna ambavyo wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe wa Kamati wamekuwa bega kwa bega katika kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kutoa maoni yao na ushauri ambao Wizara imekuwa ikifanyia kazi. Ningelipenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa William J. Kusila, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Col. Saleh A. Farrah, Mheshimiwa Mohamed A. Abdulaziz, Mheshimiwa Maria I. Hewa, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Dr. John S. Malecela, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Col. Feteh S. Mgeni, Mheshimiwa Benson M. Mpesya, Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, na Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda.

Vilevile namshukuru sana Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. L. Foka na Sekretarieti ya Kamati, Ndugu Peter Magatti na Ndugu Patson A. Sobha, kwa kazi na huduma nzuri wanazotoa kwa Kamati na hivyo kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na hata kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Juni, 2007, katika kikao cha Kamati kilichofanyika jijini Dar es Salaam, Waziri wa Usalama wa Raia, aliwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati na Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007. Kamati ilipokea na kuchambua kwa kina Taarifa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipata malezo ya kina toka kwa Waziri ambaye alieleza Dira, Mwelekeo na Majukumu ya Wizara, Utekelezaji wa Maagizo/Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2006/2007 pamoja na kuelezea mafanikio na matatizo ya utekelezaji katika mwaka wa Fedha wa 2006/2007.

Aidha, Kamati ilipata maelezo ya kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2007/2008 na Maombi ya Fedha za Matumizi kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara hii imetekeleza kwa kiasi kikubwa majukumu yake na pia imeyafanyia kazi Maoni na Ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na utekelezaji wake unaonekana dhahiri. Pamoja na mambo mengine, Wizara imeonyesha mafanikio katika utekelezaji wa masuala mbali mbali kama:-

Kuimarisha Hali ya Usalama Nchini;kudhibiti Hali ya Uhalifu; kuanza Mchakato wa Kuandaa Sera ya Usalama wa Raia;mchakato wa kuunda Kikosi Maalumu cha Kulinda Watalii;mchakato wa Kurejesha Ulinzi wa Polisi katika Bandari;kuangalia upya Muundo, mfumo, sheria na Kanuni za Jeshi la Polisi;mchakato wa kunzisha Polisi Jamii; nakuboresha maslahi ya askari Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika maeneo mengine ambayo Kamati imeona kuna upungufu na juhudi zaidi zinahitajika, Kamati ilishauri na kutoa maagizo ipasavyo yakiwemo masuala yafuatayo:-

Tatizo la Mwekezaji wa Utalii Serengeti kuwa na Kikosi chake cha Ulinzi;maeneo Nyeti ya Nchi kama Vile Bandari kulindwa na Walinzi wa Kampuni za Kigeni;tatizo la Usalama Barabarani;Udhibiti wa Matumizi ya *SIM – Cards*;uhamiaji Haramu;biashara haramu ya Usafirishaji Binadamu; dawa za Kulevya; namigomo ya Wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio ambayo Kamati iliyaainisha, pia kulikuwepo na matatizo yaliyojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2006/2007 kama ifuatavyo:

(i) Tatizo kubwa ambalo limeathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2006/2007 ni upungufu wa fedha katika kutekeleza mipango mbalimbali ya Wizara. Upungufu huu umeathiri utendaji katika jeshi la Polisi kwani kuna upungufu wa idadi ya askari kutokana na uwiano mdogo uliopo kati ya askari na raia kuwa 1:1300 wakati Kimataifa inatakiwa kuwa 1:500.

(ii) kukosekana makazi ya kutosha kwa askari wetu katika Makambi na hivyo kuwafanya waendelee kuishi uraiani.

(iii) upungufu wa Ofisi na Vitendea kazi kama vile: magari, pikipiki na vyombo vya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2007/2008. Katika Makadirio hayo Wizara ya Usalama wa Raia inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 146,896,446,000/= kwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo.

Kati ya Fedha hizo, shilingi 75,013,260,000/= zikiwa ni Matumizi Mengineyo (*OC*) na shilingi 66,366,186,000/= ni Mishahara. Bajeti ya Maendeleo imetengwa shilingi 5,517,000,000/=

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulinganisha na bajeti ya mwaka 2006/2007, bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2007/2008 imeongezeka kwa Jumla ya Shilingi 4,696,438,700/= ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 3.3. Hata hivyo, ongezeko hilo limetokana zaidi na kuongezeka kwa mishahara kutoka shilingi 52,728,751,000/= mwaka 2006/2007 na kuwa shilingi 66,366,186,000/= mwaka 2007/2008/=.

Aidha, kuna punguzo la bajeti katika Matumizi Mengineyo na katika fedha za Maendeleo. Fedha za Maendeleo zimepungua kwa Shilingi 1,836,256,300/=, wakati fedha za Matumizi Mengineyo zimepungua kwa shilingi 7,104,740,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2007/2008, sasa naomba kutoa ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa Mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Usalama Barabarani na Kupunguza Msongamano:-

(i) Kamati inashauri kuwepo kwa mkakati imara wa utaratibu wa Mabasi yaendayo Mikoani kuwa na Ratiba maalumu ya Kuondoka na kufika kwa muda uliopangwa. Ratiba hizo zibandikwe ndani ya basi husika.

(ii) Sheria ya Usalama Barabarani iboreshwe ili kuwabana Wamiliki wa Mabasi kuwajibika kulipa Bima kwa wote wanaoathirika na ajali kwa basi husika.

(iii) Serikali iimarishe vitendea kazi vya Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na vifaa vya kupimia mwendo wa magari.

(iv) Serikali iimarishe elimu ya Usalama wa Barabarani ili alama za kuepusha ajali zitumike vyema.

(v) Kampuni Binafsi za Ukaguzi wa Usalama wa Magari zianzishwe chini ya Uangalizi wa Wizara ya Usalama wa Raia.

(vi) Serikali itumie Askari Kanzu kusafiri na Mabasi yaendayo mikoani na kurekodi mwenendo wa basi na wahudumu wake na kisha kutoa taarifa basi lifikapo mwisho wa safari.

(vii) Kwa upande wa mijini, kuwepo na operesheni maalumu ya kukomesha upakiaji na usimamaji ovyo wa mabasi ya abiria katika sehemu zisizo na vituo.

(viii) Serikali idhibiti Watumiaji wa viatu vya magurudumu *(Rollers)* wanaodandia na kujishikiza katika magari yaliyo katika mwendo.

(ix) Serikali ihamasishe Wawekezaji Binafsi wawekeze katika Boti za kusafirisha abiria kati ya Jiji la Dar es salaam na sehemu zote zilizo kando kando ya Bahari ya Hindi katika Mpango mpya wa kupunguza msongamano Jijini Dar es salaam.

(x) Serikali Kuu ichukue Jukumu la kumiliki na kuhudumia Barabara za Jiji badala ya kuziachia Manispaa.

(xi) Suala la kuimarisha usafiri wa Umma litiliwe mkazo badala ya kila mtu kuwa na usafiri wake wakati wa kuingia na kutoka Jijini.

(xii) Wadau mbali mbali wa barabara washirikishwe katika kutatua tatizo la Msongamano wa magari Jijini Dar es salaam badala ya kuuachia mzigo huu Jeshi la Polisi peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Biashara Haramu ya Kusafirisha Dawa za Kulevya:-

(i) Serikali iimarishe ulinzi wa Mipakani, Viwanja vya Ndege na Bandari ili kudhibiti biashara haramu ya kusafirisha dawa za kulevya. Aidha,Serikali iwe makini zaidi na wahamiaji kutoka Pakistan na Somalia ambako kuna viashiria vya makundi ya kigaidi kuweza kujipenyeza.

(ii) Serikali itoe semina na mafunzo zaidi kwa askari wetu ili waweze kukabiliana na Biashara ya Kusafirisha dawa za kulevya.

(iii) Serikali ishirikiane na nchi zingine zilizopiga hatua katika mapambano dhidi ya bishara haramu ya kusafirisha dawa za kulevya.

(iv) Serikali inunue Mbwa Maalumu wengi zaidi wa kubaini dawa za kulevya kwa kuwa waliopo wamechoka na ni wachache.

(v) Serikali iimarishe mapambano dhidi ya Wasafirishaji, Wauzaji na Watumiaji wa Dawa za kulevya na iweke kipaumbele kwa upande wa Zanzibar katika mapambano yake dhidi ya Dawa za Kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ujambazi:

(i) Jeshi la Polisi liendeleze na kuimarisha mpango wa Polisi Jamii.

(ii) Serikali iimarishe Operesheni ya mara kwa mara katika maeneo yenye wimbi la ujambazi kama aliyofanya Kamanda Venance Tossi katika Operesheni huko Kagera.

(iii) Helkopta za Polisi zitumike kufanya Doria ya kushtukiza katika maeneo sugu kwa ujambazi na uharamia.

(iv) Serikali inunue Boti za Ulinzi katika Bahari na Maziwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuingilia Mawasiliano:-

(i)Kamati ilishauri kwamba kuna umuhimu wa kuingilia mawasiliano ya Simu ambayo Polisi wanatilia mashaka. Hata hivyo, suala hili lichukuliwe kwa umakini sana ili kutoingilia uhuru wa watu na mambo yao ya ndani na pia kusababisha usumbufu kwa wageni.

(ii) Kuwe na utaratibu wa *Sim – Cards* kununuliwa kwa usajili maalumu badala ya sasa kila mtu ananunua popote na kutumia anavyotaka na kisha kutupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Makampuni ya Ulinzi:-

(i) Serikali ifuatilie kwa makini suala la Kampuni Binafsi ya Ulinzi kwa Mwekezaji wa Utalii Serengeti.

(ii) Wafanyakazi wa Kigeni katika Makampuni ya Ulinzi wasiruhusiwe kulinda maeneo nyeti kama vile Bandari.

(iii) Serikali iharakishe Ujenzi wa Kituo cha Polisi Bandarini

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Askari Polisi na Raia:

(i) Serikali ifanye jitihada za kuongeza idadi ya Askari Polisi ili angalau uwiano wa askari mmoja kwa raia uwe mzuri ili kuondokana na uwiano mdogo wa sasa wa Askari kwa raia.

(ii) Askari wahudumiwe kwa namna tofauti na watumishi wengine wa Umma. Hata bajeti ya Idara ya Polisi isilinganishwe na Taasisi zingine.

(iii) Jeshi la Polisi liwe na Utaratibu wake wa Bima ya Afya.

(iv) Iundwe Tume ya Vyombo vya Majeshi ili kushughulikia maslahi ya Askari.

(v) Uundwaji wa Sera ya Usalama wa Raia uharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga Mkono Hoja na naomba kuwasilisha. (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Asante! Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na shughuli yetu ya leo, napenda pia niwatambulishe wafuatao:- Kamishna Msaidizi, Venance Tossi ambaye mmemsifu vizuri sana hapa na sisi sote tunakiri, yuko hapa, yeye ni Kamishna wa Operesheni Makao Makuu – Polisi. Amesimama yuko huku? Amekwenda kazini! Kwa hiyo, wako kazini kwa watumishi wanaofanya kazi. Halafu pia naomba nimtambulisheKamanda James Kombe, Kamishna Msaadizi Mwandamizi wa Usalama Barabarani.

Vilevile naomba nimtambulishe Kamishna Msaidizi, Mussa Ali Mussa wa Operesheni Zanzibar. Kwa hiyo, mnaona tofauti, wamekuja huku kwa sababu sasa wako kazini, kwa sababu wakikaa wageni katika *Public Gallery* hii huku mbele yetu, hawapaswi kuandika wala kusoma. Wanaokaa hapa na hapa, wanaweza kuandika na kusoma. Kwa hiyo, ndiyo maana wamekaa huku. Karibuni sana tunashukuru kwa kazi zenu nzuri. *(Makofi)*

Tunaendelea! Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Mheshimiwa Sanya! Leo umetokea na suti kabisa! (*Kicheko)*

**MHE. IBRAHIM MOHAMED SANYA – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Naibu Spika, si ndio najitayarisha mwaka 2010 kuchukua uwaziri bwana! *(Kicheko)*!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema nikachukua fursa hii kwa kuwaombea ndugu zetu waliotangulia mbele ya haki, nao ni marehemu Juma Jamaldin Akukweti na marehemu Amina Gabriel Chifupa. Wote hawa Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi, *Amin!* Na sisi atupe hatima njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, hatuna budi kumshukuru Mola wetu kwa kutuwezesha kuwepo hapa na kuwa na afya njema inayotuwezesha kuwatumikia wananchi wote wa nchi hii. Napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2004, Kanuni ya 43 (5) (b) (c) na 81 (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwako wewe binafsi na kwa Mheshimiwa Spika na wenyeviti wako wanaokusaidia. Nitakuwa nimekosa hekima na busara kama nitashindwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa jimbo la Mji Mkongwe Zanzibar kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia katika kuhakikisha kazi zangu kama mbunge wao nazifanya vizuri.

Aidha, nakishukuru chama changu cha wananchi (*CUF*) kwa kuzidi kuniunga mkono katika jitihada zangu za kuwa mbunge mahiri na pia kwa mashirikiano na viongozi wenzetu wa vyama vya upinzani katika kuonyesha mwelekeo halisi wa demokrasia katika nchi yetu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa pongezi na shukrani za dhati kwa Viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kazi yao kubwa ya kuiongoza kambi yetu. Aidha, nitumie nafasi hii kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Bakari Mwapachu na Naibu wake , Mheshimiwa Mohammed Aboud, kwani hawa ndio vinara na wapishi watakaoweza kuonesha ukomavu wao wa kisiasa wakisaidiana na watendaji wote katika wizara hii. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa hapa Bungeni mwaka jana, aliweka bayana majukumu saba ya Wizara hii ambayo ilianzishwa kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 1 la Januari 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alisema kwamba majukumu haya ni baadhi tu, lakini lazima tuelewe kuwa hii ni Wizara ya Serikali ambayo imepewa mamlaka na watanzania kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Hivyo ingekuwa busara zaidi kama Mheshimiwa Waziri akaainisha majukumu yote ya Wizara na sio saba tu, ili yajulikane na Watanzania wote kupitia Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kuokoa muda mimi nitayatolea maelezo mafupi majukumu mawili tu miongoni mwa hayo saba, nayo ni:-

(i) Kushirikisha jamii katika kuweka mikakati ya kuzuia uhalifu kupitia utaratibu wa Polisi Jamii. Hatua hii ni ya busara na inastahili kuungwa mkono na watanzania wote. Lakini askari polisi wanatakiwa wao wenyewe wawe ni chachu ya jukumu hili na kuondosha ile dhana kwamba jeshi la polisi haliko makini katika kazi zake za kuzuia uhalifu, na kazi yao ni kuwabambikizia kesi raia wasio na hatia pamoja na kushirikiana na wahalifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake hawatokuwa waangalifu basi mradi huu utashindikana, kwani inasemekana kuwa baadhi ya askari polisi huwasaliti wale watu ambao hushirikiana nao katika kuibua magenge haya ya wahalifu.

Vilevile baadhi ya watendaji katika ngazi mbalimbali za Serikali kama vile baadhi ya Masheha kule Zanzibar inasemekana hukataa kutambua makundi ya jamii yanayotaka kushirikiana na polisi katika kutekeleza jukumu hili. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo tunaiomba Wizara hii ihakikishe kwamba askari polisi yeyote atakayetoa siri za raia wema aonekane kuwa ni msaliti katika jeshi hili, na iwapo atabainika kufanya hivyo baada ya kufanyika uchunguzi basi achukuliwe hatua kali dhidi yake ikiwemo ya kufukuzwa kazi.

(ii) Jukumu la pili ni kusimamia maendeleo ya watumishi wa Wizara hii. Pamoja na mambo mengi ambayo Serikali hufanya ili kuboresha maslahi ya watumishi na watendaji wake katika Wizara hii, lakini napenda kusisitiza kwa kutoa wito wangu kama nilivyosema katika kipindi kilichopita kwamba askari polisi ni lazima wakatiwe bima za maisha kupitia mfuko wa Serikali.

Sote tunaelewa vyema kwamba askari polisi ni mlinzi na mpiganaji anayeweza kutumia silaha za moto pindi ikitakiwa kufanya hivyo wakati wa dharura, na uwezekano wa kupoteza maisha au kupoteza kiungo au viungo kwa kujeruhiwa ni mkubwa na matokeo kama haya bado tunayashuhudia yakiendelea. Hivyo basi ni stahiki yao kabisa kwa Serikali yao kuwawekea bima ya maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema vilevile tukaangalia vigezo vya mafao ya askari polisi kwa nchi za Afrika Mashariki, *SADC,* na zile za Jumuiya ya Madola ili vitumike kuboresha maslahi kwa jeshi la Polisi la Tanzania. Hatua hii ikitekelezwa vyema itaongeza ari ya kiutendaji kwa askari wetu, na lile lengo lililokusudiwa linaweza kufanikiwa kwa kiasi cha kuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 9 (g) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, naomba ninukuu, inasema kwamba : "Serikali na vyombo vyake vyote vya umma vinatoa nafasi zilizo sawa kwa raia wote; wake kwa waume, bila kujali rangi, dini, kabila au hali ya mtu." Ibara ya 13( 5) imetoa ufafanuzi wa neno kubagua kama ifuatavyo: "ni kutimiza haja, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbali mbali kwa kuzingatia utaifa wao, kabila, pahali walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini….." , mwisho wa kunukuu. Kwa haki hiyo ya kikatiba ajira katika jeshi la polisi ni haki ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwiano katika jeshi la Polisi kama chombo cha Muungano ni jambo muhimu sana. Sura iliyopo sasa hivi kwa maofisa wengi waliopo Zanzibar sio sura halisi inayotakiwa katika jeshi letu, maofisa wengi ni kutoka ama Tanzania Bara au Unguja. Lakini kutoka katika kisiwa cha Pemba nafasi kama hizi huwa hazilingani na nafasi wanazopewa wenzao.

Hii inadhihirisha maudhui ya kwamba jeshi hili lina kasoro inayoweza kurekebishwa kwa dhamira nzuri ya kuleta uwiano wa madaraka ya kazi kwa pande zote za Muungano. Ni imani ya Kambi ya Upinzani kwamba haki hii itawafikia Watanzania wote ili kuzidi kuendeleza Taifa letu katika hali ya umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jeshi la Polisi na Kusimamia Demokrasia Nchini katika ujenzi wa demokrasia ya kweli, na kwa dhamira nzuri, taifa letu linalazimika kufanya mabadiliko mazito katika taasisi zake nyingi ili kuondoa dhana ya chama kushika hatamu. Moja kati ya mabadiliko haya yanavihusu vyombo vyote vya ulinzi kwa ujumla wake lakini kwa hapa leo nitagusia jeshi la polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Umoja wa Mataifa inayoitwa, *United Nations International Police Task Force* inasema, naomba ninukuu: "*In democratic society the police serve to protect rather than to impede freedoms. The very purpose of police is to provide a safe, orderly environment in which these freedoms can be exercised.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kujiuliza ni: je, jeshi letu la Polisi linaendana na nukuu hiyo? Kulingana na hali halisi iliyopo katika jamii ya kitanzania inayoanza

kuzoea mfumo wa siasa za vyama vingi, Jeshi la Polisi limekuwa likitumiwa kukwamisha ustawi wa mfumo huu. Mifano halisi ni malalamiko mbalimbali kutoka kwa viongozi wa vyama vya siasa katika ngazi mbali mbali za uongozi. Lakini Bunge kama muhimili mmoja wa dola ambalo linawawakilisha watanzania wote wawe na kauli moja ya kulifanya jeshi hili liwe la ulinzi na usalama kwa kuhakikisha uhuru wa mtu mmoja mmoja au kikundi vinalindwa kwa mujibu wa Katiba na sio vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa minajili ya kuleta mfumo mpya ndani ya Jeshi la Polisi basi ni vyema Sheria Namba tano ya Mwaka 1992 ikatumika ipasavyo. Sheria hii ndiyo iliyofungua milango ya siasa ya vyama vingi hapa Tanzania. Sheria hii imetamka wazi kutohusisha taasisi za umma na vyombo vya Ulinzi katika harakati za kisiasa. Lakini inasemekana kwamba baadhi ya askari polisi bila kificho wala woga hawajaonesha kubadilika kitabia katika mfumo wa siasa za vyama vingi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jarida la *Human Right Resource Book for SADC Parliamentarians* lililotolewa katika mkutano wa *SADC PARLIMENTARY FORUM,* Aprili, *2000, Cape Town,* Afrika Kusini, katika ukurasa wa 53, kipengele cha 3(e) kinasema: “Kuhakikisha kwamba matumizi ya nguvu za kipolisi yanatekelezwa kwa mujibu wa sheria za nchi na maadili ya kazi zao, na kwamba polisi mwenyewe awajibike kwa kuvunja sheria za nchi na maadili ya kazi yake.”

Mheshimiwa Naibu Spika, imezoeleweka kusemwa kwamba kazi ya polisi ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Katika lugha za kisheria falsafa hii huitwa, *maintaining law and order;* lakini watafiti wamebaini kuwa wajibu huo wa polisi *has no reference to the protection of human rights. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika wakati kama huu wa kuendeleza mifumo ya kidemokrasia duniani, utandawazi na azma ya kuelekea kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki, Jeshi la Polisi lazima liwe na wajibu kama ifuatavyo:-· (i) Lazima jeshi lijengwe katika misingi ya uwajibikaji (Hakuna kulindana).·(ii) Polisi wawajibike kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Nchi. Wawajibike katika kuendeleza mifumo ya kidemokrasia na ile ya kijamii· (iii) Watoe kipaumbele katika kulinda usalama, Haki na mali za watu wote kwa mujibu wa Tamko la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Binadamu (ambalo Tanzania imeliridhia); (iv) kutoa huduma za kitaalam na zinazokubalika (sio kubahatisha na kubambikizia watu kesi ); (v) Polisi wawe ni wawakilishi wa jamii wanayo ihudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko makubwa ya matumizi ya teknolojia Duniani, huambatana na majambazi ambayo hutumia teknolojia ya kughushi nyaraka bila ya kutumia silaha au nguvu kama ilivyozoeleka.Kuna kitu kinaitwa *organized crime,* aina hii ya uhalifu ambao mara nyingi hufanywa na watu wenye taaluma ya hali ya juu kabisa. Hivyo huu ni wakati mwafaka kwa jeshi letu la polisi nao wakafunzwa na kuwa na taaluma pamoja na nyenzo za kisasa ili kukabiliana na uhalifu kama huu pindi utatokea, hasa katika taasisi zetu zote za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi litarudisha heshima yake kwa raia na pia kuaminiwa iwapo tu kazi zao zitalenga matakwa ya umma na kuwa na ari na moyo katika kuyalinda yale makundi yaliyo dhalili kama vile watoto, walemavu, wagonjwa, wazee na hata akina mama wanaodhalilishwa au hata kuuawa kwa imani za kishirikina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili Serikali iepukane na mzigo mkubwa wa mahabusu, ni lazima jeshi la polisi kuwa makini kwa kufanya upelelezi wa kina wa kesi kabla ya kumweka mtuhumiwa mahabusu.

Hii itasaidia upelelezi kufanyika kwa haraka ili upatikane ushahidi sahihi kabla ya kuchukua hatua za kumweka mahabusu, na vilevile kuondokana na uvunjwaji wa haki za binandamu kwa mtuhumiwa. Iwapo mtuhumiwa atakuwa mahabusu na huku uchunguzi ukiwa unaendelea unaweza kutoa mwanya kwa maafisa uchunguzi kutumia nafasi zao kazini kwa manufaa binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajali za barabarani bado ni tatizo ambalo jeshi la polisi limeshindwa kulidhibiti. Hivyo Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Wizara yake ya Usalama wa Raia, kuunda Kamati Maalumu ya wataalamu kutoka katika Jeshi la Polisi lenyewe na wataalamu kutoka katika idara nyingine za Serikali na katika taasisi za watu binafsi ili kuangalia na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili ambalo limekuwa sugu na linalosababisha vifo vingi pamoja na majeruhi ambao wengi wao hubaki kuwa walemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ujambazi kwa kweli umefika wakati sasa kwa jeshi letu la polisi kufanya kazi za ziada ili kuutokomeza kabisa ujambazi katika nchi yetu. Ule wakati wa kupongezana pongezana umekwisha, ni lazima usimamizi wa uchumi wetu uende sambamba na ulinzi wa uhakika kwa raia na mali zao hasa ukizingatia tunao wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika matokeo ya hivi karibuni inaonekana kuwa hali ya mipaka yetu sio shwari kama tunavyoamini. Hapa simaanishi baina ya nchi yetu na nchi jirani kisiasa, lakini hoja ni kwamba vipi raia kutoka nchi jirani kuingia na silaha nzito nzito yakiwemo mabomu ya kuzika na ya kutupa, *SMG,* bastola na risasi kadhaa na hata kupatikana na nguo maalumu za kujikinga na risasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi wameingizaje bidhaa hizi hatari kupitia mipakani au tuseme wamezipata hapa hapa nchini? Leo vijana wetu wanaofanya biashara ya kuingiza sukari kwa njia za panya huwa wanakamatwa mara zote kule mpakani Mbeya, lakini inashindikana kuwakamata raia kama hawa wa kigeni ambao hujiandaa kuja kufanya ujambazi na huwa wanapata fursa ya kuingia na silaha hizo nzito mpaka mijini bila ya kukamatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile inawezekana fedha walizokamatwa nazo zikiwemo za Tanzania na za kigeni ndizo zinazotumika kuwahonga raia wetu au hata baadhi ya askari wasio waaminifu ili wapate kutekeleza azma yao ya ujambazi. Ni

vyema sasa tukajipanga vyema maeneo ya mipakani hasa upande wa Arusha kwani inaonekana kuna matetemeko, sio ya ardhi tu bali hata ya ujambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kutoa mamlaka ya kipolisi kwa taasisi nyinginezo kwa kiasi fulani imeanza kujiimarisha kwa upande wa Tanzania Bara. Makampuni binafsi yanayojishughulisha na kazi za kiulinzi kwa raia na mali zao yanazidi kusajiliwa. Kimsingi huu ni utaratibu mzuri ambao unafuata mkondo wa Sheria na kwa kiasi fulani unasaidia kutoa ajira na kuweka hali ya usalama kwenye maeneo mengi ya kazi. Lakini hatua ya kuikabidhi kampuni ya Ulinzi binafsi kulinda mpaka wa Tanzania na Kenya kule Sirari Mkoani Mara haukuwa uamuzi wa busara. Bahati nzuri waandishi wa habari waliliona hilo na kulitolea taarifa na tunaipongeza Serikali kwa kuchukua hatua za haraka kuweka mambo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa inaonesha kuwa uwiano wa askari na raia kwa Tanzania kwa sasa ni 1:1300. Baadhi ya vyombo vya habari vimetoa takwimu ya 1:1500 kama ilivyotolewa na Kurugenzi ya *U.N. HABITAT* Tanzania. Kiwango cha kimataifa kinachokubalika ni 1:400 – 600. Hii ni kusema askari wa Tanzania ana kazi mara mbili kwa kulinganisha na kiwango hicho cha kimataifa. Lakini inawezekana pia ikawa uzito wa kazi yake ni mara 12 kwa kukosa vitendea kazi, mafao na huduma zisizoridhisha na uhaba wa elimu inayoendana na wakati kwa mujibu wa kazi zake. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ndogo ya (1) ya Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano inatamka: ” Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.” Katika nchi maskini kama yetu huduma za jeshi la polisi huonekana kufanya kazi zaidi katika maeno ya mijini, maeneo yenye watu matajiri au utajiri sana na kuyaacha maeneo mengine hasa ya vijijini wakiwa mbali na chombo hiki muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufanikisha azma njema kwa kila raia lazima ikumbukwe umuhimu wa askari kwa usalama wa raia. Na kwa hiyo hata wale polisi waliopangiwa maeneo ya mbali na miji ya mikoa au wilaya basi ni vyema wakapewa uhakika wa kiutendaji kwa kuwapatia nyenzo muhimu za kazi yao. Aidha, si busara kwa Mtanzania wa kijijini kusafiri eneo refu ili kufuata huduma ya kipolisi. Hili tulizingatie sana ili kuondoa dhana ya upendeleo kwa chombo hiki muhimu kwa usalama wetu sote. Hatua hizi za kufanya huduma za kipolisi kuwa karibu zaidi na maeneo ya aina mbalimbali ya kiraia zitasaidia sana katika:-·

Kupunguza ujambazi, uharamia na unyanyaswaji wa raia hasa wale ambao tunawaita kwa kitaalamu, *marginalized* au *vulnarable groups and individuals;* Itapunguza hofu miongoni mwa raia na kuwapa matumaini ya usalama katika shughuli zao za kila siku; na·itaongeza matumaini ya kiusalama katika maeneo ya kazi, kama vile mashule, kliniki, mahoteli ya utalii na kwenye mbuga zetu na pia itasaidia kudhibiti makosa mengi yahusianayo na usafiri, yaani *traffic safety.*

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji wa Serikali hutegemea bajeti. Hivi sasa tumo katika kujadili hilo kwa ajili ya Wizara ya Usalama wa Raia. Kimsingi jeshi la Polisi ni

chombo cha kutoa huduma. Kwa hiyo, hakitegemewi sana katika kuchangia pato la taifa. Pato ambalo hukusanywa na jeshi hili ni lile la utozwaji faini kwa uhalifu wa sheria za usalama barabarani. Lakini hata pato hili dogo huwa kwa kiasi fulani haliwasilishwi serikalini kwa ukamilifu wake. Na ni vyema pato hili likabaki katika miji inayolikusanya na kununuliwa vifaa mbalimbali vya kutendea kazi kama vile, *motor bikes,* zana za mawasiliano na *jackets* za mvua kwa askari husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kwa sababu ya upya wa Wizara hii na kwa mujibu wa majukumu yake basi lazima Serikali iweke fungu la kutosha ili kufanikisha yaliyokusudiwa. Tukiweka upande suala la mafunzo ya awali kwa ajili ya kazi za kipolisi na asasi zake, lakini watendaji wa wizara hii iwe wale wanaohusika na mambo ya kiutawala au wanaokuwa kwenye *field.* Lazima sasa tubadilike na kuleta taswira nyingine mbele ya jamii ya ndani na nje ya nchi yetu.

Kwa mujibu wa taarifa za Mheshimiwa Waziri kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Wizara inakusudia pamoja na mambo mengine, kutekeleza yafuatayo: Kuajiri vijana wenye elimu bora; kuongeza na kuboresha maslahi ya kipolisi na kulipa madeni yao; kuimarisha Idara ya upelelezi; kutoa elimu ya uraia; kutoa zawadi kwa wanaotoa taarifa za uhalifu; kuwa na *Joint military operations*. Yote haya na mengine mengi lazima yatekelezwe kwa kuligana na hali halisi ya kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa namna nchi yetu ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya taarifa za fedha za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2006 inaonesha upungufu mwingi sana wa udhibiti wa fedha za serikali kwa Wizara ya Usalama wa Uraia. Baadhi yake ni kama ifuatayo:- Upotevu wa fedha taslimu na vifaa jumla mil.200.5; ununuzi wa kutozingatria zabuni – shilingi milioni 235.6;

Ukosefu wa nyaraka za makubaliano ya Mikataba ya Ujenzi wa Nyumba na Ofisi za polisi – shilingi bilioni 2.7; malipo kwa kutumia ankara kifani – shilingi milioni 31.5.Kama Wizara haitakuwa makini, siku zote itakuwa inatengwa fedha na kupotea katika hali kama hii na kulifanya jeshi la polisi lisifikie malengo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukubwa wa nchi yetu kijiografia na tatizo la uhaba wa vitendea kazi kama vile kila mmoja wetu anavyoelewa, hivyo askari polisi wa ngazi za chini wamekuwa wakikabiliwa na tuhuma za kupokea rushwa ndogo ndogo toka kwa wananchi. Inasemekana kwamba baadhi ya askari hupangiwa kufanya kazi sehemu zilizo mbali na nje ya vituo vyao kwa mujibu wa taratibu za za jeshi hilo. Lakini jambo ambalo si la busara ni kuwataka watumie fedha zao za mifukoni kujigharamia wenyewe, na kuahidiwa kuwa mara wataporudi vituoni watalipwa kwa kuwasilisha madai yao kwa wakuu wao wa kazi, hali ambayo huchukua muda mrefu kupata marejesho yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia hali halisi ya kipato cha askari wetu, hakuna asiyeelewa kuwa ni kipato kinachomwezesha mkono kwenda kinywani tu, au kwa lugha nyingine ni kusema "*from hand to mouth.*"

Si vyema askari kutumia fedha zao, jambo hili linaweza kuzaa mianya ya kupokea rushwa na kurejesha nyuma nguvu zao za kulinda raia na mali zao na kukosekana kwa ufanisi wa utendaji katika jeshi la polisi.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilitolee tamko suala hili la askari kutumia fedha zao au kumtaka raia achangie usafiri au mafuta kwa vile kituo anachokwenda kutoa taarifa huwa kinakosa huduma kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Serikali kutambua kwamba kila askari wa jeshi la polisi hufanya kazi kwa mujibu wa sheria, lakini vilevile ni vyema tukatambua kwamba hata kama watafanya hivyo bila ya kuangaliwa maslahi yao, itakuwa ni kujidanganya.

Polisi lazima wawezeshwe kwa kupata vitendea kazi bora na vya kisasa lakini sambamba na hilo lazima yaangaliwe maslahi yao yatakayotoa ari na utulivu wa kufanya kazi zao vyema.

Polisi kwenda likizo bila posho ni tatizo sugu katika Wizara hii na huwa haitolewi kwa wakati mwafaka. Usafiri na makazi bado ni kitendawili ingawaje kuna mipango ya muda mrefu ya kujenga maghrofa kwa pande zote mbili za Muungano kwa kushirikiana na *NSSF*.

Vilevile ieleweke kuwa askari anapopata uhamisho ni vyema wakati akipokea barua yake hiyo lazima iambatane na posho ya kumsafirisha yeye na familia yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kustaafu ni haki ya kila raia anayeajiriwa, lakini katika jeshi la polisi hata unapofikia wakati wa kustaafu huwa kunakuwa na usumbufu wa kupata mafao yako. Ni vyema hili likaangaliwa kwa kina ili mstaafu apate haki zake mara tu anapomaliza muda wake wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie hotuba yangu hii kwa kunukuu maneno mazuri sana yaliyotolewa na mtoa mada wa Jeshi la Polisi kwenye semina ya Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge lako Tukufu hapa Dodoma tarehe 17 April 2007.

Mtoa mada alisema: "Utekelezaji wa maboresho ya Jeshi la Polisi unahitaji gharama kubwa. Gharama hizi zinatakiwa zitokane na mapato ya ndani au kutoka kwa wafadhili.

Hapa panahitaji kuzingatia athari za Jeshi la polisi kufanyiwa maboresho na wafadhili kwa kuwa watakuwa na haki ya kuelekeza mwelekeo". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba yetu ya bajeti iliyopita tulitoa tahadhari kuhusu misaada ya wafanyabiashara kwa jeshi la polisi. Tunapotoa tahadhari hii

tunafikiri hakuna hata mmoja kati yetu asiyeelewa ubaya wa kukaribisha wafanyabiashara au watu binafsi kuingiza mikono yao katika jeshi la polisi.

Kwa utendaji wa haki na uliotukuka kwa wananchi, chombo hiki kiachwe ili kijitegemee kiutendaji. Na wengi wetu tunajua vizuri kwamba kama kupokea misaada kwa vyombo vyetu vya ulinzi basi iwe baina ya nchi na nchi.

Mheshimiwa Sika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga fedha za kutosha kulingana na mazingira halisi yaliyopo. Suala la kuwa Serikali haina fedha, Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha aliionyesha Serikali ni wapi fedha zinapoweza kupatika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maboresho ya Jeshi la Polisi yanahitaji Utashi wa Kisiasa *(political will)*. Hilo litawezekana kama yalivyo mengine, ikiwa kila mmoja atatekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa wageni katika nchi yetu, Zanzibar ni Visiwa, navyo mara nyingine huingia watu wasio raia wa Tanzania na hasa kwa vile hakuna pasi za kusafiria baina ya Tanzania Bara na Visiwani na hili hutokea kwa sababu raia wa nchi za jirani huja moja kwa moja Zanzibar mara wanapoingia kupitia mipakani kwa njia halali au za haramu.

Ni hivi karibuni tu limetokea tokeo la kumtorosha mwanafunzi Mariam Farid wa darasa la tisa, akiwa na umri wa miaka 16, na inasemekana kwamba aliyemtorosha mwanafunzi huyo wa kike ni mwalimu wake mwenye asili ya kutoka Uganda anayeitwa Innocent Laizer Kayuna, ambaye alikuwa akifundisha katika skuli hiyo inayojulikana kwa jina la *Starnet* na hadi leo hii hajulikani alipo.

Naomba Mheshimiwa Waziri alitolee ufafanuzi wa kina suala hili hasa ukizingatia kwamba kabla ya hapo ni sula lililoripotiwa katika vituo vyote vya polisi Zanzibar hadi Makao Makuu. Wazazi wa mtoto huyu mdogo wamekuwa na majonzi makubwa kwa kutojua mtoto wao alipo. Vile vile itakuwa jambo la busara kwa Serikali yetu kuharakisha kutoa vitambulisho vya uraia wetu ili kudhibiti wahamiaji haramu kama hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa tulizonazo kwamba hata Mheshimiwa Waziri wa Elimu Zanzibar, amechukua hatua ya kuifunga skuli hiyo kwani hili ni tukio la pili baada ya lile la mwanzo la kuwachukua wanafunzi kadhaa na kuwapeleka katika fukwe za bahari zilizopo karibu na skuli hiyo na matokeo yake wanafunzi zaidi ya 10 walichukuliwa na maji na kufariki hapo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza kwa hatua hiyo Mheshimiwa Waziri wa Elimu wa Zanzibar, lakini tumelia na kunyamaza kwa wale waliofariki, je, kwa huyu

aliyetoroshwa ambaye hatujui yuko wapi na kama yuko hai au ni mateso ya aina gani anayopata huko aliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba jeshi la polisi kwa kushirikiana na *Interpol* pamoja na Balozi zetu zilizoko nje ya nchi na Wizara ya Mambo ya Ndani, kufuatilia na kujua hatma ya mtoto wa Kitanzania aliye mdogo kiumri yuko wapi, ili arejeshwe nyumbani na kuendelea na masomo. Vile vile ni vyema iwapo mhusika wa tukio hilo atapatikana ili apandishwe kizimbani na kuhukumiwa kwa mujibu wa sheria. Tunaomba mtoto Mariam arejeshwe nyumbani kwa wazazi wake haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa za kulevya bado kabisa halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Ni vyema Serikali kuwa makini sana na maadui hawa ambao wamo ndani ya jamii yetu. Kama ni vigogo basi lazima tutambue kuwa vigogo hawa hata kama ni vigogo vya mpingo ni lazima wakumbane na sheria na wasiwe juu ya sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuujenga uchumi wetu, basi huwezi kuwa na uchumi imara bila ya vijana ambao ndio nguvu kazi ya uzalishaji. Je, kuwa na ongezeko la wabugia unga kutaleta faraja gani katika jamii hata kama tutakuwa na uchumi imara? Ni vyema basi vijana wakapatiwa dawa na makazi maalumu ili kupata mafunzo ya kuachana na tabia hiyo, sambamba na kuchukuliwa hatua kali zaidi kwa waletaji na wasambazaji na wauzaji wa unga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa muda muafaka wa kuwasilisha maoni ya kiujumla ya Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Usalama wa Raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba kuwasilisha na naomba vile vile hotuba yangu ichukuliwe kama ilivyo kwenye *Hansard.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana viongozi waliotoa hotuba zao kufuatana na utaratibu wetu. Sasa walioomba mpaka sasa ni 30 kwa hiyo, ambao hawajachangia kabisa ni wane, waliochangia mara moja ni 14, ambao wamechangia zaidi ya mara mbili wako saba nadhani na hawa huku, sijui wamechangia mara ngapi.

Kwa hiyo, tutakuwa na wasemaji wachache sana na kwa kukadiria hapa unakuta asubuhi hii  tukiweza kupata wachangiaji sita ni bahati. Kwa sababu wengi hamjapata nafasi ya kuchangi kwa hiyo, itabidi mchana wachangie watu wawili tu. Kwa hiyo, sasa hivi namuita Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji.

**MHE. DR. HAJI MWITA HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi asubuhi hii kuwa wa mwanzo kuchangia katika Wizara hii ya Usalama wa Raia ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kwa niaba ya wananchi na wapiga kura wangu wa Jimbo la Muyuni, naomba nitoe rambirambi kwa vifo vya

Marehemu wote waliopita pamoja na cha mwisho kilichojitokeza asubuhi hii cha mama yetu mpendwa mama wa Mheshimiwa Ali Ameir kilichojitokeza huko Zanzibar. Mwenyezi Mungu, ampe wasaa na subira kwa yote hayo yaliyomtokea. Sisi tuko pamoja naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea na kuchangia naomba kwanza tu nitoe pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jinsi walivyowasilisha mada hii asubuhi hii ambayo kwa kweli imetupa maelekezo na miongozo sahihi kwa jinsi gani jeshi letu hili la polisi na Wizara nzima ya Usalama wa Raia ilivyopania katika kuhakikisha usalama wetu sote pamoja na mali zetu. Nawapongeza sana na natoa shukrani. Isingekuwa vema kuweza kukosoa hotuba na sitafanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningeomba kwa mambo mawili tu hayo kwa ruhusa yako ningeomba niyazungumze kwa sababu ikiwa kama nitakuwa na zaidi ya hayo pengine naweza nikaja nikakosea njia na sipendi, haja yangu muhimu ni kuhakikisha na kuthibitishia Bunge lako Tukufu kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia hotuba hii ya Wizara ya Usalama wa Raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo ningependa kulizungumzia asubuhi ya leo ni kwamba sote tunaelewa nini wajibu wa polisi katika nchi yetu. Polisi ya sasa hivi siyo polisi ya zamani. Nakumbuka wakati nilipokuwa shule nilipofika darasa la tatu kwenye miaka ya 1957 nilizuiliwa kwenda darasa la nne kwa sababu nilikuwa mfupi sana. Kwa bahati ya kuzaliwa njiti na wazee wanauliza mwanangu ukifika darasa la nane katika kimo hicho utakuja kufanya nini na wakati huo huo ilikuwa kazi zetu sisi kutoka shamba aidha, uwe polisi au uwe mwalimu.

Nilipofika darasa la saba bado nilikuwa sijakua wakati ule kabla ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na niliacha shule kwa sababu sikuwa na tamaa ya kwamba pengine nikimaliza darasa lile kwa ufupi niliokuwa nao nisingepata kazi. Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 nilirudi shule na nikaendelea na masomo mpaka hii leo na kufikia kupata *degree* ya kuwa daktari. Nashukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wazee wangu kwa kunikubalia kufikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimetoa historia hii, Jeshi la Polisi, wakati ule huwezi ukapata ajira kama hukufikia urefu fulani. Naamini walikuwa na maana yao. Lakini katika dunia ya leo, dunia ya sayansi na teknolojia ni jambo la kusikitisha la kuona kwamba kijana mwenye afya nzuri, ana akili timamu na ana uwezo. Lakini inapofika wakati wa kujiandikisha Jeshi la Polisi amepungua sentimeta moja ya urefu anaambiwa, wewe hufai kuwa polisi. Kwa kweli jambo hili linanisikitisha. Najua kazi ya kulinda usalama wa raia na mali haitegemei wafupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sisi wafupi akina Mwita wa Zanzibar siyo Mwita wa Musoma tuliokuwa tumezaliwa njiti hatuna urefu wa kutosha mtu anaambiwa kwamba wewe umepungua sentimeta moja na hufai polisi nadhani umefika wakati suala hili tulizingatie. Jeshi la Polisi la sasa linataka akili timamu, maarifa na uwezo bila shaka

na tunaamini wako wafupi kama mimi wapo kwenye Jeshi la Polisi na wamekuwa mahodari kweli katika utendaji wa kazi.

Kwa hiyo, ningeiomba sana Wizara hii pamoja na Kamishna wa Polisi ambaye naamini kwa jinsi alivyokuja na kasi na naamini kwamba wako askari wafupi ambao wanafanyakazi vizuri sana. Alizingatie suala hili walau tuone kwamba na sisi ambao hatuna vimo na sisi tuna akili ya kuweza kufanyakazi ya polisi. Sidhani kama kuchunga mbwa wa polisi kunahitaji mtu mrefu. Sidhani kama kuangalia *speed* ya gari ambalo linakuja mbio kama kunahitaji urefu, sidhani kama kukaa bandarini kumuona kwamba yule jambazi anaingia na silaha kuitambua silaha, kama kunahitaji watu warefu. Hata na sisi wafupi kazi hizo tunaziweza. Naiomba tena na tena Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa aweze kulifanyia maarifa suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati huo huo alipomaliza kuzungumza hapa Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alitoa malalamiko yake na kusema kwamba ajira ya Polisi inatakiwa uangalifu na itakuwa hatari sana ikiwa Jeshi la Polisi litaajiri watu ambao hawaaminiki. Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa na Jeshi la Polisi. Siyo kuangalia kwamba huyu anatoka wapi, ndiyo apewe kazi ya polisi. Unampa mtu kazi ya polisi baada ya kumwamini kwamba ataitekeleza vizuri kazi hiyo ya polisi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na utaratibu ambao unakwenda isipokuwa wa kuzingatia akili timamu, uwezo na elimu, siyo wa kuzingatia kwamba kwa sababu anatoka, Zanzibar kwa sababu anatoka Pemba kwa sababu anatoka Tanzania Bara ndiyo apate kazi ya polisi hapana. Vigezo ni vile vile lakini cha muhimu ni kuona uaminifu wa kazi hii kwa sababu kazi hii kwa kweli inataka uaminifu wa hali ya juu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa nilizungumzie kuhusu malalamiko ya askari ambao wanamaliza kazi. Kwa kweli naiomba sana Wizara hii pamoja na Kamishna wa Polisi na Jeshi la Polisi, kwa ujumla kuzingatia kuhusu askari ambao wanastaafu bado usumbufu wa kupata mafao yao ungalipo. Naamini jitihada zinapita za kufanya utaratibu kwa kadri inavyowezekana na nina hakika kwa nguvu ambazo zimechukuliwa au zinachukuliwa, suala hili baada ya muda si mrefu litapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo ili kuokoa muda nichukue nafasi hii, kulipongeza sana Jeshi la Polisi kwa juhudi zao wanazochukua za kutulinda kwa usalama wetu pamoja na mali zetu lakini na kuiomba Wizara na Serikali kwa ujumla ihakikishe kwamba inawapa fedha za kutosha polisi ili kufanikisha kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo sihitaji kuchukua muda naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, kwa kutupa dakika tano nadhani wengine wakifanya hivyo wengi watatosheleza. *(Makofi)*

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa na mimi fursa ili nishirikiane na Wabunge wenzangu katika kuichangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia. *(Makofi)*

Mimi naomba nianze kwa pongezi, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia na Naibu wake kwa ziara waliyoifanya Pemba. Walifanya ziara, wakaawarifu viongozi wote wanaohusika wakiwemo Wabunge na wameshirikiana nao kikamilifu. *(Makofi)*

Baada ya hapo nimpongeze pia Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kupitia kwa Inspekta Jenerali wa Polisi, naomba apokee pongezi hizi kwa sababu kwa sisi ambao tunaangalia mwenendo wa askari pale kwetu ni kamanda huyu ambaye ameleta utulivu mkubwa katika historia ya Makamanda wengi waliowahi kuja pale. Hata hiki kitengo cha polisi jamii amekisimamia vizuri na nafikiri Mkoa wa Kaskazini Pemba kinafanyakazi vizuri kuliko sehemu nyingi za Tanzania Visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije katika askari polisi. Yamesemwa hapa katika hotuba ya Kamati na katika hotuba ya Upinzani kuwa askari polisi wanafanyakazi kubwa na sote tunajua. Lakini nini wanacholalamika hii ndiyo *point* ya msingi. Askari huwa wanaahidiwa na viongozi wao na viongozi wao ninaokusudia ni kwa Waziri au wakubwa wao. Kwa mfano, askari hawa waliahidiwa posho ya matibabu ya shilingi 200,000 kuwa watapewa kwa mwaka shilingi lakini 200,000, hawajapata hizi fedha.

Sasa wanalalamika juu ya fedha hizi hii ndiyo hoja ya msingi. Ukisema utawapa maana yake uwape. Kama hukuwapa ni matatizo makubwa. Kwa sababu hizi posho ndogo ndogo ndiyo ambazo wao zinawasaidia kuweza kuishi. Hebu tujalie sisi Wabunge, kama ingekuwa tunakuja Dodoma tunakaa tunalipwa mshahara tu hatupewi angalau posho ya kujikimu hivi kweli ile *package* ya mshahara ingetuwezesha sisi kuishi hapa? Sasa na wao mitaani hawawezi kuishi kwa mshahara wao. Lakini hizi haki zao ndogo ndogo wapewe ili ziliwasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya mishahara, nasikia wameongezewa mishahara, lakini utafiti nilioufanya umegundua kuwa askari wa chini wameongezewa shilingi 6,300 ni nyongeza. Lakini kwangu mimi ni nyongeza ndogo sana. Sasa vitu kama hivi wakilalamika ni vizuri tuwasaidie kwa sababu wao ndiyo ambao wanatoa maisha yao kwa ajili ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika suala zima la hizo fedha zenyewe Mikoa ya Tanzania ipo 26 na Makamanda wa Polisi vile vile wapo 26. Lakini sidhani kama kuna *vote 26* ambazo zinatumika katika kuangalia maslahi na malipo ya askari polisi. Kama hilo halipo basi ni vizuri hizi kasma nyinginezo zinazopelekwa hasa kule Zanzibar ziende kwa Mikoa kwa sababu unapoweka Makao Makuu ya jambo lolote lile lina matumizi makubwa. Wanaweza wakatumia baadaye ukastukia Mkoa wa Kaskazini au Kusini, fungu lao limepungua na wataambiwa limetumika Makao Makuu hivi unasemaje ukiambiwa limetumika Makao Makuu? Sasa jambo hilo naomba liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye uhamisho, askari wanalalamika hasa waliopo Visiwani kuwa hawapati uhamisho wa kwenda sehemu nyingine za Tanzania. Sasa na hii ni hoja ya msingi kwa sababu hiki chombo katika maumbile yake ni chombo cha Muungano. Sasa unapomweka askari katika Mkoa mmoja kwa muda wa miaka 26 anakaa pale, kwangu mimi *I think that is not fair*. Ni vizuri kwa sababu chombo hiki ni cha Tanzania nzima japokuwa Wizara ina malalamiko haina fedha za uhamisho, mpeleke kwanza masuala ya fedha utampa baadaye lakini ile haki yake ya kumhamisha ulishampa. Lile lalamiko la msingi utakuwa umeliondoa ulishamhamisha. *Then* utamwambia fedha zako za uhamisho zitafuata baadaye. Wala usimkomoe mhamishe kwa mujibu wa taratibu maana yake tukisema hivi baadaye inaweza kuwa labda kumkomoa mtu hapana, maana yake ni kuwa ifanywe hii *fair transfer* ambayo kila mfanyakazi atalizika nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda sasa niendelee na suala la nyumba za polisi limesemwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, pale Wete niliwahi kusimama katika Bunge la mwaka 1995/2000 nikasemea juu ya Nyumba za Polisi. Mimi nilidhani labda baada ya kusema vile hatua ya kufaa ilichukuliwa. Leo ninapozungumza hapa kuna askari tayari wamehamishwa katika nyumba za polisi. Mie sidhani kama wamehamishwa kwa ajili ya kuwa nyumba zijengwe wamehamishwa labda zisije zikawaangukia waende wakatafute mahali pa kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi hili wazo tuliloambiwa hapa la kuwa zitajengwa nyumba na kila nyumba ina uwezo wa kuchukua familia 120 nafikiri tuangalie sana katika sehemu ya nyumba za polisi wa Wete. Polisi wa Wete, Micheweni, Konde na polisi wa Kengeja wanalalamika kuhusu nyumba. Nyumba kwa mujibu wa taratibu nilizosikia hapa zitakuwa tano zitakazojengwa Zanzibar kwa vile kazi mnayo. Lakini mimi ningeshauri mbali na kujenga hizo nyumba mpya basi mngefikiria namna ya kurekebisha angalau zile zilizopo zikaweza kuwa-*served* hawa watu. Kwa sababu kwangu mimi siyo busara hata kidogo askari kukaa uraiani kwa sababu wale wana miiko yao na ni lazima iangalie hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije sasa katika suala zima la Jeshi la Polisi la mapambano dhidi ya ujambazi, hapa niseme kuwa hili ni suala mtambuka, si la Wizara ya Usalama wa Raia, hili ni suala la Wizara ya Fedha, ni suala la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuja hapa tunaomba tujengewe barabara nzuri, tujengewe madaraja mazuri, tujengewe miundombinu mbalimbali, msingi wa matumizi ya mambo hayo ni kuwapo na utulivu na amani katika nchi. Kama utulivu na amani havipo wala hiyo nyumba nzuri hutakaa, wala hiyo barabara nzuri hutaipita na gari yako. Kwa sababu hutoki ndani ukaiendesha ile gari. *(Makofi)*

Mimi siku za nyuma nilikuwa nikidhani kuwa masuala ya silaha nzito, masuala ya vita yanalihusu Jeshi la Wananchi wa Tanzania, lakini uzoefu nilioupata katika kipindi hiki kidogo baada kadhia nzima ya majambazi imenidhihirishia kuwa askari polisi sasa na wao wanakabiliana na hali kama ambayo wanakabiliana nayo Jeshi la Ulinzi. Sasa kukabiliana nao ni suala moja lakini kuandaliwa kukabiliana nalo janga kama hilo ni suala la pili. Hapo ningependa nitoe wito kwa Serikali nzima waangalie namna ya

kuwawezesha Wizara ya Usalama wa Raia katika kuwafundisha vijana suala zima la kukabiliana na ujambazi wa kisasa walioona kwenye televisheni katika ile nyumba iliyovamiwa juzi kule Arusha katika eneo la Njiro Kontena, waliona aina ya silaha iliyokuwepo pale wala siyo rungu lile wanalotumia *FFU*, nafikiri *FFU* wangekwenda na rungu wangekimbia kwa sababu mimi nimeona pana silaha nzito ambazo zilikuwa zinatumiwa.

Sasa ina maana tunahitaji kufanya mabadiliko katika jeshi zima la polisi. Kama tunawataka vijana wetu waende kwenye *operation* warudi na roho. Kama tunawataka vijana wetu waende kwenye *operation* halafu upeleke karandinga tukawapakie tukawazike sawa. Lakini kama tunataka warudi na roho, lazima tuwawezeshe kweli kweli, tuwawezeshe kwa mbinu, tuwawezeshe kwa silaha na tuwawezeshe kwa mafao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mmoja aliniambia zamani mimi sijui kama alikuwa mkweli alisema *pilot* wa ndege vile akirusha ndege analipwa fedha zake kwa sababu anaweza akafa. Pengine sivyo hivyo lakini maana yake ni kuwa watu wenye kufanyakazi za *risk* kwa maana ya kuhatarisha maisha wanapaswa waangaliwe vizuri ili na wao wazifanye kwa moyo mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujambazi naomba niishie hapo. Limesemwa suala hapo na naomba hili suala tuelewane vizuri kabisa, mimi nakubaliana na hoja kuwa katika Jeshi la Polisi au Jeshi lolote aajiriwe raia anayeaminiwa. Mimi naunga mkono hoja hiyo, kwa sababu kama humuamini utamwajiri vipi katika chombo chenyewe kama hiki. Lakini kuna malalamiko pengine si ya kweli, katika maafisa 18 wa vyeo vya juu wa Jeshi la Polisi Zanzibar hakuna Afisa anayetoka Kisiwa cha Pemba. Sasa pengine hiyo taarifa siyo ya kweli na inaonekana mara nyingine tunaposema mambo hapo labda watu wanadhani tunaokota lakini siyo tunafanya utafiti wa vitu kama hivyo. Kwa sababu hatuwezi kuja hapa tukaporoja tu.

Sasa ningeliomba basi Jeshi la Polisi, ningeiomba Wizara ya Usalama wa Raia, iangalie hali hii kama ni ya kweli irekebishwe. Ni suala la kurekebisha tu kwa sababu na hao askari wapo wa Unguja na Pemba, askari wanaopata mafunzo pamoja kwa sababu hakuna wengine wanaokwenda kufundisha katika vyuo vingine ni vyuo hivyo hivyo vinavyofundishwa ni kozi hizo hizo zinatoka. Sasa kwa nini unapopandisha madaraka huangalii? Hii inaleta tafsiri ya kuwa wakubwa wa polisi kwa sababu wanatoka baadhi ya sehemu fulani wanahisi kuvuta watu. Sasa katika Tanzania ya leo ya mwaka 2007 kusikia Watanzania wanalalamikia masuala kama hayo ni kitu cha kusikitisha kwa sababu mimi naamini mahali popote kwa mujibu wa Mtanzania, kwa mujibu wa nchi yetu, kwa mujibu wa historia ya nchi yetu, haturuhusu ubaguzi. Sasa ikiwa huruhusu ubaguzi Kikatiba, huruhusu ubaguzi kimaneno, lakini kivitendo unauruhusu, inasitikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana jambo hili liangaliwe mara moja na ikiwa kuna uwezo wa kulirekebisha lilirekebishwe mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa askari na mafao yao. Mimi nilitaka nilalamikie askari wanaofariki. Hivi kwa nini askari anafariki dunia mpaka na yule mrithi wake afariki ndiyo apewe fedha? Maana yake nashindwa kufahamu mimi inasubiriwa na yule mrithi naye afariki apatikane mrithi mwingine, hapa ni vizuri kama mtu amefariki dunia harakati za kumpa mafao ziandaliwe ili masuala ya kunung'unika kwa wale warithi na hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kuna askari mmoja *PC* Hamis Ali namba yake ya kazi ni D.2678 naikariri kidogo kidogo. Jina lake ni *PC* Hamis Ali namba yake ya kazi ni D. 2678, huyu kijana ni kijana wa Mjimbini, Pemba ni kijana wa aliyekuwa Mkoa wa Kusini Pemba, Jimbo la Mtambile, alifukuzwa kazi katika mazingira ya kutatanisha sana. Wapo askari wengi wamefukuzwa kazi wala hatujasema, lakini mazingira ya huyu ni ya kutatanisha sana. Namuomba Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia ashirikiane na viongozi wa juu wa jeshi la Polisi watazame hili suala la vijana wetu, kama kweli ni suala la kutatanisha, kama kweli ameonewa basi sheria na haki zitumike kwa sababu unamuonaje mtu? Leo ukimuonea huyu kwa sababu wewe una madaraka, keshokutwa utayakosa, Mwenyezi Mungu anaweza akaandaa namna na wewe ukaonewa, utafurahi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dini ya Kiislamu inakuambia tenda haki kwa watu wote. Mwenyezi Mungu ndiyo anavyosema tuwatendee watu haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho napenda niwaambie Waheshimiwa Mawaziri, mkija hapa mnaweza mkatujibu maneno mazuri sana, lakini maneno huwezi ukayachemsha ukayala, vijana wapelekeeni fedha mapema waweze kuafu nafasi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. ENG. LAUS OMAR MHINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nataka nianze mchango wangu kwa kutoa rambirambi kwa ndugu wote waliopata misiba ya kutokwa na ndugu zao, jamaa, rafiki na sisi Wabunge pia tukiwa kati ya hao. Mungu aziweke roho za Marehemu wote mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nianze mchango wangu kwanza kwa kuipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia jinsi ilivyotengenezwa na alivyoiwasilisha, kwa kweli nadhani imempendezesha kila msikilizaji aliyeisikiliza. Pongezi hizo zisimwendee Waziri peke yake, pia ningependa zimwendee na Naibu Waziri pamoja na Wizara nzima kwa ujumla kwa maandalizi mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu kwanza, nitauanzia kwa kulipongeza jeshi zima la polisi. Kwa kweli sote tu mashahidi kama tukitaka tuongee ukweli kazi inayofanywa na askari wetu wa Jeshi la Polisi ni nzuri. Hii inadhihirisha hata ukiangalia katika kitabu kidogo tulicholetewa hiki ukiangalia makosa ya jinai mwaka 2004 yalikuwa karibuni 80,000 leo mwaka 2006 yamefikia kwenye 50,000 punguzo la karibu ya makosa

30,000. Hii kwa kweli inastahili hawa wenzetu kuwapongeza kwa kazi nzuri. Hizi ni takwimu ambazo wala hazina utata, tumeletewa na nina imani ndiyo hali halisi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengi tuliona wimbi la ujambazi lilivyoanza kutokomea, sisema kama limetokomea moja kwa moja lakini jinsi lilivyopungua, tumeona wiki iliyopita tu ni jinsi gani askari wetu walivyojitolea mhanga kupambana na majambazi ambao walikuwa na silaha, mimi naweza nikasema ni za jeshi siyo za kiaskari lakini ushupavu wa askari wetu mpaka wamefanikiwa kuwakamata wahalifu wale. Kwa kweli askari wetu wanastahili hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhalifu huo usipowakamata watu tu silaha zinazokamatwa mpaka dakika hii ni silaha ambazo kwa kweli zingeweza zikateketeza raia wengi wasio na hatia Tanzania. Lakini kwa ujasiri wa jeshi letu la polisi, kwa ujasiri wa askari wetu wa upelelezi wanapopeleza taarifa na taarifa hizo kufanyiwa kazi kuwapeleka vijana wetu kwenda kupambana kwa kweli hili linastahili na pongezi za hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi hizi mimi pia ningependa nizifikishe kwa askari hawa, ningependa nizifikishe kwa askari wetu wa Usalama Barabarani, kwa kweli sijui lakini mimi labda niseme sitasita kusema kwamba Kamanda Kombe anastahili sifa. Kwa hali niliyoiona siku zilizopita Dar es Salaam kutoka Mwananyamala mimi mwenyewe kwa kuendesha gari kuingia mjini ilikuwa inanichukua si chini ya saa moja. Leo hii kutoka Mwananyamala kwenda mjini inanichukua si zaidi ya dakika 20. Kwa kweli jeshi hili la usalama barabarani linastahili pongezi ya hali juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa hizi kwa kweli zinatokana na nini? Sifa hizi mimi nataka niwapongeze sana Wakuu wa Jeshi la Polisi kwa kuanzisha ushirikiano mzuri kati ya jeshi la polisi na raia. Mimi nadhani ni kutokana na juhudi za jeshi la polisi lilivyojihusisha na raia kushirikiana na ndiyo maana limefanikisha kuweza hata kuwaibua majambazi waliokuwa wamejificha katika nyumba mbalimbali, ushirikiano huu naliomba jeshi la polisi uendelee na ukue zaidi ya hapa ulivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine kwa kweli ningependa niuelekeze kwenye huduma hii ya polisi isiendelee au isiboreshwe mijini tu. Kwa kweli vijijini nako tunahitaji huduma hii ya polisi. Mimi mwenyewe nikiwa natokea katika Jimbo la Korogwe Vijijini inasikitisha kuona hata Makao Makuu ya baadhi ya Tarafa hayana kituo japokuwa kidogo cha polisi. *(Makofi)*

Naliomba Jeshi la Polisi kwa kweli lijaribu kupeleka huduma hii vijijini ikiwezekana katika kila Kata kuwe na kituo kidogo cha polisi. Inasikitisha kama nilivyosema hapo awali, inasikitisha kwamba Makao Makuu ya Tarafa yangu ya Bungu hayana kituo cha polisi. Makao Makuu ya Tarafa yangu ya Magoma hayana kituo cha polisi. Naliomba Jeshi la Polisi iliangalie kwa kweli katika hali ya huruma hili, ili huduma hii isiende mijini tu. Kwanza tuzingatie kwamba majambazi haya tunayoyazungumzia wengi wao pia wanaishia vijijini, wanafanya uhalifu mjini, wanajifichia vijijini au wanatokea vijijini kwenda kufanya uhalifu mijini. Kwa hiyo,

tutakapokuwa na jeshi la polisi mpaka ngazi ya vijijini kwa kweli kidogo hii hali ya ujambazi au hali ya uhalifu tutakuwa tumeipunguza kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, palipo na mazuri mabaya pia hayakosekani. Ndugu zangu wa polisi mabaya ambayo kidogo mimi nimeyaona ambayo hatuna budi kwa kweli tuyaangalie kwa undani ni kero ambazo zinasababishwa na askari. Mimi naweza kusema labda ni askari wachache ambao siyo waaminifu. Kikubwa ambacho kinakera kwa wenye magari hivi sasa ni hili tatizo la kusimamishwa kila baada ya hatua kumi. Ninaposema hatua kumi sina maana kweli hatua kumi, lakini baada takribani kilomita kumi. Mimi mwenyewe nimeona hilo kwa macho yangu. Nimetoka Korogwe kwenda Tanga huu ni mwendo wa kilomita kama mia moja tu nimesimamishwa njiani siyo chini ya mara kumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na unaposimamishwa njiani huku kwa kweli huulizwi lolote la maana. Je, mzee hujambo? Je, unaelekea wapi? Sasa wewe unaniona naelekea Tanga unaniuliza naelekea wapi tena? Au sana sana labda mtu atakuambia unaweza kumpa *lift* jamaa yangu anaelekea Tanga yaani umenisimamisha kwa sababu ya *lift* tu. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, ningeomba wakuu wangu wa polisi waliangalie hili kwa makini. Pia juu ya kusifu sana wenzetu wa *Traffic* ningewaomba wakuu wa Jeshi la Polisi pia kuna baadhi ya wachache, wachache nasema kwa kweli, ni wachache, wana mienendo ambayo siyo mizuri. Nimelishuhudia mwenyewe pia kwa sababu siyo kuwa nasafiri kwa gari yangu binafsi tu bali nimeona mimi mwenyewe kwa kushuhudia, *traffic* anasimamisha basi, kondakta hamuulizi au haelezi kosa la kondakta bali anamchukua nyuma ya basi sasa huku nyuma ya basi wanazungumza nini? Kama ni kosa si basi amweleze pale pale. Hili ningeomba wakuu wangu wa polisi mliangalie mlitupie macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha mwisho sana ningependa kwa kweli pia kujaribu kuwatetea ndugu zangu wa polisi. Ndugu zangu wa polisi katika mazingira wanayofanya kazi ni magumu sana, sote tunafahamu haya. Tungeomba au naomba na napendekeza kwa kweli wapatiwe vitendea kazi, japo hata pikipiki kwa wale askari wa katika vituo vidogo. Wengine hawana hata huduma ya pikipiki hata za mawasiliano pia hawana. Ili tuliboreshe jeshi letu kwa kweli ningeomba huduma hizi zijaribu kuboreshwa na pia ifikie mahali pia tuwaonee huruma nao ni wazazi, sasa baadhi ya polisi kwa kweli ukiwaona ni wazazi wanakaa kwenye nyumba za vibanda vya *full suit* za mikonge, natoa mfano wa Arusha pale Kaloleni kwa kweli inatia huruma.

Ninaelewa wazi kabisa kwamba Wizara ya Usalama wa Raia inajitahidi na imekwisha ahidi na inajenga nyumba karibuni magorofa 30 Dar es Salaam na magorofa 30 mengine Visiwa vya Zanzibar. Lakini jitihada na juhudi bado zinahitajika, tuwasaidie hawa ndugu zetu wa polisi wanaofanya kazi katika mazingira magumu na wanaojitolea nafasi zao kwa ajili yetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kengele ya pili inipigie. Naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FATMA OTHMAN ALI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuweza kusimama leo hii kwenye Bunge lako hili Tukufu. Kwa niaba ya wanawake wa mkoa wa Mjini Magharibi, tunatoa rambirambi zetu kwa ndugu jamaa wa Marehemu, mtoto wetu, ndugu yetu, Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Amina Chifupa. Mungu ailaze roho yake pema peponi, *Amin.*

Nianze kwa kuchangia Wizara hii ya Usalama wa Raia kwanza kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa *IGP* pamoja na Makamanda wake wa mikoa yote 26 kwa kazi kubwa waliokuwa nayo, wanayoendelea nayo kwa wimbi la ujambazi lililojitokeza kwenye Mikoa yote. Kwa kweli tunampongeza, tunawapongeza na maaskari wetu. Lakini pongezi zaidi nampongeza Ndugu yangu *ACP* Mussa Ali wa Zanzibar kwa jitihada zake alizozifanya yeye pamoja na Makamanda wenziwe na maaskari wetu wa Zanzibar kwa ushirikiano wao waliokuwanao wa kulinda haki, usalama wa raia na mali za raia. Kwa kweli askari wa Zanzibar wamefanya jitihada kubwa sana kupambana na wimbi kubwa la ujambazi lililotuingilia katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini basi askari wetu hawa wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, hawana vitendea kazi, vitendea kazi hawana. Ukija usalama wa barabarani yaani *Traffic* wana upungufu mkubwa sana wa magari, pikipiki hata zile *radio call* vijana wetu hawana. Gari zao asubuhi ziko gereji, jioni zinafanya kazi au jioni ziko gereji asubuhi zinafanya kazi. Kwa kweli namwomba Waziri akitazame vizuri kikosi hiki cha *traffic* au hawa watu wa usalama barabarani kwa kuwapatia vifaa kama vile mapikipiki, gari na redio za mikononi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuje kwenye dawa za kulevya. Tunacho kikosi Zanzibar cha Kuzuia Dawa za Kulevya. Lakini utashangaa hiki kikosi ni kikubwa, kinapambana na dawa za kulevya lakini hawana gari angalau ile mbovu ile hawana. Wanapotaka kwenda kufanya kazi zao lazima uende Makao Makuu ya Polisi wakaombe gari ndiyo uende kwenye shughuli za kazi, kwa kweli hili ni tatizo, tena tatizo kubwa sana.

Ningemwomba na hili Mheshimiwa Waziri akitazame hiki kikosi cha Kuzuia Dawa za Kulevya awapatie angalau gari moja au pikipiki kwa ajili ya kufanikisha shughuli zao za kazi. Kama tunavyoelewa Zanzibar maduka ya dawa za kulevya hivi sasa yapo mengi. Kweli askari atembee kwa miguu kutoka Kituoni kwake mpaka anakokwenda kupambana na vijana hawa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri alitazame hili kwa moyo wa huruma kikosi hiki cha kuzuia dawa za kulevya cha Zanzibar wapatiwe magari. Suala lingine la nyumba, Mheshimiwa Waziri ametujibu hapa kama nyumba kwa Zanzibar tuna nyumba tano, tatu Unguja na mbili Pemba. Lakini nimweleze Mheshimiwa Waziri kuwa nyumba tatu kwa Zanzibar hazitoshi na hazitoshi kabisa. Askari wengi wa Zanzibar wanakaa uraiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri na hili nalo atutazame kwa moyo wa huruma, pale Zanzibar atupatie walau nyumba saba na kule

Pemba awapelekee tano ili walau askari wetu kidogo watakuwa na hali nzuri kwa sababu askari wanaoishi ndani ya Boma pale Ziwani, kwenye Kambi ya Ziwani wanaishi kwenye mazingira magumu kweli. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri katika hiyo mipango yao ya nyumba, basi Zanzibar atugawie nyumba 13, kwenye nyumba 7 atugawie pale Unguja na tano atupelekee Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la hapo hapo katika Kambi ya Ziwani. Ndani ya Kambi ya Ziwani, tuna hospitali. Hospitali hii tunasema ni kubwa kwa askari, kwa sababu inahudumia askari karibuni wote wa Zanzibar na raia wanaokaa karibu na hospitali hii. Lakini cha kusikitisha wafanyakazi mahodari, madaktari wazuri, lakini hawa ni madaktari wa kuandika vyeti tu. Mgawo wa dawa wanaopewa hospitali hii ni mdogo sana. Kwani ikifika saa tatu asubuhi pale hupati dawa. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri Bajeti ya mwaka unaokuja awatengee kifungu chao hiyo hospitali ya Zanzibar wawe na kifungu chao cha dawa. Kwa sababu inawahudumia hata askari wanaokuja Zanzibar kwenye mafunzo huwa wanahudumiwa na hospitali hii. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri mwakani unapokuja na Bajeti uihurumie hii hospitali ya Ziwani. *(Makofi)*

Suala lingine ni mafao ya askari wanaokufa. Tuna askari Zanzibar, kuna *Inspector* Saleh Said Juma, huyu alikuwa mfanyakazi kwenye *Bar* ya Polisi pale Ziwani, amekufa tangu mwaka 2003, kuna *PC WP* Zuena Hussein Haji, mwanamke huyo amefariki tangu mwaka 2003 mpaka leo hawajapata mafao yao. Hii inatusikitisha sana, yaani kutoka Dar es Salaam mpaka Zanzibar inafika miaka minne watu hawa wasipate kweli mafao yao? Naomba Mheshimiwa Mkuu wa Jeshi la Polisi, tumekusifu, hodari na kweli hodari, lakini na hili nalo la manufaa ya hawa watu au hawa askari, pia ulifuatilie ubovu uko wapi, kwa nini watu wanapokufa Zanzibar wanachelewa kupata mafao yao? Tatizo liko mahali gani? Ningeomba Mkuu wa Jeshi hebu lifanyie uchunguzi na hili tupate ufumbuzi. Si hilo tu hata askari wanaoacha kazi jamani askari wanaoacha kazi Zanzibar wana matatizo makubwa, wanatutilisha imani. Utamwona *Inspector* wa polisi ameshaacha kazi, leo anaburura madumu ya maji na baiskeli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukimwuliza anakuambia sijapata mafao yangu. Kweli anadhalilika askari yule wakati kweli yeye alikuwa mkuu wa kituo pahali fulani. Leo anahangaika na madumu ya maji nini kwa sababu hajapata mafao yake. Naomba na hili Mheshimiwa Waziri uliangalie kwa jicho la huruma. Uangalie askari hawa walau na wao wanapoacha kazi wawe wameshapata kile kitu chao wafanye mipango yao ambayo walikwishakuipanga.

Suala lingine tunazo *police post* lakini hizi *police post* tulizokuwa nazo hazina ukakamavu, hazina ukakamavu kwa ukosefu wa vitendea kazi, ukosefu wa askari. *Police post* moja iko tuseme Shaurimoyo, utakuta ina askari watatu. Kweli hali hii ya ujambazi iliyokuwepo sasa hivi nchini pote kwenye kituo kidogo cha polisi mnakwenda kuwapeleka askari watatu au askari wawili, anaumwa na tumbo anabaki mmoja! Nalo hili namwangushia Mkuu wa Jeshi la Polisi hasa Zanzibar alifikirie vizuri na atazame vituo vyake hivi vidogo vya polisi waweze kuwa na askari wa kutosheleza vile vile wapatiwe vitendea kazi. Jamani kweli jeshi la polisi lina ukosefu basi na wao wakaomba misaada kwa wafadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi nichangie Wizara ya Usalama wa Raia. Naanza kwa kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na nawapongeza Mheshimiwa Waziri, msaidizi wake na watendaji wote, kazi wanaoifanya tunaiona, lakini waongeze juhudi zaidi. Kwanza mimi nianze na usalama wa raia nchi nzima, bado kuna maeneo ambayo yana wasiwasi sana. Juzi tukio la Arusha linatokea mimi nilikuwa Arusha, kwa kweli inatisha. Kwa hiyo, tunaomba waongeze nguvu, waongeze nyenzo maeneo yote na hata hayo ambayo hatukutegemea kwa mfano eneo lililotokea kwa watalii hilo linatupunguzia sifa ya nchi yetu. Nchi yetu ina sifa kubwa sana na hawa majambazi wanaokamatwa wanatoka nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo nchi jirani tuna mahusiano mazuri, lakini ni washindani wetu kibiashara. Sasa kama wataingilia hata hoteli za kitalii kwa kweli itakuwa matatizo makubwa. Tunaomba jitihada ziongezwe ili usalama uwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia Mkoa wetu wa Singida, Mkoa wa Singida kule nyuma ulikuwa hauna matatizo sana. Kukaja kipindi ukatulia, tukasahau kabisa mambo ya ujambazi. Lakini sasa hivi yameanza kujitokeza tena. Juzi juzi hapa raia mwema ameuawa bila sababu, kwa hiyo, tunaomba Mkuu wa Polisi nchini iangalie Singida kwa jicho la huruma. Huo mkoa uko katikati, wageni wengi wanakuja pale na ni eneo dogo sana. Kama kule nyuma mliweza kudhibiti na mkajua wahalifu wanaoingia na kutoka hivi kwa sasa kuna nini? Tunaomba msaada wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi upande wa jimbo langu, nimeahidiwa nikianza na Kituo cha Polisi Nduguti, hapo ndiyo katikati mwa Jimbo na ndiyo hapo tunategemea kwamba pakitokea tatizo kona yoyote ya jimbo polisi watakimbia kutoka pale waende mara moja. Lakini hawana Ofisi na wananchi wako tayari kujenga Ofisi ya kisasa. Hawana magari, kwa hiyo, mimi naomba hiyo ahadi ya miaka yote ikamilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda kituo cha Polisi Iguguno, umeme unapita chini ya mita 15 huu ni mwaka wa tano naahidiwa. Umeme utaingizwa ndani ya Kituo cha Polisi. Kwa kweli haipendezi na inawasikitisha sana wananchi wa Iguguno, kuna umeme unapita wao wakienda Polisi wanakuta wamewasha vibatali. Mimi naomba sana hiyo liangaliwe na vile vile kituo cha polisi cha Ibaga hiki kiko mpakani, askari wako pale, ofisi haitamaniki, wanakaa kwenye Ofisi ya Katibu Tarafa, halafu la kusikitisha zaidi hawana silaha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pametokea ujambazi mara nyingi wa wizi wa mifugo nawapitia tuende, wanakwenda hawana silaha. Sasa mimi nawaambia mtakwenda kufanya nini? Niwapongeze sana askari wetu wa Nkili na Wahdazabe walioko kwenye bonde la Ziwa Eyasi wanatusaidia sana. Sasa mimi naomba hiki kituo cha polisi

kidumishwe na kiongezewe askari kwa sababu ni eneo kubwa wanalolimiliki liweze kusaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tukio ambalo lilitokea Singida hivi karibu umepita muda kidogo, lakini linatisha na linatutia aibu. Kuna vijana wa polisi walihamishiwa Singida muda si mrefu, wakapangiwa Kituo cha Sepuka, katika pitapita wakakamata ng'ombe wa wizi na wakapeleka Makao Makuu ya Wilaya, Singida Mjini pale. Ng'ombe wale walikaa pale wakajitokeza wajanja, wakasema ng'ombe ni wao, *OC CID* akaruhusu wale ng'ombe wapelekwe kwa wale watu. Kumbe wale walikuwa siyo wenye ng'ombe. Wakapewa ng'ombe, walipokuja wenyewe halali, wenye ng'ombe halali badala ya kusaidiwa wakawekwa ndani na mpaka leo wanasota na walikuwa wageni, mmoja alihamishwa kutoka Zanzibar kwenda pale. *OC CID* aliyekuwa anatoa *order* adhabu aliyopata ni ya kuhamishwa na akapandishwa na cheo. Sasa ni *OCD*. *(Makofi)*

Mimi ningemwomba Mkuu wa Polisi aliangalie hili apitie upya *at least* wale askari wasaidiwe, wasiendelee kusota. Tukio la kusikitisha zaidi lilitokea tarehe 26 Juni, 2007 Kata ya Mwangeza, Kijiji cha Mwangeza, kuna Bwana mmoja anaitwa Malugu Mkwabi, alimtorosha mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Chemchem, akaenda akakaa naye zaidi ya miezi minne kule yaani akaoa. Lakini bahati nzuri yule mtu akakamatwa akapelekwa Kituo cha Polisi Matongo na walipompekua acha uhalifu alioufanya wa kumtorosha na kumwoa mwanafunzi wa shule alikamatwa na ngozi moja ya chui na ngozi moja ya simba na risasi tatu za *SMG,* kwenda Kituo cha Matongo akaongea na Mkuu wa Polisi pale akamwachia.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu ambaye alifanya uhalifu wa kumtorosha mwanafunzi, halafu kakutwa na nyara za Serikali, kakutwa na risasi ambayo siyo halali, akaachiwa. Mheshimiwa Diwani na viongozi wakamwambia aende kumwona *DC.* Alipokwenda kumwona *DC, DC* akamwagiza aende kwa *OCD.* Huyu ndugu anaitwa Charles Saenda alipofika kwa *OCD* anaeleza habari zake akawekwa ndani yeye baba wa yule binti ambaye aliachishwa shule na kutoroshwa. Mimi ningeomba hilo hebu lichukuliwe kuwa jambo la haraka sana na lishughulikiwe. Matatizo kama haya ndiyo yanaleta dosari kwa chombo chetu cha usalama wa raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi ningeomba sana muangalie haya mambo na wale wote waliohusika wachukuliwe hatua na mimi ningependa jioni wakati mnamaliza tuambiwe mmefikia wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la mwisho mimi ningesema kwamba sisi tunawaheshimu sana askari wetu wanafanya kazi nzuri. Lakini pale mnapowaacha wanakaa muda mrefu pale mnaacha *traffic* miaka nenda rudi, ukitoka hapa ukienda Dar es Salaam ukitoka hapa ukienda Singida ukitoka hapa ukienda Arusha barabarani unawakuta wale wale kila siku, kwa kweli inaanza kutukatisha tamaa. *(Makofi)*

Mimi ningeshauri hawa wahamishwe na ikiwezekana wabadilishwe kazi. Walishasahau kazi ya u-*traffi*c na ndiyo maana ajali zinatokea. Kwa sababu gari inakuja basi inasimama, dakika tano wamezunguka nyuma ya gari, yule anaachiwa anakwenda.

Kwa hiyo, mimi ninaomba sana na kufanya majaribio Mheshimiwa Waziri hebu Mkuu wa Polisi nchini hata kama yeye atakwenda na helkopta au na ndege watu wake watakaopita kwenda Dar es Salaam kwenye kila kituo atakaowakuta *Police traffic* wawaulize wamekaa muda gani kwenye kituo hicho? Hiyo itatusaidia kupunguza ajali na vile vile yale mambo ya kuweka milango ya dharura hebu isiwe kauli tu. Hebu simamieni hilo litekelezwe. Ajali iliyotokea Singida hivi karibuni ya *Mohamed Trans* sisi tulifika wakati inatokea. Kwa kweli inatisha na kungekuwa na mlango wa dharura wananchi wengi wangepona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, wasaidizi wenu wote lijengeeni Taifa hili heshima kwa kuangalia uhalifu unaotokea, ukomeshwe na wale wanaotoka nchi jirani, imarisheni vituo vyenu vya polisi vilivyoko mpakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Usalama na Raia, kabla sijachangia hotuba hii niungane na Wabunge wenzangu wote wale waliotoa mkono wa msiba kwa wote waliotangulia mbele ya haki na mimi Wabunge hao niko pamoja nao na nawatakia malazi mema roho zao wote waliotangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo sasa naanza kwa kutaka kuchangia hotuba hii lakini kwanza nimsifu Waziri wa Usalama wa Raia kwa hotuba yake ilivyo nzuri na safi lakini vile vile niwasifu viongozi wote wa Jeshi la Polisi kwa ukakamavu wao kwa muda mfupi walivyodhibiti ujambazi uliokuwa unakera sana hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema si wakati wa kupongezana, lakini mimi nasema kwamba ni wakati wa kupongezana, kwa sababu mtu yeyote yule anayefanya jambo jema, japo liko mikononi mwake kulifanya lazima umpongeze, kwa sababu wapo wengine wanajijua wazi kwamba wafanye mambo na hawayafanyi. Kwa hivyo, wale wanaofanya vizuri ni wajibu wao kuwapongeza. Lakini ile hoja aliyosema kwamba Usalama wa Raia haki yao au kazi yao kulinda mali ya wananchi, nasema polisi wanafanya hivyo na ndiyo maana wakathubutu kuwashinda majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa sina haja ya kulisema jambo hili kwanza si wajibu wangu kwa hapa kusema kwa kutetemeka lakini kutokana na hali yangu si nzuri na nimekwenda kupima *pressure* kidogo imekuja juu kwa hivyo msinishangae.

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo hapa kwa dhamira ya kuzungumza na kuwaweka wananchi wetu mahali pazuri. Lakini kama sisi Wabunge tukianza kukaa hapa na kuyagawa au kuzigawa nchi zetu kwenye matabaka, tunawaweka mahali pabaya wananchi wetu ambao wanatufuata sisi na unaweka umajimbo ndani ya Tanzania ambalo jambo hilo halipo, ninalolisema mimi kama walivyodai, Kambi ya Upinzani kwamba upande wa polisi hakuna wazaliwa kutoka Pemba hilo mimi nalikataa, yuko ndugu yetu huyu ambaye anaitwa Shaibu Mohamed Ibrahimu, yeye ni *RPC* ambaye yuko Shinyanga.

*RPC,* lakini vile vile kituo cha polisi cha Makunduchi ambako ndiko nilikozaliwa mimi mkuu wa kituo hicho alikuwa anatoka huko huko Pemba na wengi wengineo ambao wapo. Kwa hivyo, tukikaa hapa lazima tuzungumze ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa hatuzungumzi Upemba, hatuzungumzi Umakunduchi, hatuzungumzi Ukaskazini wala Umwanza na ikiwa tunazungumza hivyo hata huyu *IGP* tutasema atoke Zanzibar na tutafika pabaya. Hapa tunazungumzia Tanzania, tunazungumzia Muungano na chombo cha polisi, usalama wa raia ni Wizara ya Muungano, tuzungumzie Muungano na vile vile hapa tuzungumzie Zanzibar, hatuzungumzii Unguja na Pemba, ime-*frame* kitu Zanzibar kwa hivyo tunazungumzia Zanzibar, tunazungumzia Muungano. Tukija Zanzibar tunazungumzia Serikali ya Zanzibar ya Mapinduzi, tukija upande wa Muungano, tunazungumzia Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi huwezi kupewa cheo wakati hujafika kupewa cheo hicho, wanaofanya vizuri ndio watakaopewa cheo, lakini ambao hawafanyi vizuri hawatopewa cheo kama *RPC* wala nini lakini wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja hotuba ya ndugu yetu Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 33, maboresho ya polisi. Sasa karibu mwaka mzima kuingia mwaka wa pili bado tunazungumzia kwamba tunapeleka Tume, maboresho ya polisi, tunaambiwa nini Wabunge, kutokana na kazi nzuri wanayofanya ndugu zetu wa polisi wa usalama wa raia, nilidhani leo tunaambiwa kwamba polisi hasa wafanyakazi wa chini tumewatendea hili, ili tuondoke hapa kuanzia askari wetu pamoja na sisi tuwe tumefarijika. Kwa hivyo, bado wakati upo ndugu Waziri naomba Tume hiyo ifanye kazi haraka, ndugu zetu ambao wanafanya kazi nzuri, wazidi kufanya kazi nzuri ya polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja upande wa pensheni, wapo askari polisi hapa ambao wamestaafu tarehe 30 Juni, 2007, lakini wengine wamestaafu tarehe 1 Julai, 2007 nasikia hao waliostaafu tarehe 30 Juni, 2007 wanalipwa pensheni kwa kipindi cha miezi sita na hawa waliostaafu tarehe 1 Julai, 2007 wanalipwa pensheni kwa kipindi cha miezi mitatu, *Oysterbay Sugar House,* ndiko wanachukua pensheni zao. Sasa hapa kama kweli ni hivyo naomba tufafanuliwe kwa nini ni hivyo na kwa nini wote wasilipwe kwa miezi mitatu, jambo ambalo kumweka mfanyakazi yeyote ambaye analipwa kwa kipindi cha miezi sita, hatuwatendei haki. Tunaomba wastaafu wote badala ya miezi mitatu, basi sasa walipwe miezi sita.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine *traffic* Zanzibar. Zanzibar sasa *traffic* imekuwa nikesme *traffic* kiutendaji ni vyombo vyote vinavyotembea barabarani hata waenda kwa miguu nao ni *traffic*. Lakini wale wakuwa *traffic* wenye dhamana ya kulinda vyombo hivyo hawana vitendea kazi, kwa hivyo, ningeomba kwa kila wakati wa doria *traffic* hao wapatiwe pikipiki za kutendea kazi. Leo askari wanaadhirika kweli kweli, wanamsimamisha hata mpanda baiskeli ambaye kafanya kosa wanashindwa kumfukuza kwa miguu na baadhi ya gari hazisimami, *traffic* wanatizama hivi hivi tunalipeleka wapi jeshi letu la polisi? Kwa hivyo kupitia kwako namuomba Waziri hili walisimamie vizuri sana pamoja na afande wangu *IGP* ndugu Mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakuja upande wa *pensioner,* kila nikisimama kwenye Bunge lako hili Tukufu huwa nasikitika sana na mikataba iliyoko ndani ya Jeshi la Polisi, na ndugu zangu wa Polisi kuanzia Mawaziri mpaka *Inspector General* wanasahau kwamba viongozi wetu baada ya kushika hatamu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano au ya Serikali na kuwaondosha wakoloni walisema maneno mawili. Yale yote ambayo yaliyo mazuri waliotuachia wakoloni tutayaboresha na tutakuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yale yote ambayo hayafai ndani ya wananchi wetu tutayakataa basi *pensioner* na kiinua mgongo na mkataba wa jeshi la polisi, mie nafsi yangu naukataa. Hauendi sambamba, kwa sababu itakuwaje, ikifika miaka kumi na mbili askari anaulizwa ajaze mikataba mitatu, kwa nini na waweke moja kwa moja aendelee na kazi au aingie kwenye *pensionable*, kwa sababu askari yule anasema mimi nataka kiinua mgongo, lakini atafanya miaka thelathini halafu anakujasikitika na wamekwama, sasa kwa nini polisi au wakuu wa polisi hawafanyi masahihisho kama wenzao hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na ndugu zetu wafanyakazi, wafanyakazi hao walijaza *pension* kwa mkupuo, lakini hapa tumewagundua na sasa wanapokea kama kawaida lakini ikifika kila Bajeti hapa wanazidishiwa mshahara, ndugu zetu wa polisi ambao walioganda kwenye kiinua mgongo hadi leo hawayapati matunda yao, wakwamueni hawa, *police general order* kifungu hicho kiondosheni kuwe na mikataba miwili tu ikifika miaka kumi na mbili uendelee na kazi au uache pale pale ukiendelea uwe mtu wa *pensionable* moja kwa moja huwezi uache na wale ambao walikwama kwa hivi sasa wakwamuliwe itakuwaje mtu akishakuwa pale lakini akifika *Sergeant,* kama yuko karibu na viongozi atafanyiwa mpango aende wapi apate kozi na apate cheo awe *inspector* ili aganduke na kiinua mgongo, akishakuwa ofisa tu basi kinamganguka, lakini wale pangu pa kavu kama mie hana kwa kwenda vinamganda, anaacha kazi kwa muda wa miaka thelathini anapata shilingi milioni moja laki mbili au shilingi laki nane, hii kweli haki ya binadamu? Sawa sawa na mikataba itakuwaje askari wa polisi afanye kazi kwa muda wa miaka thelathini leo aje apate shilingi laki nane, halafu wakati huo huo hana pensheni, hivi tutawatizama nini na atashawishiwa vipi huyu ndani ya Serikali. Kwa hivyo na hili ningeomba safari hii nisipate jibu kwamba wana hiari, wale sasa hawana hiari wako chini ya nchi lazima turekebishe mambo ambayo hayaendi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ndugu zangu hawa *Sergeant Arms*, ndugu zangu hawa na wale wote wanaofanya kazi eneo hili la Wabunge kila nikija mie nawaona hawana *seniority,* hawapati vyeo hawa, hawapati vyeo na wanadili na viongozi wakubwa tu, sijui sababu sasa mie jambo la kwanza ningeomba tu nijibiwe kwamba wako ndani ya usalama wa raia na wao ni polisi au wao wako sehemu kama ile tunayoitaja askari wa binafsi nje kule, kama nao wako ndani ya jeshi hili la polisi wanafanya kazi nzito waonekane waende kozi kama wenzao tukija tufurahi aliyekuwa Koplo awe *Sergeant*, aliye *Sergeant* awe *Inspector* na aliye *Inspector* azidi kupanda, askari wa kawaida achukue Koplo na hii sisi tutafarijika, tutajua kwamba wale ambao wapo karibu wanatuenzi na wao wanaenziwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ukiwa unaumwa umesema hivyo, je, ungekuwa mzima mambo yangekuwa magumu.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Bajeti ya Wizara hii iliyoko mbele yetu hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamanda wote wa Jeshi la Polisi pamoja na askari wote wa jeshi la polisi kwa kazi nzuri ambayo wameweza kuifanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi majuzi tu nchi yetu tena iliingia tena kwenye wimbi la ujambazi, Wabunge pamoja na wananchi tulipata tena wasiwasi kama tulioupata kipindi kile kilichopita nchi yetu ilivyovamiwa tena na wimbi hili la ujambazi. Lakini nalishukuru jeshi la polisi pamoja na askari wote ambavyo wameweza kuifanya kazi hii vizuri na kuweza kuwakamata majambazi ambao waliweza kuiba kule Mwanga na Arusha, nawapongeza sana na ninaomba vijana wetu wa polisi wawe na moyo huo huo kuilinda nchi pamoja na raia na mali zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na vifaa kwa ajili ya askari wetu, tumesoma kwenye vyombo vya habari kwamba wale majambazi waliokamatwa kule Arusha walikutwa na fulana za kuweza kuzuia risasi, lakini sidhani kama askari wetu walikuwa nazo. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kuiomba Wizara kwamba vifaa ni muhimu sana kwa askari wetu ili waweze kuitetea nchi na kuweza kupambana vizuri na majambazi ni vizuri kupata vifaa hivyo vya kisasa na wangekuwa navyo naamini kabisa mapambano yale yasingechukua muda mrefu hivyo wangeweza kuwakamata kwa urahisi. Hivyo ningeomba sana suala hili la vifaa liweze kupewa uzito wa kutosha ili kuwatia moyo na kuwatia nguvu askari wetu kwamba tunawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni nyumba za askari, pamoja na kuwa Waziri amelizungumzia suala hili katika hotuba yake lakini kwa idadi ya nyumba alizozisema katika hotuba yake hazitoshelezi kwa askari tulionao katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wamesemea sana suala hili la nyumba katika maswali na katika michango mbalimbali iliyotolewa katika Bunge lako Tukufu. Tunaiomba Wizara ilichukulie maanani suala hili la nyumba, ili askari wetu wote waweze kupata nyumba kuwaondoa kule mitaani wanakoishi uraiani, ili kuweza kurudisha ile heshima ya jeshi na maadili ya jeshi kukaa kwenye kambi zao na ninalisema hili kwa kuwa ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu na hasa kwa wale askari ambao wako vijijini. Miji ni tatizo lipo lakini vijijini wao wana tatizo zaidi la nyumba na hata usafiri na hii inawasababishia kushindwa kufanya kazi zao vizuri kwenye vituo walivyopelekwa. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba nyumba zitajengwa ila sijui ramani yake ikoje, zisije zikawa ni zile nyumba tulizozoea za *bedroom* moja au mbili ndio zitakazojengwa tujue askari wetu wameoa, wana watoto wa jinsia mbili wa kike na wa

kiume, tusingependa tena zile nyumba za zamani zikajengwa sasa. Hatuwezi kumshirikisha dada na kaka kukaa chumba kimoja na kuvaa nguo katika chumba kimoja. Tunaomba *room* ziongezwe kwa askari wetu hawa ili waendelee kuipenda kazi yao na kufanya vizuri zaidi katika kazi zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningependa kulisema ni maslahi ya askari wetu, maslahi ni muhimu sana kwa wafanyakazi na hasa katika hawa askari wetu wa chini ambao hawana vyeo vikubwa kama wengine. Kumekuwa na malalamiko mengi kwamba maslahi yao ni madogo na ukizingatia kazi wanazozifanya wana kila sababu na wao kuongezewa maslahi yao ili waweze kutenda kazi zao vizuri na tukifanya hivi itapunguza tatizo zima la rushwa, kujiingiza kwenye vishawishi vya rushwa wengi wanafanya hivi kutokana na maslahi yao kuwa madogo, wanashindwa kujikimu wao na familia zao, gharama za shule ni kubwa, gharama za kuwasafirisha watoto wao kwenda shule ndiyo hivyo tena, kwa hiyo inabidi suala hili tulitazame vizuri ili askari wetu wafanye kazi zao vizuri na hili ni pamoja na kupandishwa vyeo kumekuwa na malalamiko hasa ya kupandishwa vyeo kwa askari wetu, tunaomba hili litazamwe, wapandishwe vyeo vyao kwa wakati, vilingane pamoja na maslahi yao na hili niungane na msemaji wa mwisho aliyowasemea askari wetu walioko katika Bunge letu nao tungependa nao waangaliwe hasa katika kupandishwa vyeo na maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye ajali za barabarani, tumekumbwa na ajali za barabarani kwa muda mrefu wananchi wetu wamepoteza maisha na wengi ni wale wanaotumainiwa na familia zao familia nyingi zimekosa walezi kwa sababu ya madereva ambao wanashindwa kufuata maadili au wengine hawana leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kupongeza pia hatua zilizochukuliwa ambazo ni za ukaguzi wa leseni kwa madereva, na hili ningeliomba zoezi hili lifanyike kwa madereva wa magari makubwa na madogo tusifanye tu kwa magari makubwa, kwa sababu wako madereva wengine wa magari madogo nao wanasababisha ajali za barabarani. Kwa hiyo zoezi hli lifanyike kwa madereva wote na ukaguzi wa leseni. na tungemuomba kamanda Kombe awasimamie vijana wake hawa wa *traffic* zoezi hili lisiendeleze tena kuibua lile tatizo kubwa tulilonalo la rushwa. Maana yake askari wa barabarani wengi tumewaona wakisimamisha magari na kuwashusha madereva kwenda nyuma ya magari yao, wengi wamesema lakini kinachotakiwa na tunachojua unapomsimamisha dereva unachomuuliza ni leseni yake, kama hana leseni huna sababu ya kumshusha unajua hatua za kuchukua. Kwa hiyo, tunaomba Kamanda Kombe alisimamie hili ili kuondoa hili tatizo la rushwa, na tunaomba *traffic* wafanye kazi zao kama maadili yao kazi yanavyowataka na si vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nije kwenye tatizo la ubambikizaji wa kesi, tatizo hili ni kubwa sana na hili limeondolea sifa jeshi letu la polisi pamoja na kuwa linafanya kazi nzuri lakini hili la ubambikizaji wa kesi limeondoa imani kwa wananchi. Hili ni tatizo kubwa sana na tunaliomba jeshi la polisi kwa kweli watilie nguvu ya ziada katika suala hili, wananchi wengi wananyanyasika kwa kubabikizwa kesi za uwongo, wanapopelekwa polisi kwa kesi moja ukitoka pale kupelekwa mahakamani, unakuwa na kesi nyingine mbili za ziada na hizo wanakwambia ni za faida unaongezewa kesi mbili

ambazo huzijui, kwa hiyo, unakwenda mahakamani na kesi tatu. Sasa utaratibu huu si mzuri unakosesha imani kabisa wananchi wetu na kesi nyingine zinakuwa ni za visa tu, aidha, kwenye biashara na wengi hata kunyang'anyana wanawake hii inasababishia watu kubabikizwa kesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana suala hili lifanyiwe kazi na wale askari wote watakaokutwa na tuhuma hizi wachukuliwe hatua kali za kinidhamu na kufukuzwa kazi. Nakubambikizwa kesi huku nako kumesababisha kuwa na msongamano mkubwa sana magerezani, tungeomba kabla ya watu hawa kukamatwa uchunguzi huu wa kina ufanyike kwenye kesi zao ili waweze kupelekwa mahakamani ukiwa uchunguzi umekamilika. Tusipelekane tu kwa visa na kama tutafanya hivyo na kulitilia maanani suala hili litapunguza msongamano katika magereza yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala lingine la msongamo katika jiji la Dar es Salaam, kumekuwa na tatizo kubwa sana la msongamano katika jiji letu la Dar es Salaam, hasa pale taa za kuruhusu magari zinapokuwa haziwaki. Asubuhi kwanza nilichukua nafasi kumpongeza Kamanda Kombe lilipoanza zoezi la njia tatu, tulimuona akiwa na askari wake barabarani wakiwa wanaongoza magari nampongeza sana na hili limesaidia kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam, lakini vijana wake pale Kamanda wao anapoondoka na baada ya muda wa msongamano kupita ile saa tatu nao huwa wanaondoka na wanapoondoka tu, msongamano unarudi pale pale na hapo unakuta taa haziwaki za barabarani, unaweza ukatumia hata dakika kumi hakuna gari inayokwenda wala inayorudi wote wameziba barabara. Kwa hiyo, tunamuomba Kamanda Kombe awapange vijana wake hata pale baada ya muda wa saa tatu na ile saa tisa wakati watu wanatoka maofisini vijana hao wawe barabarani ili kuwaongoza watumiaji wa magari kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tungependa pia itolewe elimu kwa wale wanaotumia miguu kwa sababu zoezi hili la njia tatu limesababisha ajali na hata wengine kupoteza maisha. Kwa hiyo, tunaomba elimu itolewe na wananchi waelimishwe vizuri ili kupunguza tatizo hili la ajali. *(Makofi)*

Mwisho kabisa nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote ambao wameweza kulisaidia jeshi la polisi kwa kutoa vifaa mbalimbali ikiwemo magari na pikipiki kwa ajili ya jeshi letu. Lakini kwa hili la pikipiki naomba nisemee kidogo zile kofia wanazovaa askari wetu sasa sijui ni tofauti ya maumbile, kofia tunakozipata nyingi ni ndogo na hazifuniki vichwa vya askari wetu, kwa hiyo, tunaomba jeshi la polisi litazame hili ili waweze kupata *helmet* kubwa zaidi za ku-*cover* kichwa kizima ili pindi pale watakapopata ajali wasiumie katika vichwa vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda uliobakia hata ningempa hata msemaji wa haraka kabisa hautoshi, kwa hiyo, mchana tukirudi tukiwa na Mheshimiwa

Anna Lupembe, Mheshimiwa Abdallah Sumri na Mheshimiwa Sevelina Mwijage basi tutakuwa na watatu tu, kwa hiyo, mjiandae.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 06:56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tulipoahirisha shughuli mchana niliwaita wafuatao kwamba wajiandae. Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Abdallah Sumry na Mheshimiwa Savelina Mwijage.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kwa jioni hii. Kwanza kabisa, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ulinzi wake mpaka siku hii ya leo. Pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kwa ushirikiano pamoja na umoja waliokuwa nao. Vile vile naomba nimpongeze Mkuu wa Majeshi - Said Mwema pamoja na Katibu kwa kazi nzuri ambazo wanazozifanya kwa kushirikiana na tumeona jitihada walizokuwa nazo kwa hali na mali mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie kwenye hoja moja kwa moja. Wilaya ya Mpanda haina Kituo cha Polisi, jengo ambalo Wilaya ya Mpanda wanatumia jengo la Halmashauri ya Mpanda Mjini. Ukiangalia sasa hivi Wilaya ya Mpanda ni Wilaya ambayo imekuwa ina wakazi wengi, ina wakimbizi wengi, maafa mengi, mauaji mengi yanatokea, sasa nashangaa mpaka sasa hivi Serikali haikuchukua jukumu lolote la kujenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la Halmashauri wanalotumia Polisi Wilaya ya Mpanda ni ndogo sana, pia sehemu ya mahabusu ni nje ya jengo pale *counter.* Ina maana mhalifu lazima atoke pale wamtembeze kwenye hatua chache mpaka kwenye mahabusu. Kweli mhalifu ni mhalifu, lakini mara nyingine mhalifu vile vile anatakiwa ahifadhiwe sehemu nzuri asionekane, maana yake anatoka nje kabisa anatembea kila mtu anamwona akiwa pekupeku kuwa huyu ni mhalifu.

Sasa nilikuwa naomba Serikali ichukue jukumu hilo la kujenga Kituo cha Polisi haraka iwezekavyo, ione umuhimu kwamba Wilaya ya Mpanda inastahili kujengewa Kituo cha Polisi kutegemea na Wilaya yenyewe kwamba ni kubwa halafu wahalifu ni wengi kwa sababu kuna wakimbizi. Tuna makambi mawili ya wakimbizi, Katumba pamoja na Mishamo. Vile vile ukizingatia Wilaya ya Mpanda imezungukwa na mapori. Yale mapori mara nyingine wahalifu wanajificha kule kama majambazi, hivyo kunakuwa kuna majambazi wengi na wale mapolisi ni wachache ambao hawawezi kumudu kazi ile. Nilikuwa naomba Serikali iangalie kwa ukaribu Wilaya ya Mpanda kutokana na hali

halisi ya Wilaya ile ilivyo. Naomba waongezwe askari, wawe wengi ili wafanye kazi yao kwa ufanisi mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende Tarafa ya Kalema. Katika Wilaya ya Kalema wale wananchi wa Kalema walichanga shilingi milioni mbili kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi, ukizingatia Tarafa ya Kalema iko Ziwa Tanganyika, kuna mambo mengi ya ajabu ajabu ambayo yanafanyika katika Tarafa ile. Sasa ukiangalia, hawa wananchi wa Kalema wamechanga shilingi milioni mbili wakajenga jengo la Kituo cha Polisi mpaka kwenye lenta na wakatafuta mabati yao wenyewe wanayoyajua wakaenda kuezeka, lakini Serikali mpaka sasa hivi haikuchukua jukumu lolote kuweza kuwasaidia wale wananchi wa Kalema kuona jitihada ambazo walizozifanya na ukizingatia pale ni mpakani mwa Kongo pamoja na Burundi, uharibifu ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Serikali ichukue jukumu la kuwasaidia hawa wananchi wa Kalema ili kuweza kuwapa moyo waweze kujenga hiki Kituo cha Polisi, wakimalizie hiki Kituo cha Polisi, waone umuhimu wa hawa watu wa Kalema wamefanya nini mpaka sasa hivi. Kusema kweli wanalalamika, wanasema sisi hatuwezi kuchanga kitu chochote, tumejaribu kujenga hiki Kituo cha Polisi lakini Serikali haichukui jukumu lolote la kuweza kutusaidia. Nilikuwa naomba Serikali ione umuhimu kuwaunga mkono wale wananchi wa Kalema ili waweze kumalizia kile Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba sehemu moja ya Tarafa ya Chala katika Wilaya ya Nkasi, nao wananchi wa Tarafa ya Chala wamejenga jengo mpaka kwenye lenta toka mwaka 1990, lile jengo mpaka sasa hivi halijaangaliwa wala halijulikani kama ni jengo. Kama kweli wananchi watupa pesa zao pale, wanajua pana matatizo gani. Nilikuwa naomba Serikali iwaunge mkono wale wananchi, wamechanga hela zao kusema wajenge Kituo cha Polisi lakini Serikali haijaona umuhimu wa wale wananchi. Nilikuwa naomba Serikali ione umuhimu wa kuona hiki kituo cha Chala pale sasa hivi walipo kwenye chumba cha Chuo cha Maendeleo ya Jamii, ina maana kama wamehifadhiwa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii wamepewa chumba kidogo sana ambapo hata mhalifu akipatikanika pale hawajui wampeleke wapi. Nilikuwa naomba Serikali ione umuhimu wa Tarafa ya Chala kuwajengea au kuwamalizia kile kituo maana yake wamejenga kile kituo mpaka kwenye lenta.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kuwa hawa maaskari wasikae sehemu moja kwa muda mrefu, tulikuwa tunaomba wakikaa muda fulani wahamishwe kwa ajili wakishazoeana na raia napo inakuwa shida na inakuwa matatizo. Tulikuwa tuomba wakiona labda askari wamekaa miaka mitatu au minne askari huyo ahamishwe kuliko akae miaka 10 au unakuta askari mwingine anakaa mpaka miaka 15 anazoeana na raia kiasi ambacho hata ile kazi hawezi kufanya vizuri kwa uaminifu anakuwa amezoeana mno na raia, tulikuwa tunaomba Serikali ichukue jukumu la kuwahamisha hawa askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya vita vya Tanzania na Uganda baadhi ya wanajeshi wetu walijiunga na Polisi, wengine walijiunga na Magereza. Polisi wengi walijiunga na Jeshi la Magereza na Polisi mpaka sasa hivi hawajui yale mafao yao

wayapate wapi. Sasa nilikuwa naomba Jeshi la Polisi, wale askari ambao waliopigana vita na wamestaafu, wajulikane kama nao vile vile walipigana vita ya Tanzania na Uganda na vile wakatoka pale katika Jeshi la JWTZ halafu wakaenda Polisi na wengine wakaenda Magereza. Wajulikane yale mafao yao yako wapi, maana yake sasa hivi wanahangaika wala hawajui wafuate wapi mafao yao. Naomba Serikali iweke utaratibu mzuri ili hawa watu waweze kujua mafao yao yako wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo sina mengi, naomba niunge mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH S. SUMRY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii ya leo ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya Usalama wa Raia, kwanza kabla ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Kamishna wetu wa Polisi, ndugu yetu Said Mwema na Maafisa wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Wizara hii na matunda yake yanajionyesha katika kila pembe ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nakupongeza wewe kwa kazi nzuri unayoifanya ndani ya Bunge letu, mlezi wa Mkoa wetu wa Rukwa, nakupongeza sana kwa kuliendesha Bunge letu. Pia ninazipongeza Wizara zote za Serikali yetu ya awamu ya nne na Serikali yetu ya awamu ya tatu iliyopita na huko nyuma kwa sababu huko nyuma ndiko kumetufikisha hapa na tunakwenda vizuri. Vile vile ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kazi ngumu walizonazo ndani ya maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, natoa salamu zangu za rambirambi kutoka kwa wananchi wa Mpanda Magharibi kwa Mheshimiwa Ameir juu ya msiba uliotokea huko Zanzibar. Tunampa pole sana na tunawatakia maumivu madogo na Mungu awasaidie kwa wale waliotutangulia na sisi tunafuatia. *Amina!*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lugha ya kwetu wanasema, *mtilansila akofikila*. Maana yake ni kwamba, ukiwa na shida ukienda mahali, fika na ombi lako. Mimi binafsi kwa niaba ya wananchi wa Mpanda Magharibi ndani ya hoja yetu ya bajeti ya mwaka 2006/2007 nilifikisha malalamiko ya wananchi wetu wa Mpanda Magharibi kwa ajili ya vijana wetu waliotekwa nyara na kuchukuliwa upande wa pili wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani wanakumbuka hoja hii ingawaje wameirithi, lakini tunasema, kazi ya Serikali ni moja na Mheshimiwa Mwema yuko hapa ananisikiliza. Mkurugenzi kabisa ndani ya *Interpol* ya dunia yetu hii, aliniahidi katika Bunge lililopita kwamba atafuatilia shauri hili na nitapata majibu kuhusu wananchi wale waliotekwa nyara na kuchukuliwa kwenda Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo lakini kwa miezi yote hii mpaka sasa hatujapata jibu lolote kama ni wazima au wafu. Tunaiomba Serikali ifuatilie shauri hili na kutupa majibu kwa lile linalotokea. Serikali tunaitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Tarafa ya Karema wamenituma, wananchi wa Jimbo la Mpanda Magharibi wanaulizia juu ya watoto wao na wameniambia nimwulize Mheshimiwa Waziri kupitia vyombo vyake katika jibu la jioni hii ya leo ataje majina ya wale watoto na mimi nisiyataje kabisa ili wasikie wao wenyewe akitaja jina moja baada ya lingine ili waweze kujua kwamba kweli Serikali yetu, kupitia Wizara hii pamoja na mamlaka yake inafuatilia habari zao hawa vijana wetu, kuwa nyie wenyewe mtaje majina yao hapa. Hicho ni kitendawili, sina wasiwasi kwa umahiri na uwezo wenu, nadhani mtanipa jibu jioni hii ya leo ili kusudi wananchi wa Tarafa ya Karema, wananchi wa Jimbo la Mpanda Magharibi, wazazi hawa wanauliza juu ya habari za watoto waweze kupata taarifa kamili, kama imewezekana au imeshindikana kwa sababu kwa sauti yangu sijapata taarifa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho ninakigusia jioni hii ya leo ni kuhusu Kituo changu cha Karema. Katika Bunge la Bajeti mwaka 2006/2007 ndani ya Bunge letu Tukufu na mbele ya ushahidi wa Kamishna wa Polisi, nililiarifu Bunge hili kwamba jengo lililojengwa na wananchi wa Karema kwa kujitolea kwa ajili ya Kituo cha Polisi Karema, Karema ikiwa ni mpaka na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mpaka na Zambia kwa kutumia ziwa lile, mpaka na Burundi kwa kutumia ziwa lile liliezuliwa na upepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kikao kile ndugu yangu *IGP* Said Mwema aliniambia tukutane Dar es Salaam na nilikwenda Dar es Salaam akanikabidhi kwa kikosi cha ujenzi kule Dar es Salaam. Kwa masikitiko makubwa nasema ndani ya Bunge hili, kwa mwaka mzima hakuna kilichofanyika kule. Sio sauti yangu mimi, sio sauti ya Mheshimiwa Said Mwema, kwa kikundi cha ujenzi hakuna kilichofanyika mpaka sasa. Ninasikitika!

Leo hii Mheshimiwa Waziri, tena ndugu yangu Mwapachu na ndugu yangu sitaki kusema jina lako, nasema muitazame Karema kwa jicho la huruma, kwamba pale ni kioo na ni sura ya mpaka wetu kwa nchi jirani, kituo kile kiweze kufanya kazi vizuri na tuweze kupata msaada wa Serikali kwa dhati kukamilisha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mpanda inaunganisha ukubwa wake sawa sawa na Mkoa wa Tanga na Kilimanjaro, vitendea kazi hatuna. Mwaka jana nilipiga kelele nikaomba tusaidiwe angalau yale magari ya zamani yaweze kuhudumia kule katika mpaka wetu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, mpaka ambao unaingiliwa na wakimbizi wengi angalau tukarabatiwe gari moja kati ya magari yale mabovu yafanye huduma kule na ahadi hii tulisema na jibu nililipata kwamba itawezekana, tutajaribu na nafasi itakapojitokeza tutawasaidieni. Tunataka kutimiziwa ahadi hiyo. Tunaomba tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yetu ya mpaka, ninawaomba viongozi wetu ndani ya Polisi, ninaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu wako mtutazame kwa jicho la pekee mkijua kwamba katika maeneo yetu, yale ni maeneo nyeti, maeneo hatari yanayokabiliwa na wavukaji wanaotumia silaha mbalimbali ili ulinzi wetu uimarike na maisha ya watu yaweze kuwa katika amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilikuwa naiomba Wizara iweze kutazama sura mpya katika maeneo yetu haya makubwa na mapana sana ili tuweze kupewa vituo vingine zaidi kwa kupata askari zaidi. Wananchi wako tayari kuweza kujenga kwa nguvu zao ili waweze kuimarisha usalama katika maeneo yetu.

Kuna maeneo kama vile Kamsanga, Ilebula, Ifukutwa, Kibo, Mnyamasi, Bugwe, Katuma, Kakese pamoja na maeneo yaliyo jirani na Kakese. Watu katika maeneo hayo ni wazalishaji wakubwa, kilimo cha mazao mbalimbali na wafugaji. Mara nyingi majambazi wanaojitokeza katika maeneo hayo. Wanawakosesha amani wananchi wetu. Wananchi hawa inabidi wasafiri kwa kilometa 80 au kilometa 100, kwenda kuhudumiwa kwenye Kituo cha Polisi Mjini Mpanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu kufanya safari na kufika katika maeneo hayo ni shauri gumu kabisa, basi ananywea, analaumu Serikali yake na wakati huo huo hana jinsi ya kufanya kwa sababu ile nenda rudi hawezi kuitekeleza kwa uwezo mdogo.

Kwa hali hii, ninaomba kwa Mheshimiwa Waziri atazame kwa sura mpya kule Kakese kutufungulia Kituo kidogo cha Polisi, huko Katuma tufunguliwe Kituo kidogo cha Polisi na wananchi wako tayari kujitolea kwa nguvu zao ingawaje wana kazi nyingi kwa ajili ya Zahanati, Shule zetu lakini bado wapo tayari kutekeleza agizo la usalama wa raia na kuanzisha vituo kwa ajili ya usalama wao na mali zao. Kibo na Ufukutwa nao wapo tayari kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi nazidi kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya, wametia ulinzi mzuri katika maeneo yetu pamoja na kwamba askari hawa ni wachache sana.

Tunaomba tuongezewe katika maeneo ya mpakani askari wa kutosha na katika Wilaya zetu tupewe vitendea kazi ili waweze kumudu ukubwa wa maeneo yetu na kuweza kutimiza wajibu wao katika ulinzi wa raia zetu. Mpango wa ujenzi wa nyumba za Askari wetu Mjini tu, ufike hadi vituo vidogo na hasa mipakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo binafsi yangu ninaunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Wizara ya Usalama wa Raia. Ninampongeza Mheshimiwa Mfuru - Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Said Mwema na pia Mheshimiwa Tosi kwa kazi aliyoifanya Bukoba ambayo haitasahaulika katika maisha ya watu wa Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja hadi kwenye Wizara. Kila mara niposimama hapa nasimamia usalama wa raia katika Mkoa wa Kagera kulingana na matatizo waliyoyapata na tuliyoyapata kwa pamoja katika kipindi hiki cha majambazi pamoja na wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masikitiko niliyonayo ni maaskari wenyewe wanavyopelekwa kwenye pori katikati ya Kasindaga, Burigi na Kimisi, hawana hata mawasiliano ya kuweza kuwasiliana na kule walikotoka na pale walipo inaniuma sana kwa sababu wakivamiwa kule ni mara moja kuuawa, kuja kupata mawasiliano mpaka apande mti kuja kuwasiliana na mtu wa Bukoba Mjini na tunawategemea sana na jeshi hili kweli wanafanya kazi ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakimbilia kwenye makazi yao wanapoishi askari wetu. Kweli tunapenda kuwafanyisha kazi hawa Askari Polisi, lakini tunashindwa kuwasaidia. ninaiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iwasaidie maaskari hawa, siyo Mkoa wa Kagera pekee bali Tanzania nzima. Ukifika kwenye kikosi cha *FFU* pale Nshambya ukiangalia majumba yao wanapoishi kweli inaonekana Serikali imewasahau, labda Mkoa wa Kagera peke yake.

Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri angalau awakarabatie wapate sehemu ya kuishi, nyumba zao ziwe na hadhi angalau ya kuonekana. Tunaona kuwapigia simu majambazi wako hapa wanakuja wanakimbia magari yenyewe mabovu wanakimbizana nayo yanazimika, wewe mwenyewe uliyepiga simu wakusaidie unakufa kabla wenyewe hawajafika unabaki kuwalaumu unasema maaskari hawanisaidii. Siyo kusema hawakusaidii ni kwa sababu hawana usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu matibabu. Ninaomba Serikali iwaangalie angalau iwafungulie zahanati katika *line* yao ya Polisi. Sio mtoto wa askari anaumwa anatoka kazini na mavazi yake anabeba mtoto kwenye *government* kupanga foleni na mimi hapa. Ni aibu kuona askari kazi anayotufanyia na yeye kapanga foleni ana mtoto pale! Serikali iwaangalie kuwajengea zahanati au kuwawekea katika *line* zao za Polisi waweze kuwa wanarudia karibu, siyo kubebana na mtoto na nini kwenda mpaka kwenye kupanga foleni pale. Ni aibu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakimbilia kwenye mshahara, wameshakuwa na kauli ya kusemwa kwamba askari wanakula rushwa. Sio kula rushwa, ni mshahara wao mdogo! Muwakumbuke kwenye mshahara msiwasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nipo kwa maaskari. Kabla sijakwenda mbali, suala lingine ninalotaka kuongelea ni kuhusu maaskari wa hapa Dar es Salaam katikati mjini maaskari wanapewa pikipiki na *radio call,* lakini hasa wa kule porini wanashindwa kuwa na *radio call* mkononi! Kwa nini wale wa kule porini msiwape mawasiliano ya *radio call* kuliko kuwapa wa hapa hapa mjini ambao wapo karibu, wana pikipiki kubwa, Askari Polisi wa kule wanatembea na miguu! Naomba chonde, Mheshimiwa Waziri aonee huruma hawa maaskari. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda upane wa matrafiki. Matrafiki wa Mji wa Dar es Salaam wameshazoeana kabisa na madereva wa madaladala, wanawadharau.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba wahamishwe wapelekwe kwenye mikoa angalau wabadilishwe labda watafanya kazi vizuri kuliko kufanya kazi ambayo wameshazoeana kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika mambo haya niliyoyachangia angalau wawaonee huruma hawa maaskari na kazi zao ngumu, maana hawana hata magari ya kuwatoa wafungwa Polisi kuwapeleka Mahakamani. Unakuta wanatembea na maaskari mwisho wake yule mhalifu anaweza akamvamia pale akamnyang'anya bunduki yake akampiga nayo. Kama siku moja tulivyovamiwa tunatoka Tunduru, askari ameshikilia bunduki yuko kweye gari la korosho ndio wakamkamata wakaanza kumnnyang'anya bunduki.

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwepo askari jeshi anasafiri wakampiga risasi. Hiyo ni kwa sababu hakuna mawasiliano yoyote ya kupiga simu kwenye kituo chochote kwenda kupata msaada. Kwa hiyo, tunawafanya kama chambo cha kuuwawa. Tusiwatumie kama chambo, kuna mikutano ya upinzani nenda mkawapige, kuna hiki nenda mkawavamie, nenda mkawapige *CUF* na mikutano tuwaangalie hata kwenye mawasiliano yao wenyewe binafsi waweze kupata na wenyewe maendeleo. Mengi nilikuwa nimeshachangia kwenye maandishi. Naomba niishie hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia angalau machache katika Wizara hii nyeti ya Usalama wa Raia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana kwa niaba ya Wanawake wa Mkoa Kusini Pemba kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Mwapachu na Mheshimiwa Kaka yangu Mohamed Aboud Mohamed kwa kazi nzuri ambayo wanayoifanya kwa ushirikiano na wananchi na viongozi mbalimbali katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nisije kusahau, napenda kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo napenda kumpongeza *IGP* Mwema, hili jina la Mwema ni mwema kweli! Mambo yanayotokea sasa hivi katika maendeleo ya Wizara hii chini ya uongozi wa baba huyu Mwema, basi ni mwema kweli! Mama yake na baba yake walivyomzaa wakampa jina la Mwema, ni mwema kweli! Sio vizuri kuzaa watoto ukawaita jina la Shida, Hasara. Kwa hiyo, huyu ni mwema, nampongeza kwa kazi kubwa anayoifanya. Tunampenda sana wananchi. Tunamwomba aendelee na moyo huo huo kwa ushirikiano wa wananchi ili nchi hii iende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara, Makamanda mbalimbali na wapiganaji wetu kwa kazi nzuri ya kulinda nchi yetu. Moja kwa moja niende kwenye hoja, napenda kuchangia kuhusu askari wa kike. Askari wa kike au askari wanawake ni askari ambao tunawategemea sana katika nchi hii. Askari wa kike ni wajasiri, ni waaminifu, kwa hiyo basi, naomba sana Serikali iwaone zaidi askari wa kike kwa kuwapandisha vyeo. Maana akina baba wengine si unajua tena wanapenda kudharau wanawake! Lakini napenda kuomba Serikali iwaone wanavyofanya kazi askari

wa kike na wawape haki ambayo inastahili, wasione kama ni wanawake tu! Wanawake mbele, wanawake mbele kimaendeleo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia moja kwa moja kwenye nyumba za Askari Polisi za Mfikiwa Jimbo la Wawi kule Chakechake Pemba. Napenda sana kuishukuru Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Wizara hii kwa kuwajengea nyumba nadhifu za kisasa Askari wetu wa Mfikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari hawa, zamani wengi wao walikuwa wanakaa kwenye mahema. Kwa kweli ilikuwa inatia huruma. Lakini tulivyokuwa tunapiga kelele hapa Bungeni, toka kipindi kile cha mwaka 2000, basi Serikali ni sikivu ikawajengea Askari hawa nyumba 53 za kisasa.

Kwa hiyo, napenda kuishukuru Serikali kwa uamuzi huu wa kuwajengea nyumba Askari wetu nao waishi katika mazingira mazuri, kwani kule tayari kuna umeme na maji.

Naomba kitu kimoja. Askari wanaoishi kule, ni mbali kidogo yaani ni kijijini, kwa hiyo, napenda na wao wafikishiwe angalau shule ya chekechea watoto wao waweze kusoma pale angalau vyumba viwili. Vilevile na Kituo cha Afya na uwanja wa michezo kama tunavyojua michezo Askari wanapenda sana, baada ya kazi kubwa wanayoifanya kwa mchana kutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja kwenye ukarabati wa nyumba za Askari Polisi za Madungu Chakechake Pemba. Zile nyumba zimejengwa toka bibi yangu hajazaliwa. Nafikiri enzi za ukoloni, yaani enzi za zamani, yaani ni mbovu, wale Askari wanavujiwa ndani na nyumba zenyewe vyumba viwili, watoto humo humo wa kike na wa kiume, baba na mama sijui akitokea mgani wanamlaza wapi!

Mheshimiwa Naibu Spika, zile nyumba ni mbovu! Naomba kama bajeti hii haikutengwa, basi wafikiriwe angalau ukarabati katika zile nyumba za Madungu. Askari wanaishi katika mazingira magumu sana, kwani huwezi kuishi baba na mama na mtoto chumba hicho hicho, ni hasara tunawafundisha watoto tabia mbaya. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nyumba hizo zifanyiwe ukarabati wa haraka hata kama bajeti haikupangwa mwaka huu, basi bajeti inayokuja naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati wa Ofisi ya Mkoa Kusini Pemba, halikadhalika jengo hili ni la zamani sana. Jengo linategemewa sana na wananchi na viongozi na Serikali hii, lakini ni bovu, la zamani sana, mazingira siyo mazuri, basi hapo ije inyeshe mvua, we! Siku moja nilikwenda pale, nilikuwa na shida zangu nyingine, mvua ikawa inanyesha, mvua mpaka ndani, Askari hawajui wakae wapi. Yaani wanafanya kuhamisha vitu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ile naomba sana ifanyiwe ukarabati na hii siyo mara ya kwanza au ya pili, wala ya tatu, ya nne, au ya tano. Hii nafikiri ni mara ya sita

tunatetea jengo lile. Tunaomba sana ukarabati ufanyike hata kama sio kwa mwaka huu lakini Serikali ione kwamba ile ofisi pale ni muhimu sana, kwa hiyo, ifanyiwe ukarabati.

Ujenzi na ukarabati wa nyumba za Askari wa *FFU* - Finya Wilaya ya Wete. Kwanza napenda kuishukuru Serikali hii na Wizara yetu kwa kujenga zile nyumba kwa muda huu. Zamani zilikaa sana zikawa hazijajengwa, lakini sasa hivi zinaendelea katika *process* ya kujengwa. Kwa hiyo, naomba Serikali isisite, hapo mafungu ambayo yanaingizwa katika ujenzi kwa kule Pemba sijaona hata moja. Naomba fungu kama halipo, basi litafutwe popote ziendelezwe zile nyumba. Pale naona umeme tayari, lakini mambo ya maji pia yana matatizo.

Naomba sana ukarabati wa nyumba za *FFU* – Finya, unajua hawa Askari wa *FFU* kule kwenye (tunawaita) "Fanya Fujo Uone". Hawa Askari ni Askari ambao wanafanya kazi usiku na mchana. Mahali popote panatokea fujo wakionekana wao tu, adui hafikii pale, mbio anakimbia. Ni Askari ambao ni watii na wanafanya kazi kwa bidii katika kuilinda nchi hii na raia wake.

Kwa hiyo, tunapenda sana na wao wahifadhiwe kwa vile na wao wanafanya kazi kubwa ya kulinda usalama wa raia na wao waonekane kama ni binadamu na wawekwe katika sehemu nzuri, maana kama Askari hujamweka sehemu nzuri pia naye roho yake inanyongea, siyo vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda kwenye Usalama wa Raia. Usalama wa Raia napenda kusema kwamba kwa mimi, siyo kwa kila mtu, ninaweza nikasema hapa na mwingine akasema vingine. Lakini mimi naona sasa hivi hali ni shwari sana Zanzibar. Hali ya kisiasa ni shwari sana na hali hii inatokana na ushirikiano mzuri wa viongozi wa Serikali yetu wa vyama vyetu, Askari wenyewe na hata raia wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaona kwamba hali ya mfarakano na vita na mauaji ya kila siku sio mazuri, kwa hiyo, wananchi wameelimishwa na wameelimika vizuri na hivi sasa wananchi ni rafiki wa Askari na Askari vilevile ni rafiki wa raia, yaani wananchi. Naomba Serikali na wananchi tuchukue jukumu hili ili kuendeleza ushwari huu au usalama huu uliopo katika Kisiwa chetu hasa cha Pemba. Wote ni ndugu moja, tusahau yaliyopita tujenge Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika huu Usalama wa Raia au hii hali ya usalama kule Zanzibar, basi kukiwa na usalama hata wawekezaji wanakuja na wanakuwa wengi na wanatuletea manufaa katika nchi yetu. Nawaomba sana wawekezaji wa nje na wawekezaji wa ndani waje Zanzibar, sasa hivi hali ni shwari. Waje Zanzibar wawekeze na wafanye biashara zao kwa usalama ambao upo kwa ushirikiano mzuri wa wananchi na vyombo hivi vya usalama wa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu hiki mimi sijaona michezo, sijui kwa nini! Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu kafanya hivi mara hii. Michezo ni furaha, ni kazi, afya pia michezo huepusha majanga mbalimbali. Si mnajua majanga mengine kama hujafanya michezo kama *netball, football* na kadhalika unakwenda kufanya majanga

mengine! Lakini ukiwa kwenye michezo mchana kutwa; unakwenda kwenye kazi, jioni una *refresh mind* kwa kucheza *football, netball* na michezo mingine, akina baba na akina mama, kwa hiyo, inakuwa raha zaidi.

Naomba fungu hata kama halijaingizwa wakati huu fungu la michezo liingizwe mwaka unaokuja. Askari wetu wana timu mbalimbali za *Premium,* wanacheza timu mbalimbali, kwa nini tunawadharau na kuwakosesha haki zao za kufanya michezo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya doria baharini kwa kule Zanzibar, Zanzibar ni kisiwa kama tunavyojua. Kwa hiyo, wahalifu wengi huwa wanapitia zile njia za baharini, wakitoka nchi nyingine za nje wanatumia meli na boti, tunaweza tukasema hivyo. Sasa vyombo vya baharini ni vichache, vile ni visiwa, tunataka tulinde Zanzibar yetu kwa sababu adui yeyote akiingia Zanzibar, ameingia Tanzania nzima.

Kwa hiyo, naomba sana boti za doria ziwe kwa wingi vilevile vifaa mbalimbali vya mawasiliano kama simu yaongezwe kwa Askari waliopo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiinua mgongo kwa Askari wanaostaafu, wenzangu walizungumza hapa. Tusiwaone Askari wazuri na vilevile wakakamavu na vilevile ni watii wakati tunawatumia, lazima tuwatayarishe. Imo kwenye kitabu cha bajeti kwamba wanatayarishwa kwa *SACCOS* na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali, kwani hiki ni kitendo kizuri sana cha kuwatayarisha Askari. Kuna siku nilisema hapa kwamba Askari ni vizuri watayarishwe kabla hawajastaafu, kumbe Waziri alinisikia kipindi cha nyuma alipokuwa Mbunge wa Jimbo la Wawi. Nilisema na *inshaalah* nitakuwa Mbunge wa Jimbo la Wawi.

Kwa hiyo, viinua mgongo vya Askari wetu tuvijali. Tuwatayarishie kabla hawajastaafu na siku wakistaafu wanachukua vitita vyao na pesa zao, lakini unakuta mtu mwezi wa kwanza, wa pili, wa tatu na hata mwaka mtu hajapata. Mtu anastaafu alishakuwa mzee mpaka anaota mvi, mpaka anatembea na mkongojo na mpaka anakufa hajapewa hela zake za kustaafu. Hiki sio kitendo kizuri. Naomba sana Serikali ifuatilie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba tena kuunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nashukuru kusema kwamba pamoja na muda mfupi, lakini tumepata wachangiaji 11. Nadhani inatosha, tuingie kwenye hatua nyingine.

Naibu Waziri naomba uanze kujibu hoja.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na uzima na kutupa uwezo wa kushiriki katika Bunge lako Tukufu jioni hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nitoe mkono wa pole kwa wananchi wote na Waheshimiwa Wabunge kwa misiba mbalimbali iliyotokea katika kipindi hiki, tumwombe Mwenyezi Mungu awalaze Marehemu hawa mahali pema Peponi, *Amina!* Lakini pia Mwenyezi Mungu awape subira wafiwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika na Wenyeviti wetu wa Bunge hili Tukufu kwa kazi nzuri na umahiri mkubwa katika kuliendesha Bunge letu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani maalumu ziende kwa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maelekezo. Ushauri wao na nasaha zao juu yetu, tunashukuru sana viongozi hawa kwa kutusaidia sana sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge lako hili Tukufu na Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wanatusaidia sana katika Wizara hii na matokeo yote haya mnayoyaona ni matokeo ya ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu pamoja na Watendaji, wafanyakazi na Askari wote wa Jeshi la Polisi kwa ushirikiano na utekelezaji mzuri wa majukumu yao. Nawashukuru sana.

Shukrani za pekee ziende kwa mke wangu na familia yangu kwa kunivumilia sana. Aidha, nawashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wao wanaotupatia katika kupambana na uhalifu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kuwa mchango wa Waheshimiwa Wabunge ni changamoto ya kuimarisha utendaji na kujipanga vizuri katika kupambana na uhalifu nchini ili nchi yetu iendelee kuwa johari ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa hoja ni nyingi na muda ni mfupi, naomba sana Waheshimiwa Wabunge watuwie radhi kama hoja nyingine hatutaweza kuzijibu hapa leo, lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa tutafanya kila jitihada kuwajibu hoja hizo kwa maandishi. Kwa hiyo, nawaomba sana muipitishe bajeti yetu bila vishindo ili tuwe na nguvu ya kufanya kazi vizuri zaidi, msituchoshe tukashindwa kufanya kazi zetu vizuri na mnajua tukichoka, uhalifu utaongezeka nchini na tunataka kupambana. Kwa hiyo, tunaomba hisani yenu. Naamini Mheshimiwa Waziri

wangu atakuja kujibu hoja nyingi. Lakini naomba nianze kwa kujibu baadhi ya hoja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa upande wa Kambi ya Upinzani. Rafiki yangu Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya kwanza namshukuru sana leo, ameanza kutumia karatasi za kijani, ni mwanzo mzuri sana. Nakupongeza sana Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Sanya wakati akiwasilisha hotuba yake hapa, aliwasilisha kwa karatasi za kijani. Ni mwanzo mzuri, Mungu amjalie kheri tukutane huku pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya alisema, baadhi ya Watendaji na Askari Polisi huwasaliti wale watu ambao hushirikiana nao kwa kutoa siri. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya kwamba sasa hivi tumejipanga vizuri kwenye suala ili wale wote ambao wanatoa siri za raia wema, tuwachukulie hatua kali sana. Tumepiga hatua kubwa sana kwenye jambo hili na ndiyo maana hata juzi tumefanikiwa vizuri sana katika kuficha hizo siri kwa kupambana na yale majambazi ya Njiro - Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kwa kazi nzuri sana waliyoifanya. Hii yote ni kuonyesha wazi kwamba sasa Askari wetu wako makini sana katika kutunza siri. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote waendelee kutupa taarifa ili tuweze kupambana na uhalifu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kambi ya Upinzani ilitaka Askari Polisi wakatiwe bima. Askari anapopoteza kiungo akiwa kazini hulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria, hata hivyo Serikali inalifanyia kazi suala hili katika maboresho yanayofanyika ndani ya Jeshi la Polisi. Hivi sasa maboresho yanakuja na inshalaha jambo hili litakuwepo.

Kuangalia vigezo vinavyofaa vya Askari Polisi kwa nchi za Afrika Mashariki, *SADDC* na zile za Jumuiya ya Madola vitumike kuboresha maslahi kwa Jeshi la Polisi hapa nchini. Uchumi wa nchi katika ukanda wa Afrika Mashariki, *SADDC* na zile za Jumuiya ya Madola hutofautiana, hivyo hata viwango vya maslahi hutofautiana. Tayari Wizara yangu imewasilisha mapendekezo ya marekebisho ya mishahara na posho za Askari kwenye Tume ya Rais ya Maboresho ya Mishahara, wanashauri Askari na Waheshimiwa Wabunge kuwa na ustahilimivu mkubwa kwani mambo mazuri hayataki haraka. Mambo yanakuja.

Kuhusu upelelezi wa kesi kufanyika haraka, Jeshi la Polisi lipo kwenye mpango wa maboresho ya Sekta ya Sheria ambapo suala la uharakishwaji katika upelelezi wa kesi ilizingatiwa katika Idara ya *CID* na vilevile tunafanya maboresho makubwa katika kukikuza kitengo hiki cha *CID* pamoja na kujenga Chuo cha *CID* hapa Dodoma na hivi sasa pia tunakarabati Chuo cha kule Kidatu kwa ajili ya kazi hiyo hiyo. Yote haya ni kutaka kufanya upelelezi wa haraka na kuongeza idadi ya Askari Wapelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala kwmaba makusanyo na maduhuli yabaki kutumika pale yanapokusanywa. Makusanyo yote kwa mujibu wa Katiba ya nchi hutakiwa kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, yaani *Consolidated Fund*. Matumizi yote ya fedha hizi mpaka yaidhinishwe na Bunge hili Tukufu, kwa hiyo, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya huo ndiyo utaratibu.

Kulikuwa na suala kuhusu upotevu wa pesa taslimu na vifaa vya shilingi milioni 200. Upotevu huu unahusiana na upotevu wa vifaa na fedha ambazo watu waliohusika na upotevu huo wameshafikishwa Mahakamani.

Pia kulikuwa na suala la ununuzi wa kutozingatia zabuni. Manunuzi haya yalikuwa ni ya dharura, lakini taratibu zote za manunuzi zilizingatiwa na barua ya kuhalalisha manunuzi haya imetumwa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukosefu wa Nyaraka za makubaliano ya Mikataba ya ujenzi wa nyumba za Polisi na Ofisi za Polisi ya shilingi bilioni 2.7, Mikataba hiyo imepatikana kutoka mikoani na imeshawasilishwa kwa wakaguzi na uhakiki umeanza wa Mikoa inayohusika ya Mwanza, Kagera, Iringa na Mbeya.

Malipo kwa kutumia Ankara Kifani shilingi milioni 31, hoja zinazohusika zimejibiwa na kufungwa. Kwa ujumla hoja zote zimeshajibiwa na kupelekwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali pamoja na Hazina.

Tatizo la rushwa ndogondogo kwa Askari Polisi wa vyeo vya chini, mafunzo yamefanyika kwa Askari wetu yakijumuisha raia, Madiwani, Watendaji wa Kata na hata vijiji kwa lengo la kuelimisha wahusika madhara ya rushwa na hatua mbalimbali zimechukuliwa kwa Askari waliopatikana na makosa haya na tutaendelea kuchukua hatua hizo na *RPCs,* wote Tanzania nzima wanalo toleo la kuagizwa wachukue hatua kali dhidi ya wale Askari wanaokula rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tushirikiane kupambana na vita hivi. Najua nia ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kupambana kwa kiasi kikubwa sana katika suala la rushwa na tunafanya hivyo kwa nguvu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu askari kutokulipwa posho wanaposafiri kikazi hapo hapo, bajeti ya Jeshi la Polisi halilingani na hali halisi ya matukio ya uhalifu. Aidha, inapotokea tukio la uhalifu, Jeshi la Polisi haliwezi kusubiri mpaka fedha ziwepo ndipo tukio la uhalifu lishughulikiwe. Hivyo wakati mwingine Askari huenda kwenye tukio bila kulipwa posho kwa vile huwa hakuna fedha. Hapa ndiyo tuona namna gani Askari wetu wanavyojitolea kujenga Taifa letu na tuone uadilifu wa Askari wetu kufanya kazi bila kujali fedha kwa ajili ya kuangalia maslahi ya Watanzania. Ninachukua fursa hii kuwapongeza sana. *(Makofi)*

Suala la Mtoto Mariamu aliyetoroshwa, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya alieleza kuhusu mtoto aliyetoroshwa kule Zanziabar. *Interpol Dar es Salaam* inaendelea kulishughulikia suala hili ambapo tayari taarifa za kutafutwa kwa mtuhumiwa

zimekwishatumwa nyumbani kwao Uganda na vilevile Afrika Kusini ambapo inasadikiwa alikimbilia mtuhumiwa huyo.

Vilevile taarifa za kutafutwa kwa mtuhumiwa zipo katika mtandao wa *Interpol* na mawasilano yanaendelea kufanyika. Kwa hiyo, tutakapowapata, Mheshimiwa Sanya atatuletea taarifa rasmi kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Suala la tatizo la Madawa ya Kulevya ni la Kimataifa. Tanzania imekuwa ikishiriki kikamilifu katika vita hii na tunaendelea na juhudi hizo. Hivi karibuni mmeona juhudi za raia mwenyewe katika suala hili, alikwenda Tanga kufanya mkutano mkubwa kwenye masuala haya. Kwa hiyo, jitihada zinafanyika kukabiliana na tatizo hili ikiwa ni pamoja na kuweka mbwa wa kunusa madawa katika viwanja vya ndege vya Zanzibar, *KIA* na J.K Nyerere.

Aidha, Jeshi la Polisi limefanikiwa kukamata madawa na watuhumiwa mbalimbali. Mfano wa madawa yaliyokamatwa Mkoani Mbeya ambapo yalikuwa yamepandikizwa ndani ya maiti, hiyo yote ni kuonyesha kwamba Jeshi letu linafanya kazi kubwa sana katika kupambana na uhalifu wa madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia nijibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, nianze na Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri ambaye yeye alitaka ipigwe marufuku ufungaji wa ngazi kwa magari ya daladala na mizigo. Wizara ya Usalama wa Raia ikiwasiliana na Wizara ya Viwanda, Biashara pamoja na Miundombinu ili kuhakikisha kwamba wamiliki wa magari ya abiria ambayo yamefunga ngazi zinazohatarisha maisha ya watumiaji wengine wa barabara, watachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba na Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan walitaka mabasi yote ya abiria yawe na mlango wa dharura. Kulingana na Sheria ya viwango ya Taifa ya mwaka 1999 kila basi la abiria ni lazima liwe na mlango wa dharura na mlango huo uwe na vipimo kama ilivyoidhinishwa katika Sheria hiyo, hivyo Serikali imetoa muda wa mwezi mmoja kuanzia Julai, 2007 ili mabasi yote ya abiria yawe na milango ya dharura baada ya muda huo kupita, mabasi ambayo hayatakuwa na milango hiyo hayataruhusiwa kubeba abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu itahakikisha kwamba Sheria hiyo inatekelezwa kikamilifu na hatutakuwa na muhali.

Vilevile Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri aliielezea Sheria ya Usalama Barabara kwamba iangaliwe upya. Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini pia alitaka suala hilo. Kufuatia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu ya mwaka 2007/2008 Wizara iko katika mchakato wa kuandaa Sera ya Taifa ya Usalama Barabarani, baada ya Sera hiyo kukamilika, inatarajiwa kwamba Sheria mbalimbali zinazohusiana na masuala ya Usalama Barabarani zitaangaliwa upya ikiwemo Sheria ya Usalama wa Barabarani Na.30 ya mwaka 1973.

Vilevile Mheshimiwa Rosemary Kasemba Kirigini na Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi walitaka suala la gari. Mheshimiwa Rosemary Kasembe Kirigini anataka gari ipatikane kwa *OCD* wa Musoma, kama nilivyoahidi ni kwamba suala hili tunalishughulikia na mara tutakapofanikiwa tutafanya kila jitihada tupate gari ya *OCD* pale Musoma.

Aidha, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi kwa kuwa Wilaya yake ya Rorya tunajua inakuwa Wilaya mpya karibuni hivi, kwa hiyo, kwanza, nakupongeza kwa hilo na tutafanya kila jitihada ili uweze kupata gari katika Wilaya hiyo. Tunaomba subira kwenu Waheshimiwa Wabunge, wakati tunashughulikia suala hili.

Aidha, Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula na Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo walisema kwamba Serikali itambue Sungusungu kisheria. Kwanza kabisa napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Sungusungu wanatambulika Kisheria chini ya Sheria ya Na. 27 ya mwaka 1975 *The People's Militaries Act Cap 111*.

Hata hivyo, Wizara yangu itaanza kuandaa Kanuni za kutekeleza Sheria hii ili kufafanua majukumu na mipaka ya kiutendaji ya Sungusungu. Kwa hiyo, tumo katika utaratibu wa kufanya Kanuni ili kuona kwamba Sungusungu wetu wanafanya kazi kwa mujibu wa taratibu za Kanuni ili kuepuka migongano mbalimbali inayojitokeza.

Vilevile Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa rafiki yangu Sheikh Abdallah Salim Sumry walizungumzia sana kuhusu Vituo vya Polisi katika maeneo yenu. Lakini ninachotaka niwahakikishie kwamba kama ninavyosema mara nyingi sana tuna mpango wa kufanya tathmini kuhusu mahitaji ya vituo vya Polisi nchini. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba mpango huu umekamilika na sasa tupo katika utaratibu wa kujenga vituo kufuatana na hali ya uwezo wa kifedha. Kwa hiyo, tunaomba subira yenu. Isipokuwa kwa ile Wilaya ya Mpanda Kituo cha Polisi cha Mpanda nataka nimhakikishie Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Abdallah Sumry kwamba tutafanya liwezekanalo tumalizie kituo hiki cha Mpanda.

Kuhusu vile vituo vingine vya Kalema, Nachala na kwingine Mheshimiwa naomba mtupe muda tuje huko tuangalie mazingira halisi kwa pamoja ili tutafute ufumbuzi wa kudumu katika matatizo haya. *(Makofi)*

Vilevile Waheshimiwa hawa walizungumzia utaratibu wa Polisi, Jamii iendelee na kuwapa Polisi vifaa na nyenzo za kutosha ili waweze kukabiliana na ujambazi. Kwanza kabisa, napenda niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuona umuhimu wa Askari Polisi kupatiwa vitendea kazi na vilevile ushirikishwaji wa wananchi katika suala zima la kuimarisha usalama chini ya utaratibu wa Polisi, jamii ishirikishwe katika kupanga mikakati ya kuzuia na kukabiliana na kero mbalimbali katika maeneo yao. Kwa hiyo, nataka niwahakikishie kabisa kwamba hivi karibuni tu tumeanza mchakato wa Sera hii ya Polisi Jamii, msingi mkubwa ni kuweka utaratibu mzuri wa kuwa na Polisi Jamii ili tuweze kupambana na uhalifu nchini na tuendelee sote kuwa katika hali nzuri katika maisha yetu.

Kuhusu suala la udhibiti wa uingizaji wa silaha haramu ambalo pia limechangiwa na Waheshimiwa Wabunge hao, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola linaendelea kudhibiti uingiaji holela wa silaha toka nchi jirani kwa kuimarisha ulinzi wa maeneo ya mipakani na kuendesha misako ya mara kwa mara ndani ya nchi na wakati mwingine kuendesha *operation* za pamoja na nchi jirani.

Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia alitaka kupunguza msongamano wa magari Dar es Salaam na kwingine na alizungumzia pia suala la utaratibu wa suala la njia tatu. Suala la njia tatu linatumika kimataifa na kwa kweli limesaidia sana kwa hiyo tuendelee kuliunga mkono Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote, nchi kama Amerika ya kusini na *Scandnavian Contries* wanatumia utaratibu huo, kwa hiyo utaratibu huo ni mzuri, tuendelee kuunga mkono huku tukitafuta suluhisho la kudumu kwenye suala la msongamano wa magari.

Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele alisema kwamba Serikali iongeze nguvu katika kukabili tatizo la Wasomali katika Wilaya ya Ngorongoro. Ili kukabiliana na tatizo la wahalifu Wilayani Ngorongoro Serikali inaendesha *operation* za mara kwa mara kwa kuwashirikisha wananchi wa Wilaya hiyo ili kuwabaini wahalifu hao na kuwachukulia hatua za kisheria na Mheshimiwa Telele ni shahidi, ameona kidogo imeanza kupungua hali hiyo na tutazidisha nguvu kuhakikisha kwamba hali iwe shwari zaidi.

Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Abdallah Salim Sumry walisema kwamba vituo vya polisi mipakani viimarishwe na kuongeza Askari na vifaa. Ushauri tunaupokea na tunawahakikishia kwamba kadri hali itakavyokuwa nzuri kifedha tutayashughulikia masuala haya kwa ukarimu wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Kaika Saning'o Telele amezungumzia juu ya utaratibu wa kumiliki silaha kwa watu binafsi. Suala la kumiliki silaha watu binafsi linahitaji kufanyika kwa umakini wa hali ya juu kwa sababu ya hatari ya matumizi mabaya yanayoweza kufanywa kwa silaha hizo. Utaratibu uliopo sasa hivi wa kumilikisha watu binafsi silaha una lengo la kuhakikisha kwamba wale wanaomilikishwa silaha ni watu waaminifu na wasiotarajiwa kuzitumia silaha hizo kinyume na sheria. Kwa hivi sasa, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau linafanya tathmini ya utaratibu huu kwa lengo la kubaini kama yapo mapungufu ili iweze kurekebishwa tuwe na utaratibu ulio mzuri zaidi.

Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mheshimiwa Dr. Diodorus Buberwa Kamala, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanywa na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan walizungumzia suala la ulinzi kwenye Maziwa na Bahari. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Idara nyingine za Serikali limekuwa likifanya doria za nchi kavu na majini kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika maziwa na bahari.

Aidha, hatua nyingine zilizochukuliwa na Jeshi la Polisi ni pamoja na kukarabati mashua na doria katika maziwa ya Tanganyika, Nyasa na Victoria. Bado jitihada hizi zinaendelea na hivi karibuni mlimsikia Mheshimiwa Rais wetu alivyolivalia njuga suala

hili na tayari ametuagiza kulifanyia kazi kwa ukaribu zaidi. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tutashirikiana kufanya kazi hii kwa ukamilifu kuhakikisha maisha ya wananchi wetu hawa waliopo katika Kanda ya Ziwa yanakuwa salama.

Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Juma Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar walisema Askari wajengewe nyumba kwenye Makambi yao na mishahara yao iboreshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema awali, ni kwamba kuna maboresho makubwa katika Jeshi la Polisi yanafanywa kwa nia hiyo hiyo ya kuimarisha mishahara ya Askari wetu, kuimarisha ujenzi ya nyumba mbalimbali za Polisi, Vituo vya Polisi na kadhalika. Kama nilivyosema awali, tunaomba subira zenu Waheshimiwa Wabunge, wakati tunashughulikia jambo hili nia yetu ni kuhakikisha kwamba Askari wetu wanaishi mahali pazuri na kuondoa matatizo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tumeanza kwa kushirikiana na *NSSF,* tunajenga hayo maghorofa 30, lakini nia yetu ni kuendelea zaidi na zaidi na kadri ya uwezo wa Serikali utakavyowezekana katika bajeti ya Serikali tutaongeza ujenzi wa nyumba za Askari pamoja na Vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan yeye alitaka Jeshi la Polisi liache kuwanyanyasa wachuuzi wa bidhaa ndogondogo. Kazi ya kuondoa wachuuzi wa bidhaa ndogondogo katika mitaa ya miji hapa nchini haifanywi na Jeshi la Polisi, kazi hii hufanywa na Halmashauri za Miji inayohusika wakiwa katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Halmashauri hizo. Askari wanaotumiwa ni Mgambo ambao ni waajiriwa wa Halmashauri hizo. Hata hivyo, Jeshi la Polisi hutumika ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa kazi hizi unazingatia Sheria za Halmashauri na unafanyika kwa usalama.

Ili kuboresha utendaji katika eneo hili, Serikali imeshatoa kibali kwa Halmashauri zote nchini cha kuajiri Polisi Wasaidizi yaani *Auxiliary Police* ambao utendaji wao unazingatia Sheria na kuheshimu haki za binadamu. Jeshi la Polisi kwa upande wake linakamilisha mchakato wa kuandaa kanuni za kuratibu na kusimamia utendaji wa Polisi Wasaidizi ili kuhakikisha kwamba wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, tutafanya kila liwezekanalo kuondoa kabisa tatizo lolote lile ambalo linakwenda kinyume na taratibu za Sheria.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan kwamba Serikali inayoongozwa na CCM siku zote haiwanyanyasi wananchi na itachukua kila jitihada kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanaishi vizuri na maisha mazuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Sijapata Fadhil Nkayamba, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Athumani Ngwilizi, Mheshimiwa Capt. George Huruma Mkuchika, Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond na Mheshimiwa Grace Sindato Kiwelu

wanataka kujua mikakati ya Serikali ya kupunguza ajali za barabarani. Tatizo la ajali za barabarani linatokana na sababu mbalimbali na utatuzi wake unahusisha wadau mbalimbali pia. Jeshi la Polisi kwa upande wake limekuwa likichukua hatua mbalimbali ili kudhibiti ongezeko la ajali mbalimbali.

Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kufanya doria kwenye barabara kuu, kuwatumia Askari wanaovaa kiraia kubaini makosa mbalimbali ya usalama barabarani, kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari, kuendesha Semina Elekezi kwa Watendaji wa Kitengo cha Usalama Barabarani ili kuwaongezea uwezo wa kusimamia Sheria ya Usalama Barabarani. Uhakiki wa leseni za kuendesha magari, pamoja na kusimamia utaratibu wa ratiba za magari wa kila Kituo, haya yote yanafanyika kwa nia ya kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vitendea kazi, waliochangia ni wafuatao: Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Prof. Philemon Sarungi, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu na Mheshimiwa Herbert Mntangi.*(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Wote wamechangia katika hoja ya vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, Wizara inatambua tatizo la vitendea kazi yakiwemo magari, pikipiki na vifaa vingine kama mashua za doria, vifaa vya mawasiliano na kadhalika.

Hatua mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuendelea kuishauri Serikali kuboresha bajeti ya Wizara, kutumia vyanzo mbalimbali vya wafadhili kama vile Programu ya Maboresha ya Sekta ya Sheria, Mashirika ya Kimataifa kama vile *UNDP* na nchi rafiki.

Aidha, ni mpango wa Wizara kuhakikisha kwamba kila Kituo cha Polisi kinapatiwa pikipiki na hili litatekelezwa kadri bajeti itakavyoendelea kuboreshwa. Tatizo letu kubwa kabisa Waheshimiwa Wabunge, ni tatizo la kiuchumi ambalo wote tunalielewa ndiyo hali yetu tuliyonayo, inabidi kidogo kilichopo tugawane kidogo

kidogo kwa kila Sekta. Lakini nia yetu ni kuwa na vifaa vya kutosha katika Jeshi la Polisi ili liweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge watuvumilie wakati tunatafuta njia za kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wafuatao wamechangia kuhusu Vituo vya Polisi na makazi ya Askari Polisi. Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Balozi Abdi, Mshangama, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Masolwa Cosma Masolwa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Herbert James Mntangi na Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Capt. John Chiligati, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Abdallah Sumry na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa makazi, Serikali inatarajia kama nilivyosema awali kujenga maghorofa 30. Kwa upande wa Tanzania Bara itakuwa maghorofa 25 na upande wa Tanzania Zanzibar yatakuwa maghorofa matano kwa kuanzia. Lakini kama nilivyosema, jitihada zinachukuliwa kuimarisha eneo hilo. Jitihada nyingine zinachukuliwa za kukarabati majengo mbalimbali ya Askari Polisi na kadhalika. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kuvumiliana wakati tukichukua hatua hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna Waheshimiwa Wabunge wengine wamechangia katika eneo hilo hilo. Kwa ruhusa yako napenda niwataje. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Hemed Mohamed Hemed, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Frorence Kyendesya, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maslahi ya Askari Polisi. Waheshimiwa Wabunge wafuatao wamechangia katika hoja hii. Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Dorah Mushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa uingiaji wa silaha na uhalifu mipakani, hoja hii pia ilichangiwa na Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Dorah Mushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Polisi litaendelea kudhibiti uingiaji holela wa silaha na wahalifu kutoka nchi jirani kwa kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya mipaka na kuendesha misako ya mara kwa mara ya ndani ya nchi na wakati mwingine kuendesha *operation* za pamoja kama nilivyosema awali. Aidha, Jeshi la Polisi linaendeleza juhudi za makusudi za kuimarisha ushirikiano wa Majeshi ya Polisi ya nchi jirani ili kurahisisha ubadilishaji wa taarifa za wahalifu na uhalifu. Ushirikiano huo unafanywa kwa kupitia mashirikisho ya Kipolisi ya *Inter-Pool, SAPCO* na *YAPCO.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujambazi kwenye Maziwa alizungumzia Mheshimiwa Paul Kimiti na kama nilivyolieleza mwanzo ni kwamba, jitihada zinachukuliwa kuimarisha vitendea katika eneo hilo. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge watuwie radhi na pia Jackson Makwetta alizungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mafunzo ya Askari na uboreshaji wa Vyuo vya Polisi ni Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoelezwa katika hotuba ya bajeti katika ukurasa wa 16, mafunzo yataendelea kutolewa ndani na nje ya nchi ili kuimarisha taaluma za Askari Polisi. Aidha, Serikali inachukua hatua za kupanua na kukarabati Vyuo vya Polisi vilivyopo na tunatarajia kukarabati Chuo cha *TANESCO* cha Kidatu kama nilivyosema mwanzo kwa ajili ya suala la *CID* pamoja na kujenga Chuo cha Upelelezi hapa Dodoma. Aidha, taratibu zinaendelea kuchukuliwa za kuimarisha utaratibu wa mafunzo kazini pamoja na kuendesha semina mbalimbali ili kuwajengea Askari uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza. Mafunzo hayo pia yatazingatia mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la upungufu wa Askari Polisi, limechangiwa na Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na Mheshimiwa Rosemary Kirigini pamoja na Mheshimiwa Savelina Mwijage. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa Askari Polisi, Serikali imeendelea kutoa kibali cha kuajiri Askari Polisi wapya kila mwaka. Mwaka 2007 Serikali ilitoa kibali cha uajiri Askari Polisi wapya 2,611. Vilevile Wizara

imekamilisha tathmini na taratibu za kuandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri zimeanza kuchukuliwa ili kuwasilisha Serikalini mapendekezo ya kuongeza umri wa kustaafu Askari wa kawaida ambao ni miaka 45 kuwa miaka 50. Kama hatua ya dharura, Serikali imewaongezea Mkataba wa kazi jumla ya Askari 521, ambao walikuwa wastaafu kwa mujibu wa Sheria mwaka huu, sasa wataendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ajali za barabarani kama nilivyowataja Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hiyo na nilishaeleza hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa na tutazidi kusimamia vizuri sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la madeni ya Askari Polisi, lilizungumziwa na Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Maida Abdallah na Mheshimiwa Mwanakhamisi Kassim Said.

Malimbikizo ya madeni ya Askari Polisi na wazabuni ya muda mrefu ni kero kubwa kwa Askari Polisi na wazabuni. Katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali ilitenga shilingi bilioni 8.5 kwa ajili ya kulipa madeni ya Askari Polisi. Kuanzia mwaka 2001 hadi Juni, 2005 madeni hayo yalihakikiwa na jumla ya shilingi bilioni 5.4 zilionekana ndiyo madeni halali. Hadi kufikia mwezi Mei, 2007 madeni hayo yalikuwa yamelipwa kwa Askari Polisi wanaohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Wizara bado inaendelea kukabiliwa na malimbikizo ya madeni ya Askari Polisi ya kipindi cha kuanzia Julai, 2005 hadi sasa yanayofikia shilingi bilioni nne na yale ya wazabuni kuanzia mwaka 2001 hadi sasa yaliyofikia shilingi bilioni 11. Wizara itaendelea kuwasiliana na Hazina ili madeni hayo yaweze kulipwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala kuhusu mafao ya Askari Polisi wastaafu na wanaofariki. Hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Kiumbwa Makame Mbaraka, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Fatma Othman Ali Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa na Mheshimiwa Savelina Mwijage.

Mafao ya kustaafu hulipwa kutegemea na kiwango cha mshahara wa mtumishi anayehusika na miaka ya utumishi wake. Kwa sasa hivi wastaafu wa Polisi hulipwa mafao kidogo kwa sababu mishahara yao ni midogo. Hata hivyo, Wizara imeandaa mapendekezo ya maboresho ya mishahara ya Askari Polisi na kuwasilishwa kwenye Tume Maalum ya Taifa ya kushughulikia maslahi ya watumishi wote wa Serikali. Hivyo, inatarajiwa kwamba baada ya mishahara kuboreshwa, mafao ya wastaafu pia yatakuwa yameboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ucheleweshaji wa mafao ya Askari Polisi wanaofariki, ndugu wa Marehemu wanahimizwa kukamilisha mapema taratibu za mirathi ili malipo yao yaweze kufanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ajira na upandishwaji vyeo, hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji,

Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Mwaka Ramadhan, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis na Mheshimiwa Issa Kassim Issa. Ili kuboresha taratibu za ajira na upandishwaji wa vyeo kwa Askari Polisi, Wizara ya Usalama wa Raia kwa kushirikiana na Mshauri Mwelekezaji imeanza mchakato wa kuandaa taratibu hizo ambazo zitaweka bayana utaratibu wa ajira na upandishwaji wa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maafisa wa Polisi wanaofanya kazi Bungeni ni Askari Polisi ambao wapo chini ya Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Dodoma. Taratibu zao za upandishwaji wa vyeo zinafuata taratibu na kanuni zilizopo.

Waheshimiwa Wabunge, inawezekana mkawaona hapa, hawakuvaa vyeo vyao kwenye mabega, lakini wanavyo vyeo na wanalipwa mishahara yao kufuatana na vyeo walivyonavyo. Kwa sababu ya taratibu za hapa, hawawezi kuvaa vyeo; kwa kuwa tena kuna Spika na wengine mambo yatakuwa magumu kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ucheleweshwaji wa kesi, hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Florence Kyendesya. Wizara yangu imejipanga kikamilifu kuondoa tatizo la ucheleweshaji wa upelelezi wa kesi. Wizara imeunda Kamati Maalum, *Task Force* ya wataalam kutoka Makao Makuu ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai ili kuchunguza malalamiko ya ucheleweshaji upelelezaji wa kesi na kuchukua hatua za haraka kurekebisha dosari zitakazobainika. Kazi hiyo inaendelea kufanyika kwa wataalam hao, kutembelea Mikoa yote nchini na kufanya ukaguzi wa kesi za siku nyingi ambazo zipo Mahakamani. Zoezi hilo linaendelea vizuri na litakuwa ni la kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tatizo la dawa za kulevya, hili limechangiwa na Mheshimiwa Yono Kevela, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na Mheshimiwa Fatma Maghimbi. Tatizo la dawa za kulevya limeendelea kuwa changamoto si tu kwa nchi yetu pekee, bali kwa nchi zote duniani.

Hivi sasa Tanzania imeongeza juhudi zaidi za kupambana na tatizo hilo. Kutokana na juhudi hizo, mwaka 2006 jumla ya matukio 5,532 ya madawa ya kulevya yameshughulikiwa na Polisi ambapo jumla ya kilo 225,372 za madawa mbalimbali zilikamatwa. Vilevile watuhumiwa 7,194 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uhamisho wa Askari wa Usalama Barabarani, hoja hii imechangiwa na Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Joyce Martin Masunga. Ushauri umezingatiwa. Hatua zitaendelea kuchukuliwa bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la ubambikizaji kesi, ni hoja iliyochangiwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Mwaka Ramadhani na Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Kwa sasa hivi Jeshi la Polisi, liko

katika mchakato wa kufanyia maboresho ambapo tatizo la ubambikizaji kesi na utendaji wenye ufanisi ni mambo yatakayopewa umuhimu wa pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kengele ya kwanza imegonga na muda uliobaki ni mdogo, ningeomba vilevile niende kwa haraka haraka nijibu masuala mengine yafuatayo:-

Kuhusu suala la Mheshimiwa Kabwe Zitto la madai ya Askari Polisi Kigoma waliompiga mwananchi Emmanuel Nyamusizi na kumuumiza, alitaka alipwe fidia pamoja na kupata matibabu na kuchukuliwa hatua wahusika. Jambo hili linafanyiwa utafiti wa kina na wataalam kutoka Makao Makuu ya Polisi kisha hatua zitachukuliwa kwa watakaobainika kuhusika. Mheshimiwa Mbunge, atajulishwa matokeo hayo. Kwa sasa inabidi iundwe timu maalum inayoongozwa na *DCI* kuchunguza jambo hilo kuhusu ukweli wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vilevile nijibu suala la Mheshimiwa Laus Mhina kuhusu Askari Trafiki kusimamisha magari mara kwa mara. Askari Trafiki wameelimishwa juu ya jambo hilo na sasa hivi naona limepungua sana. Wanachukua zile hatua za dharura pale wanapoona panahitaji kufanyika hivyo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba waungane nasi katika suala hilo kwa sababu mnaona ajali nyingi zinazotokea za barabarani. Kwa hiyo, kufanya vile pia ni kupunguza ajali za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa alizungumzia kufukuzwa kazi kwa Askari Polisi *D. 2678 PC* Khamis Ali. Uchunguzi uliofanyika umebaini kwamba Askari Polisi huyo alifukuzwa kazi halali na kwa mujibu wa taratibu. Hivyo, Mheshimiwa Mbunge, naomba akubaliane na utaratibu wa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Mfuko wa Bima ya Afya, Wizara inakamilisha mchakato kama nilivyosema awali na mapendekezo ya kuwajumuisha Askari Polisi kwenye Mfuko wa Bima ya Afya unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anna Komu naye alitaka wachukuliwe hatua Askari wanaopewa taarifa kuhusu wahalifu. Kama nilivyokwishasema, hili jambo tunalishughulikia na nataka niwahakikishie kwamba Askari wetu wanafanya kazi nzuri kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa muda niliopewa umekwisha na nina uhakika mengi nimejaribu kuyajibu na Mheshimiwa Waziri atakuja kuyajibu mengi zaidi, kwa hiyo, naomba kama nilivyosema awali mtuvumilie, mtupitishie Bajeti yetu hii vizuri ili mtuunge mkono tuweze kufanya kazi zetu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu Naibu Waziri amezungumza kwa muda mrefu, Waziri mwenyewe atazungumza kwa muda wa dakika 20.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa hekima na busara zako kubwa katika kuliongoza Bunge letu. Jambo hili linadhihirisha kuwa dada zetu nao wana uwezo mkubwa katika uongozi iwapo watautafuta na wakipewa nafasi. *(Makofi)*

Pili, nakushukuru kwa fursa hii uliyonipa ya kujibu baadhi ya hoja. Hoja nyingi zimekwishajibiwa na Naibu Waziri. Kwa hiyo, nitakachofanya ni kufanya majumuisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed kwa ufafanuzi mzuri na maelezo ya kina na fasaha aliyoyatoa katika kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Namshukuru na kumpongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa ushauri na maelekezo fasaha waliyotupa na namna tunavyosaidiana katika utendaji kazi wetu wa kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yao tumeizingatia, niseme tu kwamba yote ambayo wameyazungumza tutayafanyia kazi; na kwa kuwa tunakutana mara kwa mara, basi kwa leo sina haja ya kujibu hoja hizo, lakini niahidi kwamba masuala hayo tutayafanyia kazi na kutoa ripoti kila wakati tunapokutana.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumshukuru kwa dhati rafiki yangu Mheshimiwa Ibrahim Sanya ambaye pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Ulinzi. Namshukuru sana kwa mchango wake mzuri na changamoto mbalimbali alizotupa siku zote. Maoni na ushauri wake tutaufanyia kazi kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango mizuri waliyoitoa kwa kuzungumza na kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yote imetolewa kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wetu. Napenda kuahidi kuwa maoni, ushauri, maelekezo na changamoto zote walizotupa tunazithamini sana na tutazifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa *concerns* walizotoa zenye lengo la kuleta amani, usalama na utulivu nchini. Nawashukuru sana kwa pongezi walizotoa na uzalendo mkubwa waliouonyesha katika michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kwa heshima na taadhima niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi na waliochangia wakati wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Ibrahim Sanya, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Laus Mhina, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Abdallah Sumry, Mheshimiwa, Savelina Mwijage, Mheshimiwa Faida Bakar na Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Anna Komu, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa George Malima. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Yono Kevela, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir Mheshimiwa, Adam Kimwanga, Mheshimiwa Luka Siyame, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Aloyce Kimaro, Mheshimiwa Hamad Mohamed, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Rajab Juma, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Azzan Zungu, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Omar Ali Mzee na Mheshimiwa Capt. John Chiligati. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Mwaka Radhaman, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Vuai Khamis na Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Juma Omar, Mheshimiwa Salim Khamis, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, Mheshimiwa Mwanajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan na Mheshimiwa Salome Mbatia. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Zubeir Maulid, Mheshimiwa Mwanakhamis Said, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Musa Emmanuel, Mheshimiwa Savelina Mwijage,

Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Florence Kyendesya, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Mheshimiwa Kiumbwa Mbarak, Mheshimiwa Joyce Martin Masunga, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Fatma Othman Ali, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Riziki Omar Juma na Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Athumani Janguo na Mheshimiwa Dr. Ali Tarab Ali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, waliochangia kupitia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Siraju Kaboyonga, Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Ania Chaurembo, Mheshimiwa Sijapata Nkayamba, Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, Mheshimiwa Capt. George Mkuchika, Mheshimiwa Idd Azzan, Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Grace Kiwelu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Uraia kwa majibu mazuri aliyotoa kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Nami pia kwa muda mchache nilionao nitajaribu kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla tu kuelezea masuala ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri amekwishayapitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kupitia Bunge lako Tukufu kutambua kazi kubwa inayofanywa na Jeshi la Polisi katika mazingira magumu ya ukosefu wa makazi, ofisi, vitendea kazi mbalimbali muhimu, upungufu wa Askari Polisi na matatizo mengine mengi.

Kama sote tunavyofahamu, kazi ya Polisi ni kazi ngumu yenye hatari nyingi ambayo Askari Polisi wanatakiwa kufanya kazi kwa saa 24 kila siku bila kupumzika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Askari wetu wanafanya kazi zao kwa bidii, moyo wa kujituma bila kuchoka.

Nawapongeza sana Askari Polisi wote nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kudumisha amani, usalama na utulivu ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio ambayo Jeshi la Polisi limeyapata kwa kiasi kikubwa yametokana na ushirikiano mkubwa tunaopata kutoka kwa raia wema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wote wanaotoa taarifa Polisi. Ni kutokana na taarifa zao za siri ndiyo Jeshi la Polisi limeweza kuwakamata wahalifu katika maeneo mbalimbali nchini likiwemo la Mkoani Arusha hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi letu la Polisi ni Jeshi la siku nyingi, muundo wake, mfumo, sheria, kanuni na taratibu zake baadhi zimepitwa na wakati. Kwa kutambua hilo, hivi sasa tuko katika kulifanyia maboresho makubwa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na kuzipitia upya sheria na kanuni za Jeshi hilo ili ziendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, programu ya maboresho tumeanza mchakato wake ikizingatia maeneo matatu kama nilivyoyataja asubuhi ya leo. Kwanza, kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa, hii ni katika kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi vya kisasa, ofisi na makazi ya kisasa.

Pia kuwa na mbinu na mikakati ya kisasa; Pili, kuimarisha taaluma katika Jeshi la Polisi; kufuata taaluma katika ajira, mafunzo, kutofuata itikadi ya Vyama, kuwa *integrity* ndani ya Jeshi la Polisi, kuwa na maadili safi ndani ya Jeshi la Polisi; suala la tatu, ni kuimarisha utaratibu wa Polisi Jamii. Hili ni kuwashirikisha kikamilifu wananchi katika maamuzi yanayohusu ulinzi na usalama katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo mbinu na mikakati mingi ya kuhakikisha kuwa Jeshi letu la Polisi linatekeleza wajibu wake kwa tija na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mbinu na mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha kazi ya upelelezi ili kuzuia uhalifu kabla haujatokea kwani kinga ni bora kuliko tiba;

(ii) Kufanya operesheni za pamoja na vyombo vingine vya Dola vya ndani na nje ya nchi na hasa maeneo ya mipakani;

(iii) Kuimairisha doria za miguu, magari na pikipiki;

(iv) Kuimarisha kikosi cha Polisi Wanamaji na kufanya doria katika bahari na maziwa kwa kushirikiana na taasisi nyingine;

*(v)* *IGP* kutoa maelekezo kwa njia mbalimbali kwa Makamanda wa Mikoa na Vikosi vyote nchini ili kuboresha utendaji kazi wao; na

(vi) Viongozi wa Mikoa na vikosi kufanya kazi kwa karibu zaidi na watendaji wao kuwa wabunifu na kusimamia kwa karibu zaidi shughuli zote katika mikoa yao na vikosi vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi sana na zimegusa maeneo mbalimbali. Baadhi ya hoja hizo zilihusu sera mbalimbali

kulifanya Jeshi la Polisi kuwa la kisasa, kulipatia Jeshi la Polisi vitendea kazi, kuboresha maslahi ya askari, kuboresha makazi ya askari, ujenzi wa Vituo vya Polisi, utaratibu wa bakhshishi na pensheni, utaratibu wa ajira na upandishwaji vyeo, mafao ya askari wastaafu, masuala ya usalama barabarani, ujambazi kwenye maziwa na bahari, tatizo la kubambikiza kesi na tatizo la dawa za kulevya.

Hata hivyo, kilichojitokeza kati ya michango ya maeneo haya kwa jinsi mlivyotafsiri sio shutuma ni utendaji kazi wa Jeshi la Polisi, bali haya yote yamelenga kutoa ushauri na mapendekezo ya namna Jeshi linavyoweza kuboreshwa zaidi ili utendaji kazi wake uwe wa tija na ufanisi. Utendaji wenye nia ya kuwajibika kwa wananchi na kuhakikisha kwamba amani, usalama na utulivu, vinadumishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, amejitahidi kwa kiasi kikubwa kujibu hoja hizo hivyo, mimi niseme tu kwamba, fikra, mawazo na michango ya Waheshimiwa Wabunge, nimezipokea kwa mikono miwili na pindi mkutano huu wa Bunge utakapomalizika, natarajia kuitisha mkutano wa Maafisa wa Wizara, Jeshi la Polisi, wataalam waelekezi, kwa maana *consultancy* na wengine ili kuyafanyia tathmini masuala yote hayo na kuyatafutia nafasi mahsusi katika zoezi zima la programu ya kuboresha Jeshi la Polisi, kwa maana ya *Police Reform Programme.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, hoja hizi mbalimbali tutazitolea majibu kwa maandishi. Aidha, tutaandaa ratiba ya kuyatembelea Majimbo ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kadri tutakavyoweza, mimi binafsi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *IGP* na Makamishna wake, kwa nia ya kutambua matatizo yaliyopo. Kwa msingi huo kuweza kuzungumza mapema na wenzetu wa Wizara ya Mipango na Wizara ya Fedha kabla ya bajeti ya mwaka kesho kuandaliwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya Jeshi la Polisi katika bajeti ya mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 28 – Wizara ya Usalama wa Raia**

Kif. 1001 – *Adminstration and General* …………….. Sh. 2,626,160, 200

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Programu ya 10, *Subvote* 1001 – *Administration and General*, Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina suala moja tu ambalo nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi wa kina. Kwanza, nashukuru kwa kuunda Kamati kwa ajili ya kijana ambaye alipigwa katika Kijiji cha Mtigo kule Kigoma. Lakini katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Usalama wa Raia, kuhusiana na suala la mtoto Mariam Fariji, amezungumzia kuhusu kutafutwa kwa mtuhumiwa kwa ajili ya kuweza kukamatwa na kwamba ameshirikiana na Polisi wa *Interpol*. Lakini licha ya kwamba huyu mtuhumiwa anapaswa kutafutwa, jambo la msingi zaidi ambalo ni jukumu la Serikali katika ulinzi wa raia ni kuhakikisha kwamba, mtoto huyu wa Kitanzania anapatikana haraka iwezekanavyo, kurudishwa nyumbani na kuungana na familia yake.

Naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ni juhudi gani ambazo zinafanyika mpaka sasa kuhakikisha kwamba, Mariam anarudi nyumbani na kuungana na familia yake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**MWENYEKITI:** Nakubali lakini kama ulikuwepo alipokuwa anajibu, nadhani alimuahidi aliyezungumza, Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya kwamba, wanaendelea na wakati muafaka wakipata taarifa za kutosha, watatoa taarifa rasmi. Nadhani hiyo alisema kwa sababu hivyo ndivyo nilivyosikia na kwa hiyo sidhani kama kuna taarifa rasmi zaidi ya hiyo, labda kama mnazo.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumzia kutafutwa kwa mtuhumiwa, hajazungumzia kutafutwa kwa mtoto wa Kitanzania ambaye amepotea. Ndiyo jibu ambalo nalitaka na mimi nilisikiliza vilevile.

**MWENYEKITI:** Tulivyosikia wote tulidhani tunatafuta huyo mtoto. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, kama unayo majibu?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linahusu pande mbili. Kuna upande wa huyo Mariam na kuna upande wa huyo ambaye amemtorosha. Sasa jitihada bado zinaendelea, taarifa ambayo tumeipatapata mpaka sasa hivi inaonesha kwamba, pengine yupo Uganda au South Africa. Bado tunaendelea na jitihada hizo sote wawili.

**MWENYEKITI:** Mimi nilielewa kwa *interest* ya sisi Watanzania, mtoto wetu, ndiyo hicho alichokuwa anajibu, unafikiri alikuwa anajibu kitu kingine zaidi ya hicho?. Kwa sababu hata Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya mwenyewe alizungumzia habari ya mtoto, kwa hiyo, nadhani tunaelewana. Tunaendelea.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru *Vote 28*, Programmu ya 10, *Subvote* 1001, kifungu 250100 – *Basic Salary.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni la kisera tu. Katika mchango wangu wa maandishi niliulizia kuhusu mfumo dume uliopo katika Jeshi letu la Polisi. Hata

ulipokuwa unatujulisha wageni hapa asubuhi, umeona mwanamke hapa alikuwa ni mmoja tu. Katika tafiti zangu, nimeona Makamishna karibu wote ni wanaume. Sasa ningependa kujua kwamba, hili Jeshi la Polisi, huu mfumo dume ulipangwa makusudi au imetokea tu? Kwa sababu naamini kabisa kuna wanawake wenye uwezo wa kupata hizo nafasi za juu. Nafikiri kwa kuanzia tu wawepo hata *Deputy Commissioners*. Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Lucy F. Owenya kwamba, mpaka sasa hivi idadi ya askari wanaume ni kubwa sana na ni suala la kihistoria. Kuna kazi ambazo wanazifanya wanawake kwa urahisi na kuna kazi nyingine ni za sulubu, maana hata katika malindo yetu katika maeneo mbalimbali usiku si utaratibu kuwa na askari mwanamke wakati ule. Inaweza kuleta madhara makubwa sana na tusingependa kuwaweka wanawake katika hali hiyo. Lakini zaidi ya hayo ni kwamba, katika hayo maboresho ambayo tuko njiani kuyafanyia kazi, suala hilo pia tutalitazama.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, jibu sahihi ni historia tu basi. Kwa mujibu wa kifungu 126, naomba msirudie hiki kifungu nimeshawaelewa mko hapa wote, kwa hiyo endeleeni tu.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea moja kwa moja. Katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea kwamba, kuna askari wawili kwa upande wangu, ambao wako katika jimbo langu; kuna Z2504 Serjeant Salum Hassan, kwa muda mrefu anasumbuka kwenda Dar es Salaam na anafikia kiwango hata nauli anakosa na akija kule kwa kweli hapati mafanikio ya aina yoyote. Hali kadhalika kuna Ndugu Hamad Faki Khamis E7315, mwaka 2001 hadi 2004 kuna askari walilipwa kutokana na uhamisho yeye alikuwa Pemba kwa bahati akaletwa Mkoa wa Kusini Unguja. Lakini kwa upande wake hakuweza kufanikiwa kupata haki yake ya uhamisho. Sasa nilikuwa napenda kupata maelezo ili niweze kujua namna gani nitawajibu hao kwa sababu nimetumwa. Asante sana.

**MWENYEKITI:** Kuna sehemu uliandika hii? Umesema uliandika, iko kwenye maandishi, kama haipo hii Mawaziri wanafanya sera tu sio majina ya askari wote.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Niliandika.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwenye mchango wake wa maandishi sikuona haya ambayo sasa hivi anatueleza. Lakini kama lipo tatizo hilo, nia yetu ni kutatua matatizo mbalimbali ya askari wetu kwenye Wizara, namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kikao hiki, tukutane tutafute ufumbuzi juu ya tatizo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, tunaomba upeleke majina hayo ili waweze kuyaangalia. Waziri ni Waziri wa Sera hawezi kujibu majina. Kwa hiyo, upeleke kwa maandishi majina ya hao jamaa zako. Tuko wote?

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashangaa sana kwa sababu …

**MWENYEKITI:** Sema ndio bwana!

**MHE YAHYA KASSIM ISSA:** Kwa sababu wao karatasi wanazo hapo. Kama wanazo yeyote aliyekuwa na karatasi yangu aangalie Yahya Kassim Issa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, asante sana. Naomba ukae chini basi. Sasa nakuagiza kwamba, upeleke kwa maandishi tena kwa majina uliyoyataja kusudi wakutafutie maelezo yaliyo sahihi.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nipo katika *Vote* hiyo hiyo ya 28, Programu ya 10, *Subvote* 1001, *item* 250100 – Mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi na katika kuchangia kwangu, nilizungumzia juu ya uhitaji wa Kituo cha Polisi katika eneo la Kata ya Tulia, Doromoni, ambako kuna shughuli za kibiashara zinazofanyika pale, zinaendeshwa na wafanyabiashara na wavuvi wa samaki wa Ziwa Kitangiri. Hili niliwahi kuliongelea mwaka jana, tunahitaji sana Kituo cha Polisi. Kwa hiyo, niliomba katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri, anijibu wana mpango gani wa kuweza kuanzisha kituo pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilizungumzia kuhusiana na suala la mabasi ya abiria. Utaratibu ambao tulikubaliana ni kwamba, mabasi ya abiria yaende mwisho saa 4:00, lakini mabasi yanayotoka Mwanza kwenda Dar es Salaam, mimi nimetoka Dar es Salaam saa 4:30 usiku, nilikuwa nakuja hapa Dodoma, nilikutana na mabasi ya *Mohamed Trans,* Zuberi, *Super Najimunisa* usiku wa saa 4:45 na kwa bahati nzuri wakati nakuja mbele nikakuta askari wa doria wapo na nilisimama nikaongea nao, nikawauliza mabasi haya kwa nini yameruhusiwa na yanaendelea na safari? Hakuna jibu nililopewa! Sasa nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anieleze; je, huu utaratibu bado upo na kama mabasi yanaendelea basi atueleze Bunge hili Tukufu kwamba huu utaratibu unaendelea na iwe kwa nchi nzima? Lakini yapo mabasi yanaendelea na *Mohamed Trans* ndiyo hilo lililoua abiria wengi Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Juma H. Killimbah, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la Kituo cha Polisi cha Tulia ni kwamba, kama tunavyojibu maswali mara nyingi hapa Bungeni, tumeeleza kwamba, tulikuwa tunafanya tathmini ya kina kujua mahali gani panahitajika vituo kwa mujibu wa vigezo vya Polisi. Hivi sasa tathmini hiyo imemalizika na katika maelezo yangu hapa nimesema, hatua inayofuata ni kujenga vituo hatua kwa hatua, kadri uwezo utakapopatikana. Suala hili tutaliangalia,

unajua nia yetu kwako ni nzuri, kwa hiyo, naomba utupe muda tutafute ufumbuzi suala hili.

Kuhusu suala la mabasi kutembea usiku ni marufuku kwa mabasi kutembea usiku zaidi ya saa 4:00 na natoa agizo hili kwa askari wote, kuchukua hatua za ziada kuhakikisha kwamba, hakuna mabasi yanayotembea usiku baada ya saa 4:00.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea tatizo la ujambazi Ziwa Tanganyika. Mheshimiwa Waziri, amejitahidi kujibu lakini kuna suala moja naona ameliruka. Pamoja na wavuvi kuibiwa mali zao, kumekuwa na utaratibu wa wao wenyewe kuchanga mafuta kwa ajili ya boti la Polisi. Katika kila mwezi wanavua siku 22, kwa hiyo, kila siku anatakiwa mwenye chombo atoe lita tano. Kwa hiyo, ina maana mara 22 ni kama lita 110 kila usiku wanapovua. Sasa wamechoka na hali hiyo wanasema kwamba, wanaiomba Serikali ichukue jukumu lake, kwa sababu ni kazi ya Serikali kuwalinda.

Tunaomba ufafanuzi; je, Serikali itachukua jukumu hilo au waendelee kuchangia mafuta? Asante.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, naomba kumjibu Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, kama ifuatavyo: Siku zote jukumu la Serikali ni kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao na kazi hiyo inaendelea kufanywa vizuri. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, sasa tumejipanga upya kupambana na ujambazi huko katika maziwa na baharini. Kwa hiyo, Serikali itaendelea kuchukua jukumu lake hilo na tutahakikisha askari wetu wanafanya kazi ipasavyo kuondoa tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Anauliza kuchangia mafuta.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Kuchangia mafuta hawatochangia. Serikali inachukua jukumu lake, wale wanaokuwa tayari kutusaidia tunawakaribisha, lakini kama hawako tayari, Serikali inachukua jukumu lake.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pogramu hiyo hiyo – Mshahara wa Waziri. Wala sina lengo la kuuzuia, nina lengo la kumtaka atoe haki za watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia hapa, nilizungumzia suala zuri tu la sera ya Wizara hii la kutoa ile posho ya matibabu kama walivyoahidi wenyewe. Tunalotaka kujua hapa ni lini wataanza kuitoa hiyo posho kwa sababu ni kilio kikubwa? Naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Tunaambiwa kuna shilingi laki mbili eti?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, kama ifuatavyo: Kwanza, tulifikiria utaratibu wa shilingi laki mbili, lakini kwa mwaka mzima kwa askari ni fedha ndogo sana kwa ajili ya matibabu. Kwa hiyo, tumekuja na lile wazo kwamba,

askari wetu wawe na Bima na Afya. Suala hilo tayari limeshawasilishwa Serikalini, avute subira kidogo aone matokeo yatakavyokuwa.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Programu hiyo hiyo. Mimi katika kuchangia kwa maandishi na kuzungumza katika mambo mengi niliyochangia, nilizungumzia juu ya Bwana Nkwabi, aliyemtorosha na kumuoa mtoto wa shule. Alikamatwa akiwa na nyara za Serikali na akaachiwa na Mkuu wa Kituo cha Matongo. Baba yake aliyefuatilia kule Wilayani alipofika akakamatwa.

La pili, lilikuwa ni juu ya taa za pale Kituo cha Polisi Iguguno, kiko barabara kuu, wageni kutoka ndani na nje wanapita pale na nguzo iko chini ya mita 15. Ningeomba tu Waziri aniambie juu ya haya. Asante sana.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mgana I. Msindai kama ifuatavyo:-

Kuhusu hili la mtuhumiwa huyu ambaye amesema amekamatwa baada ya kwenda Kituo cha Polisi. Ningeomba atuachie, kwa sababu maelezo niliyoyapata kutoka kwa *RPC* ni kinyume kidogo na hivyo alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, kwa heshima kubwa sana, anipe muda nilifuatilie kwa kina suala hili ili tupate ufumbuzi wa kudumu na suala hilo liondoke kabisa.

Kuhusu taa za Iguguno, kadri ya fedha zitakapopatikana, tutahakikisha kwamba, umeme unakwenda Iguguno. Kwa sababu ni suala la siku nyingi, tunaipa upendeleo maalum.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi. Niliwasilisha mchango wangu kwa maandishi, nashukuru Mheshimiwa Waziri amenitambua na baadhi ya hoja ambazo nilizitoa tangu mapema pia amezijibu. Lakini kuna mambo mawili ambayo nilisubiri majibu sikuyapata na nimeona Mheshimiwa Waziri anisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, niliomba Kamati ilipendekeza kwamba, ratiba za safari za magari yanayokwenda mwendo mrefu zibandikwe kwenye magari. Mimi nikapendekeza na nikashauri kwamba, ratiba ziwe katika tiketi. Kwa mfano, ambao wamesafiri katika mabasi ya Scandnavia unaona tiketi zao. Kule nyuma badala ya kuchora ramani ya picha za magari, wachore ratiba kwamba, gari inatoka Dar es Salaam saa ngapi inafika Morogoro saa ngapi na Dodoma saa ngapi. Vilevile kama inaendelea mpaka Kahama, mpaka Bukoba linafika saa ngapi ili kila abiria aweze ku-*monitor* na tunaposema abiria wasaidie ku-*control* mwendo wa dereva, kila mmoja a-*control* akiwa na ratiba yake, sikupata majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nilichangia kuhusu kukithiri kwa ujambazi katika Mkoa wa Kagera na nikapongeza sana kazi inayofanywa na Serikali.

Nikasema wananchi wa Kagera walisikitishwa kwa kuondolewa Kamanda Tosi na wakaomba kwamba, hawasemi lazima kwamba Kamanda Tosi arudi, lakini ni nani aliandaliwa ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Kagera katika kupambana na ujambazi huu na hata doria linalowekwa halitoshi? Mimi tarehe 7 Juni nilikuwa nakwenda Ngara, nilikutana na gari moja tu wakati wa kurudi kesho yake sikukutana na gari lolote. Sasa hali hii imesababisha ujambazi umeanza tena kushamiri, mbona hili sikupata majibu. Naomba majibu Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Ruth B. Msafiri kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu masuala ya ratiba. Haya ni masuala tulisema tunataka tuyatazame kwa ukamilifu katika ile sera ya usalama barabarani. Kwa hiyo namwomba tuvute subira wakati wenzetu wa Miundombinu wakiufanyia kazi hiyo.

Kuna hili suala pia la kusema kwamba, mabasi yasisafiri baada ya saa 4:00 usiku, hili lina maagizo kutoka kwa Waziri Mkuu kwamba, hili nalo tulifanyie kazi na tutalifanyia kazi. Wenzetu wanapotembea usiku sisi tumelala, nafahamu kuna matatizo yake lakini pia inabidi tulitazame kwa umakini.

Suala la pili kuhusu ujambazi kwamba, tumemwondoa Kamanda Tosi, lakini tumemwondoa Kamanda Tosi yeye ameweka misingi mizuri ya utendaji kazi pale. Itafika siku moja Kamanda Tosi atachoka. Kwa hiyo, tulichoweza kufanya ni kumwagiza yeye aweke taratibu nzuri ya kupambana na ujambazi. Kijana huyo ambaye tumempeleka *RPC* husika, anafanya kazi nzuri. Kwa hiyo, nasema tumpe nafasi na yeye pengine atafanya vizuri kama vile alivyofanya Kamanda Tosa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, nina masuala mawili yanahusiana na sera.

La kwanza, katika taratibu za Mawizara, tofauti ya nyongeza ya mshahara kila mwaka ambao huwa hausimami, lakini katika Jeshi la Polisi mtu akifikia cheo fulani na akabakia na cheo hicho kwa muda wa miaka mitatu au miaka sita, ile nyongeza inasimamishwa, huwa haiongezeki. Kitendo ambacho kinasababisha mwingine atakayeajiriwa labda mwenye *qualification* sawa sawa lakini yeye kapata nafasi kila mwaka anabadilisha vyeo au anakwenda masomoni, anabadilika anampita mshahara huyu aliyekaa muda mrefu sana ama mwenye *same level*. Ningeomba Waziri atufafanulie hapo. Halafu ikiwa tuna matatizo ya fedha na askari anapoomba likizo anaambiwa ajilipie nauli na mambo yake yote, akirejea ndiyo adai zile gharama zake. Sasa ikiwa akirejea ndiyo adai hizo fedha, zitapatikana wapi kama tatizo ni ugumu wa fedha; kwa nini asipewe pesa za likizo mwanzoni? Hilo ni suala la kwanza.

Suala la pili ...

**MWENYEKITI:** Suala la pili. La kwanza lilikuwa nyongeza ya mshahara, hili malipo ya likizo. Kwa hiyo, umemaliza.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii mambo ya pesa ilikuwa ni moja, sasa kunakuja mambo mengine kabisa.

**MWENYEKITI:** Hapana.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA R AIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kama ifuatavyo: Hata hivyo, sikuona mchango wake kwetu sisi, lakini naomba nilijibu swali hilo.

**MWENYEKITI**: Ulizungumzwa kwenye Hotuba ya Wapinzani.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Ahaa asante! Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa ni kwamba, kuhusu masuala haya ya kukaa muda mrefu, ingekuwa ni vyema ukatuandikia vizuri, ukatuletea mifano ili tuweze kulishughulikia jambo hili vizuri zaidi. Hapa si rahisi kuweza kugundua nani amekaa muda mrefu asipate fedha zake na kadhalika. Kwa hiyo, ninamwomba atuandikie ili tuweze kumpa majibu sahihi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la likizo. Utaratibu wetu ni kwamba, pesa za likizo zinalipwa si kutokana na utaratibu wa *cash bugdet* huu. Pesa za likizo zinalipwa kutokana na kwamba, mwezi ule ambao anakwenda likizo analipwa. Hivi sasa tunafanya utaratibu wa kuondoa tatizo hili la kulipwa kwa mwezi mwezi, kwa sababu mara nyingi askari hawa hupata likizo kila baada ya miaka mitatu na likizo yao huwa ni ya miezi mitatu. Kwa hiyo, inakuwa wanapata usumbufu mkubwa. Sasa hivi tunafanya utaratibu kwamba, anapokwenda likizo, fedha zote ziwe zimepatikana. Tulikuwa tunafanya utaratibu wa kulipwa mwezi mwezi kutokana na utaratibu wa *cash budget.* Lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunafanya marekebisho makubwa ili suala la kulipwa kwa pamoja liwezekane. Si kwamba analipwa baada ya kurudi likizo, analipwa katika miezi ile ile, lakini mwenyewe huwa hayupo na huwaachia wenzao wengine kuwachukulia, hapo hutokea tatizo kubwa sana.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilieleza utaratibu wa masharti ya utumishi katika Jeshi la Polisi na mafao yao baada ya kustaafu. Inaonekana kwamba, wale ambao waliweka Mkataba wao katika pensheni wanapostaafu wanapata fedha nyingi zaidi. Lakini wale walioingia katika masharti ya bahashishi, basi baada ya kustaafu wanapata fedha kidigo sana. Mheshimiwa Waziri, mara nyingi amekuwa akituambia hapa kwamba, utaratibu unfanywa ili kuwaweka askari polisi wanapostaafu katika masharti ya pensheni wote kwa pamoja. Sasa mimi nataka kujua ni lini utaratibu huu utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tuna utaratibu wa pensheni na *gratuity.* Utaratibu huu umewekwa makusudi kuweka mlango kwa wale ambao hawataki pensheni. Utaratibu wa pensheni na *gratuity* si wa

lazima ni wa kwako wewe mwenyewe askari kuamua utaratibu upi unautaka. Kwa wale askari ambao hawajafikia cheo cha Inspekta, ukishatumikia jeshi kwa miaka kumi na mbili, unaruhusiwa kuchagua eneo moja kati ya mawili haya. Kwa wale waliofikia cheo cha inspekta wakati wowote, moja kwa moja wanaingia katika mkataba wa pensheni. Suala hapa tunafikiri namna ya kupunguza muda sasa badala ya miaka kumi na mbili iwe chini zaidi ili mtu aweze kufanya maamuzi. Lakini kuufunga huu mlango mwingine ambao si wa lazima, unawafupishia fursa wale ambao hawako tayari kwenda kwenye pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko haya yanakuja kwa wale watu ambao waliamua huko nyuma kutokukaa katika Jeshi la Polisi kwa muda mrefu na baadae wakachukua utaratibu wa *gratuity.* Sasa walipoona nje kugumu, wakaendelea kufanya kazi mpaka pale walipoamua kustaafu na wenzao waliochukua pensheni, wakaona wenzao wamepata kiwango kikubwa kuliko wao. Ndiyo kwa kweli limekuwa tatizo kubwa sana. Lakini kulifungia mlango kabisa kabisa kwa sababu ni suala la uchaguzi, sioni kama kuna mantiki yoyote pale. Mtu ana uamuzi wake mwenyewe. Suala la lazima hapa ni kutoa elimu zaid kwa askari wakaelewa nini *gratuity*, nini pensheni, halafu wafanye maamuzi kuliko kufunga kabisa. Unaweza ukafunga kabisa lakini wale wengine wanaotaka fursa hiyo hawawezi kupata.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kuniona na mimi ni fungu hilo hilo - Mshahara wa Waziri, lakini sikusudii kuchukua mshahara wake kwa sababu atashindwa kunisaidia mahali ambapo nataka kuomba. Wakati nilipochangia kwa maandishi, niliomba suala langu la matatizo ya Wilaya ya Geita lichukuliwe kwa dharura. Nilieleza mwezi uliopita majambazi yaliua katika Kijiji cha Katoro. Majambazi yalivamia, yakaiba na yakaua. Wiki iliyopita nilipigiwa simu saa tisa za usiku, baada ya mawasiliano kuwa magumu nikampigia Afisa Usalama Wilaya ya Geita, ndiye aliyeenda kumtafuta *OCD* na kwa kuwa hakuna usafiri, wakahangaika baadaye wakawa wanapigiana simu watu wakakimbia, baadae wakaenda wakakuta majambazi yameondoka lakini yameua mtu mmoja. Jana wananchi baada ya kuona kwamba, majambazi yanazidi kuwatoroka, wakaamua kuua jambazi mmoja na matatizo haya yako majini na sehemu nyingi. Kwa sababu ya vyombo vya usafiri, nikaomba Mheshimiwa Waziri, anisaidie Wilaya ya Geita waione kama mahali ambapo kwa sababu ya mkusanyiko wa watu wengi, kuna watu karibu milioni moja, wapeleke angalau usafiri wa gari na pikipiki kuwasaidia wale askari.

La pili, nikaomba mgodi mkubwa sana pale ambao una-*attract* watu wengi kwenda pale, lakini kwa upande wa askari hausaidii. Angalau itumike nguvu ya kuwaambia basi watoe hata *Land Cruiser* moja kuwasaidia wale askari ili waweze kufanya kazi kwa sababu wanapopata matatizo ndipo wanapochemka. Lakini matatizo makubwa yanaletwa na ule mgodi. Ninaomba msaada huo.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba, Wilayani Geita ipo changamoto kubwa ya kiuchumi, kwa hiyo, matukio kama hayo ni lazima yatakuwepo. Ninapenda kumwahidi kwamba, punde tutakapopata magari, tutaweza kuwapatia gari moja pale. Lakini hivi karibuni tutapata pikipiki kama

170, basi Geita itakuwa ni moja ya Wilaya ambazo zitapatiwa pikipiki angalau moja kama sio mbili.

**MHE. YONO S. KEVELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi na huko nyuma niliwahi kuzungumzia kuhusu tatizo kubwa la Kituo cha Polisi katika Jimbo langu la Njombe Magharibi kwamba, hatuna hata kituo kimoja cha Polisi na bahati nzuri au mbaya ni kwamba, uhalifu pale umeshamiri tena wa kutumia silaha za moto hasa pale Ilembula. *RPC* wa Iringa ni shahidi yangu, amekwenda pale amekuta matatizo makubwa sana. S asa nataka Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi atanieleza nini kuhusu suala la kujenga Kituo cha Polisi pale Ilembula, kwa sababu Jimbo zima halina kituo hata kimoja na tuna Tarafa tatu; yaani Wanging'ombe, Mdandu na Imalinyi?

Sasa hivi anasema kwenye Sera kutakuwa na Polisi Kata, wakati sisi Tarafa zote tatu hatuna hata Kituo kimoja cha Polisi. Mbaya zaidi katika Wilaya ya Njombe wale Askari wanafanya katika mazingira magumu, hakuna gari hata moja na kama ipo ni mbovu. Kuna siku moja tulikuwa Saja kulikuwa kuna gari moja ambalo ni bovu kabisa. Sasa mimi nataka nipate ufafanuzi; kwa nini Kituo cha Polisi kisijengwe pale Ilembula, walau Jimbo langu liwe na Kituo kimoja cha Polisi? Hilo naomba ufafanuzi kwa sababu wananchi wangu wanapata shida sana, kwa sababu vigezo vyote vya kipolisi tumetimiza.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mahitaji ya usafiri pale Ilembula.

**MWENYEKITI:** Hapana, Ilembula Kituo cha Polisi, Njombe usafiri.

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Sasa anasema haya yote yamo katika Bajeti yetu Mwenyekiti, kwa hiyo, tutayatekeleza katika kipindi hiki cha fedha cha 2007/2008.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimwomba Mheshimiwa Waziri, anipatie ufafanuzi mbalimbali juu ya mambo yanayohusu madawa ya kulevya, pamoja na maelezo yake ya jumla, lakini ninapenda vilevile kupata maelezo ya haya nitakayoulizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii, kwa kuwakamata waharifu wengi wa madawa ya kulevya mipakani na sehemu nyingine na vilevile kwa kuharibu mashamba mengi ya bangi. Tuliwahi kusikia kuwa, majina ya vigogo wanaojihusiha na dawa za kulevya yanajulikana; na kwa kuwa mpaka hii leo wanaokamatwa ni wale wadogo wadogo tu sio vigogo, lakini kwa kuwa hadi hapa Bungeni baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, waliwahi kuonesha utayari wao kwa kushirikiana na Wizara hii ili kuwakamata wanaohusika na dawa za kulevya; kwa nini basi mpaka hii leo vigogo hao hawakamatwi au ndiyo inayosemekana kwamba, *syndicate* ya watu ambao si rahisi kuwakatama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshikuru Mheshimiwa Mbunge, kwa kutupa pongezi, pongezi zake tunazipokea. Nataka kumhakikishia kwamba, zoezi la kupambana na uhalifu wakiwemo wa daya za kulevya, linaendelea vizuri. Alitaja kwamba, wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliokuwa tayari kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ni kweli wapo waliojitokeza lakini kwa utaratibu ule ule wa siri kwamba, tusitaje wanaotoa siri, ndivyo ambavyo tunafanya na taarifa zao zimesaidia sana kukamata watu mbalimbali na hata hao anaowaita vigogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamekamatwa wakiwemo vigogo anaosema Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Hakuna kigogo mbele ya Sheria na yeye kama anamjua kigogo yeyote huko nje, tuko tayari kumchukulia hatua zinazofaa. *(Makofi)*

**MHE. ISSA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, lakini kwanza, natanguliza maneno mafupi: Kumekuwa na hofu ya Mheshimiwa Waziri katika maelezo yetu tuliyochangia kwa maandishi kwamba, maandishi hayo nadhani hakuyasoma. Katika mchango wangu wa maandishi, nilichangia kuhusu habari ya kijana aliyeachishwa kazi kwa njia ya utata na haki zake asizipate na mshahara mpaka leo ungali ukienda katika sehemu husika na askari huyo ni F. 4884 - Hassan Mohammed Abbas. Ninataka maelezo ya kina kuhusu habari ya kijana huyo.

La pili, nakumbuka Zanzibar imepata uhuru kwa kupindua na Bara imedai uhuru na imepata, lakini vijana wetu Maaskari wanaostaafu wanapata mateso sana wakati wa kudai haki zao za pensheni na viinua mgongo. Tatizo hili hasa linatokana na utaratibu mbovu ulikuweko kwenye kitengo cha mafaili, ambapo hata kufanya kazi kwa askari hapastahili kufanyiwa kazi kwa jinsi mafaili yalivyokaa. Ni mapema mno askari wetu kupata *TB* wanaofanya kazi pale na ndiyo upotevu wa mafaili unapotokea na haki zao zisipatikane. Naomba nipate ufafanuzi na maelezo kamili kuhusu masuala hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nafikiri la sera lile la pili, la kwanza kama tulivyoagiza, walete majibu kwa maandishi kusudi waingie ndani ya hayo mafaili ambayo hayaonekani. Jibu swali la pili tu.

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze kwa kutambua Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, ameyapongeza kwa nguvu zote na ni kweli ndiyo Mapinduzi yaliyowatoa wanyonge na kuwaweka huru. Ni kweli yanajitokeza matatizo katika suala zima la wastaafu kufuatilia haki zao. Kama tunavyosema, sasa hivi tunafanya maboresho katika Jeshi la Polisi, ikiwemo suala la kutatua matatizo haya ya wastaafu kupata haki zao. Lakini pia tuelewe kwamba, hili suala la wastaafu kupata hazi zao si suala la Idara ya Polisi tu, wastaafu wanatakiwa wapate haki zao kutokea Hazina. Sasa huko nako pia wakati mwingine kunakuwa na matatizo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika

maboresho ya Jeshi la Polisi, tunataka kuondosha kabisa utaratibu wa kuweka mafaili na kila kitu sasa kitawekwa katika kwenye mtandao wa kompyuta na mambo yote haya yatakamilika vizuri sana ili kuondoa matatizo haya. Nataka nimhakikishie si nia yetu kabisa kuwapa usumbufu askari wetu hasa waliotumikia nchi, tunawajali na tutaendelea kuwajali. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … … … … … Sh. 1,037,208,400
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … … … … …. Sh. 373,718,200
Kif. 1004 - *Public Safety and Security Monitoring* … Sh. 1,376,430,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Information, Education and Communication*...Sh.121,930,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, una swali? *(Kicheko)*

**WAZIRI FULANI:** Hapana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1006 - *Procurement Management Unit* … … … …Sh. 550,831 200
Kif. 2001 - *Police Main Force* … … … … … … … … Sh. 76,913,190,848
Kif. 2002 - *Police Marine* … … … … … … … … … Sh. 1,475,258,520
Kif. 2003 - *Railway Police Division* … …. …. … … … Sh. 409,921,309
Kif. 2004 - *Police Signals Branch* … … … … … … … Sh. 5,629,952,470
Kif. 2005 - *Police Zanzibar* … … … … … … ....... Sh. 10,147,057,130
Kif. 2006 - *Police Airwing* … … … … … … … … … ... Sh. 2,146,307,062
Kif. 2007 - *TAZARA Police* … … … … … … …. … ... Sh. 511,973,020
Kif. 2008 - *Field Force Unit* … … … … … … … … … Sh. 4,373,822,340
Kif. 2009 - *Traffic Police* … … … … … … … … … … Sh. 1,472,161,165
Kif. 2010 - *Police Airport* … … … … … … … … … … Sh. 477,551,597
Kif. 2011 - *Police Dog and Horses* … … … … … … … Sh. 578,753,110
Kif. 2012 - *DSM Special Zone* … … … … … … ….. Sh.8,910, 415,498
Kif. 3001 - *Police College Moshi* … … … … … …... Sh. 2,681,763121
Kif. 3002 - *Police College* … … … … … … … … … … Sh.1,289,617,630
Kif. 4001 - *Police Vehicles Maintanance Unit* … … … … Sh. 512,191,362
Kif. 5001 - *Police Medical Unit* … … … … … … … Sh. 1,783,949,898
Kif. 6001 - *Police Building Brigade* … … … … … … Sh. 2,367,568,300

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7001 - *Criminal Investigation Division* … … … …Sh. 13,093,665,900

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Programme 70, Kifungu 260500, *Item* 260500 - *Military Procurement Supplies and Services.*

Mnamo Novemba, 2006, nilitembelewa na wageni ambao walikuwa na matizo ya kesi za kubambikizwa, pamoja na mambo mengine ya ukiukwaji wa Haki za Binadamu. Nilimwandikia Waziri wa Usalama wa Raia na watu hao walionana na Naibu Waziri na yeye alilisitiza awaone halafu waandike baarua. Wakaandika wakapeleka vielelezo vyote. Kwa vile ni masuala mtambuka pia nikamwandikia Waziri wa Sheria na Katiba, ambaye nashukuru ali-*acknowledge at least* kupokea barua ya malalamiko yale.

Lakini Wizara ya Usalama wa Raia, haikufanya hivyo. Mpaka hivi sasa yale mambo kwa mfano ni suala la *double standards*, kuna mtu amevamiwa na majambazi, majambazi yamekamatwa yakapelekwa Polisi baadae kesi hiyo haijakwenda Mahakamani mpaka leo, *just* tu kwa sababu huyu mtu ni wa Chama cha Upinzani. Sasa hizi *double standards* hizi ambazo hazijachukuliwa hatua ziko nyingi.

Ninasikitika kidogo Mheshimiwa Waziri, aliposikia hii *issue* alitaka nimpelekee vielelezo wakati ambapo vielelezo alishapewa Naibu Waziri. Nasikitika kwa hilo, lakini Naibu Waziri analifahamu vizuri. S asa nataka anifafanulie je, hatua zitachukuliwa baada ya kumkumbusha hivi sasa baada ya mwaka mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruksa yako, natamka kwamba, hatua zitachuliwa kwa mujibu wa Sheria.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 7002 - *Stock Theft Prevention Unit* … … … … … … Sh.533,046,920

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 28 - Wizara ya Usalama wa Raia

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 1,169,500,000

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona na kunipa nafasi. *Subvote* 1003, Kifungu kidogo cha 6389 - *Construction of Office Buildings.*

Katika Kitabu hicho zimeoneshwa zimetengwa karibu takribani shilingi bilioni1.1. *Concern* yangu ni kwamba, tuna tatizo kubwa sana la mpaka wa Tanzania na Msumbiji kupitia Mukulu, mahali ambapo sasa Wizara ya Miundombinu wameanza kujenga daraja. Tumekuwa tukikamata wahalifu na Wasomali wengi wamekuwa wakiingia kupitia hapo, pana vurugu na shughuli zote za ujambazi zipo pale. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri, aniambie kama katika fungu hili la kufanya hizo *construction* ya ofisi; je, lile suala langu ambalo toka Bajeti ya mwaka jana nimekuwa nikilizungumza, fedha hii pia inahusisha na ujenzi wa ofisi hiyo kule mpakani na nilishapata barua yake akimwagiza *IGP* ashughulikie suala hilo?

**MWENYEKITI:** Yaani ni kwamba, hizi hela zitajenga huko Mukulu?

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hilo ni kweli tumekuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na Mheshimiwa Jenista Mhagama; na tatizo limekuwa ni Bajeti hatukuwa na fedha za kutosha kuweza kujenga kituo hicho mwaka huu wa fedha. Lakini napenda kumahikishia kwamba kwa mwaka ujao wa fedha tutafanya juu chini tuweze kujenga kituo hicho.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 - *Police Main Force* … … … … … … … Sh. 4,040,000,000

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante na nitakuwa *very short.* Katika moja ya maswali yangu hapa Bungeni, niliulizia kuhusu ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Kalinzi na Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, wanaangalia kutokana na mazingira maalum ya Kalinzi. Sasa nimeona kwamba, zimetengwa jumla ya shilingi milioni 550 za ujenzi wa vituo vya ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, *item* gani?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2001 - *Police Main Force* na *6303 - Rehabilitation of Police Buildings*.

**MWENYEKITI:** Hii inahusu Zanzibar.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** 6303 - *Rehabilitation of Police Buildings*.

**MWENYEKITI:** *Ok,* endelea.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Sasa pale kuna majengo ambayo Wananchi wa Kalinze walikuwa wanaomba yatumike kwa ajili ya Kituo cha Polisi. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri, wajaribu kuangalia kama wanaweza kuyakarabati yale majengo, akasema wataliangalia suala hili. Sasa sijui katika hizi shilingi milioni 550 Kituo hiki cha Polisi kipo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa eneo hili ni la ukarabati na najua Kalinzi, Mheshimiwa Zitto ameipigia kelele muda mrefu, tutafanya kila jitihada tuhakikishe tunakikarabati Kituo hiki ili huduma za kiaskari ziendelee katika eneo lile.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nipo kwenye kifungu hicho hicho.

**MWENYEKITI:** Kifungu hicho hicho kipi?

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 6303 - Ukarabati. Kuna kituo kilichoko Natroni, nadhani Waziri anakifahamu wananchi walikijenga mwaka 2003. Serikali imetoa shilingi milioni saba kwa ajili ya kupaua lakini haijamalizika, kila mwaka wanasema hatuna pesa, naomba kujua kama hizo fedha za kukarabati hicho Kituo zipo kwenye kifungu hiki?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Michael L. Laizer, analifahamu suala hili kwa kina, kwa sababu tuliomba *estimate* za Kituo hiki na zimefika. Tunamhakikishia katika Bajeti ya wakati huu, zimo humu na tutakijenga.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu 28, Kifungu kidogo 2001, *Item 6107 - Technical Equipments; Radios and Accessories.* Katika kuchangia kwa maandishi, nilisema kwamba, katika Kituo changu cha Polisi cha Bububu wamepata redio moja ambayo inakuwa ni ngumu kuwasiliana. Je, katika kipindi hiki wataongezewa *Radio Call* nyingine ili wapate kuwasiliana?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mara tutakapopata fedha na kununua *Radio Call* nyingine, namhakikishia Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa kwamba, Bububu tutapeleka *Radio Call*. Mpango huo tunao, ni suala la fedha, pale tutakapopata fedha tutafanya hivyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 – *Police Marine* ……………………….....….Sh. 42,500,000

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhonga S. Mhwanya, ulisimama kabla ya kusema, kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa kwanza, wewe utasimama tena. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. *Vote 28, Subvote 2002*, Kifungu kidogo 6108 - *Improvement of Marine Patrols*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Bajeti cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 22, alizungumzia *concern* yake kuhusu matatizo yanayotokea kwenye Bahari na Maziwa. Lakini uwezo wa Serikali wa kununua hizi *Boats* ni kwamba, haupo au bado Serikali haina uwezo. Kwa kipindi cha hivi karibuni, ndio tunasikia ajali nyingi zinavyotendeka hasa kati ya Pemba na Tanga, kati ya Unguja na Dar es Salaam, kuna vifo vingi vinatokea baharini kwa watu wanaopatwa na dhoruba. Sasa hizi shilingi milioni 42.5 za *Improvement of Marine Patrols*, hebu atufafanulie *improvement* hizo ni zipi na je, hazitoshi kununua *Boat* ambayo *at least* iwe na *out boat engine* ya *45 notes* ambazo zipo, ikaweza kufanya *patrol* kati ya Pemba na Tanga, Unguja na Dar es Salaam au kwenye Maziwa? Mheshimiwa Waziri, atufafanulie na kwa kiasi fulani atatueleza nini?

**MWENYEKITI:** Umeuliza kwamba, je, ndiyo hizi?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kwenye masuala ya kushughulikia masuala ya vyombo vya baharini, siyo katika pesa hizi anazozizungumzia Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kwa sababu ukitazama huko, nyuma, kwa kawaida Jeshi la Polisi kwenye maeneo ya *Other Charges* wanaweka vifungu vinavyoshughulikia kazi hiyo. Hizi ni zile *minor repair,* kwa ajili ya kushughulikia vyombo vyetu vya baharini.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. *Vote 28, Subvote 2002, Police Marine - 6108*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu niliambatanisha na taarifa mbalimbali kutoka Mkoa wa Kigoma, kuonesha hali ya uhalifu. Lakini vilevile kuna Vituo vya Polisi ambavyo viko Mwambao wa Ziwa, kuna hiyo Kalia, Sigunga, Kibirizi na Kagunga, ambapo ndio mpakani. Lakini hakuna boti kabisa kwa ajili ya kufanyia doria. Sasa katika hizi shilingi milioni 42.5, maeneo hayo yanaweza yakapatiwa boti ukizingatia hata Polisi wenyewe katika Vituo hawatoshi, lakini hata boti hakuna; je, tunaweza tukapata?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, labda mtumbwi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, fedha hizi ni za *repair* ndogo ndogo, hazijapangwa kwa ajili ya kununulia boti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli upo umuhimu wa kuwa na boti katika eneo hilo, lakini, sasa kutokana na ufinyu wa bajeti, hatukuweza kwa mwaka huu kununua boti kwa ajili ya eneo hilo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika kipindi cha mwaka ujao, tutafanya jitihada ya kutafuta boti ndogo kwa ajili ya eneo hilo. Kununua boti mpya kwa ajili ya shughuli za kufanyia doria, kunahitaji shilingi bilioni kumi kwa boti mpya ya kisasa kwa ajili ya kufanya shughuli hizo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira, aache tushughulikie. Suala la boti hizo ndogo

ndogo, kipindi cha mwaka wa fedha ujao, tutaliangalia suala hilo. Kwa sasa hivi, hizi ni pesa za *repair*, hatuwezi kuzibadilisha kwa mujibu wa utaratibu wake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Police Medical Unit*………………………..Sh. 265,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

## T A A R I F A

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitisha Makadirio ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa mwaka wa fedha 2007/2008, kifungu kwa kifungu, bila mabadiliko yoyote. Naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu liidhinishe makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Usalama wa Raia kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hatuna matangazo mengine, isipokuwa kuna mtu mmoja kaniandikia barua, anaomba Mwongozo wa Spika kwamba, wakati wa Kamati ya Matumizi, mbona mnasema maswali mawili, wakati wengine wanasema dakika tano?

Waheshimiwa Wabunge, kawaida kufuatana na Kanuni ni dakika tano. Ila inazuia hotuba, inataka ufafanuzi. Sasa kwa dakika tano ukizidi maswali mawili, wewe tayari umetuhutubia sisi na sisi hatutaki, ndiyo hivyo. Kwa hiyo, maswali mawili yanaendana na zile dakika tano. Kwa hiyo, ni dakika tano na ndio maana tunaweka kengele hapa na kugonga. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lazima nikubali kwamba, kadri siku zinavyokwenda, mnazidi kujifunza vizuri zaidi katika Kamati ya Matumizi. Kwa hiyo, tuendelee kujifunza kwa sababu tusipojifunza, tutafanya kama *pombe shop*, kumbe hapa ni rasmi kabisa. Kwa hiyo, mjifunze na nadhani inaenda vizuri.

Baada ya hapo, naomba niwashukuru, kwa siku ya leo tumefanya kazi nzuri. Naomba tuahirishe kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.33 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne, Tarehe 24 Julai, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*